



EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

UKRISTO NA UISLAMU: Mambo Muhimu—Sehemu ya Tatu

Mwandishi

Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Cornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders East Africa, Inc.
714 S. Summit St., Appleton, WI 54914
+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

Juni 2019; kimepitiwa Aprili 2020

Haya ni mafafanuzi ya Uislamu kutokana na mtazamo wa Kikristo na malinganisho ya mafundisho ya Kikristo na Kiislamu. Sehemu ya tatu inajumuisha majadiliano juu ya Yahweh na Allah na Biblia na Korani. Fundisho hili linahitimisha kwa kujadili njia ya kujenga daraja la kuunganisha ufa uliopo baina ya Uislamu na Injili, pamoja na kuitumia Korani na mafundisho yao kuwaelekeza Waislamu kwa Yesu Kristo. Nyongeza imeorodhesha mpangilio wa Kigeolojia ambao kwa huosura za Korani zilitolewa.

YALIYOMO

4. YAHWEH NA ALLAH

I. Utangulizi.....94

II. Kufanana baina ya Yahweh na Allah94

A. Sifa.....94

B. Matendo.....95

III. Tofauti kati ya Yahweh na Allah.....95

A. Yahweh na Allah: majina yao.....95

B. Yahweh na Allah: ujuzi wao.....96

C. Yahweh na Allah: mahusiano yao na wanadamu.....96

D. Yahweh na Allah: uaminifu wao.....98

E. Yahweh na Allah: tabia zao.....99

IV. Utatu.....100

A. Uislamu kwa usahihi unaukataa “utatu wa uongo” wa Allah, Yesu, na Mariamu.....100

B. Uptosshaji wa Kiislamu juu ya Utatu.....100

C. Maelezo juu ya fundisho la Utatu.....102

D. Ulazima wa fundisho la Utatu tunaupata kutokana na kweli tulizopewa kwenye Biblia.....102

E. Ingawaje hautaeleweka kwa ufasaha, Utatu siyo fumbo ni uhakika na wa kuelezeka.....104

F. Matokeo.....107

V. Yahweh na Allah: Hitimisho.....109

5. BIBLIA NA KORANI

I. Utangulizi.....109

II. Maendeleo ya Biblia.....109

III. Mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia.....110

IV. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia.....110

A. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu Korani inathibitisha uwepo wake, uhalisia wake, na kuaminika kwake.....111

B. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu Mohamedi anathibitisha uhalisia na kuaminika kwake.....114

C. Kwa sababu Yesu ni “mjumbe wa mapenzi ya nguvu” (Q. 46:35) na kuaminiwa kwenye unyofu wa Agano la Kale, Uislamu pia unapaswa kuamini unyofu wa Agano la Kale.....114

D. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu nakala nyingi za kabla na baada ya Mohamedi zipo na hazijabadilika.....115

E. Hakujawahi kutokea mtu aliyekusudia, aliyekuwa na msukumo, uwezo au nafasi ya kuiharibu Biblia hata kuthubutu kufanya hivyo.....116

F. Hitimisho.....117

V. Je Mohamedi alitabiriwa kwenye Biblia?.....117

A. Je Mohamedi ni “nabii” anayetajwa na Musa kwenye Kumb 18:15-19?.....117

B. Je Mohamedi ni “Msaidizi” anayetajwa na Yesu kwenye Yohana 14:16; 15:26; 16:7?.....120

C. Hitimisho.....122

VI. Maendeleo ya Korani.....123

A. Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetoka kwa Umar bin Al-Kattab au Uthman bin Afan.....123

B. Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetokana na matendo na desturi za kipagani.....123

C. Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetokana na maisha binafsi ya Mohamedi.....125

D. Ukusanyaji, marudio, na viwango vya Korani.....125

VII. Mkanganviko na makosa kwenye Korani.....129

A. Mkanganviko.....130

B. Makosa.....131

VIII. Fundisho la Kuondolewa.....	132
A. Fundisho la kuondolewa linapingana na maeneo mengine kwenye Korani na kuushambulia moja kwa moja unyofu wa Allah.....	133
B. Fundisho la kuondolewa linaifanya Korani isieleweke kwa mapana.....	133
C. Fundisho la kuondolewa lina madhara makubwa kwa kila anayedai kuwa Uislamu ni “dini ya amani”.....	133
D. Matatizo mengine ya fundisho la kuondolewa.....	134
IX. <u>Biblia na Korani: Hitimisho</u>.....	134
<u>6. KUUNGANISHA MGAWANYIKO BAINA YA UISLAMU NA INJILI</u>	
I. <u>Utangulizi</u>.....	135
II. <u>Masuala ya Jumla</u>.....	135
A. Kweli zinazowaongoza Waislamu kumgeukia Kristo.....	135
B. Kweli zinazowawezesha mashahidi wa Injili kwa Waislamu.....	137
III. <u>Kutumia Korani na desturi za Uislamu kuwaongoza Waislamu kwa Yesu Kristo na Injili</u>.....	139
A. Korani kama daraja: Mbinu za NGAMIA.....	139
B. Korani kama daraja: upeo mwingine wa mawasiliano.....	143
C. Tamaduni za Uislamu kama daraja: mpango wa wokovu wa Qurban.....	145
D. Tamaduni za Uislamu kama daraja: upeo mwingine wa mawasiliano.....	146
E. Kushughulikia maswali na malalamiko.....	149
IV. <u>Kuunganisha mgawanyiko baina ya Uislamu na Injili: Hitimisho</u>.....	150
NYONGEZA A—MPANGILIO WA KIJIOLOGIA WA SURA.....	151
ORODHA YA VYANZO.....	153
MWANDISHI.....	153

4. YAHWEH NA ALLAH

I. Utangulizi

Q. 29:46 (Hilali-Khan) anasema, “*Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja; nasi ni wajitupao Kwake (kama Waislamu).*” Vivyo hivyo, watu wengi, kwa sababu za kidini na za siasa ya kijamii, wanaamini kwamba Mungu wa Biblia (Yahweh) na Mungu wa Korani (Allah) ni mmoja. Hata hivyo, ingawaje ipo mifanano mingi kati ya Allah na Mungu wa Biblia, zipo pia tofauti za kina. Tofauti ni za kiutendaji vya kutosha kiasi kwamba hitimisho pekee la usawa ni hili, wakati Wakristo na Waislamu wote wanamwabudu Mungu mmoja, “Mungu wetu na Mungu wako” siyo wamoja.

II. Kufanana baina ya Yahweh na Allah

Kwakuwa wote wawili Ukristo na Uislamu wanashikilia kwamba yupo Mungu mmoja ambaye ni mtawala wa vyote, haikanushiki kwamba tabia nyingi za Mungu na Allah zaweza kuwa sawa hata kama wao siyo wamoja.

A. Sifa

Hadithi zinatueleza, “Mjumbe wa Allah alisema, ‘Allah anayo majina tisini na tisa, mia moja kasoro moja; na yeye atakayeyakariri hayo yote moyoni mwake ataingia Paradiso.’ Kuhesabu kitu maana yake ni kukijua kwa moyo.” (al-Bukhari: 7392; angalia pia 2736, 6410; Muslim: 2677a, b; at-Tirmidhi: 3506, 3508; Ibn Majah: 3860) Mchambuzi wa masuala ya Kiislamu ameyaorodhesha majina. Majina kimsingi huelezea tabia za Allah. Mengi ya majina hayo yanafanana na sifa za Yahweh ingawaje siyo Mungu yule yule:

JINA LA ALLAH NA NUKUU YA KORANI	SIFA MFANANO ZA KIBIBLIA ZA YAHWEH
2 AR-RAHMAN - (Mkarimu [i.e., Mwema]): Q. 1:3; 17:110; 19:58	Mwema – Kut 22:27; 34:6; 1 Pet 2:3
3 AR-RAHIM - (Mwenye Rehema): Q. 2:163; 3:31; 4:100	Mwenye Rehema – Kut 34:6; Kumb 4:31 Luke 6:36
4 AL-MALIK - (Bwana mtawala [au Mfalme]): Q. 20:114; 23:116; 59:23	Mtawala – Zab 103:19; Isa 43:15
5 AL-QUDDUS - (Mtakatifu): Q. 59:23; 62:1	Mtakatifu – Isa 6:3; 43:15; Ufu 4:8
9 AL-AZIZ - (Mwenye nguvu): Q. 3:6; 4:158; 9:40	Mwenye nguvua – Zab 50:1; 93:4; Luka 1:49
11 AL-MUTAKABBIR - (Mfalme): Q. 59:23	Mfalme – Ayubu 37:22; Zab 29:4; Waeb 8:1
12 AL-KHALIQ - (Mwumbaji): Q. 6:102; 13:16; 39:62	Mwumbaji – Mwanzo 1:1; Mhub 12:1; Warumi 1:25
15 AL-GHAFFAR - (Mwenye kusamehe): Q. 20:82; 38:66; 39:5	Mwenye kusamehe – Kut 34:7; Dan 9:9; Waef 4:32
20 AL-ALIM - (Mjuzi wa vyote): Q. 2:158; 3:92; 4:35	Mjuzi wa vyote – Ayubu 11:11; Zab 44:21; Matt 6:8
27 AS-SAMI - (Msikivu wa vyote): Q. 2:127; 8:17; 49:1	Msikivu wa vyote – Zab 34:17; 69:33; 1 Yohana 5:14-15
28 AL-BASIR - (Mweye kuona vyote): Q. 4:58; 17:1; 42:11	Mwenye kuona vyote – Mwanzo 16:13; 1 Sam 16:7; Math 6:4
29 AL-HAKAM - (Hakimu): Q. 22:69	Hakimu – Ayubu 21:22; Zab 7:8; Yohana 8:50
33 AL-HALIM - (Mvumilivu): Q. 2:255; 42:4	Mvumilivu – Warumi 3:25
37 AL-ALI - (Aliyetukuka): Q. 2:255; 4:34; 31:30	Aliyetukuka – Mwanzo 14:18-20; Hes 24:16; Matendo 7:48
39 AL-HAFIZ - (Mhifadhi): Q. 11:57; 34:21; 42:6	Mhifadhi – Zab 31:23; 36:6; 2 Pet 2:5
43 AL-KARIM - (Mkarimu): Q. 27:40; 82:6	Mkarimu – 1Nyak 29:14; Yak 1:5
47 AL-HAKEEM - (Mwenye hekima): Q. 2:129; 31:27; 46:2	Mwenye Hekima – Job 9:4; Isa 31:2; Warumi 16:27
48 AL-WADUD - (Mwenye upendo): Q. 11:90; 85:14	Mwenye upendo – Kut 34:6-7; 1 Nyak 16:34; 1 Yohana 4:7-8
49 AL-MAJEED - (Mtukufu): Q. 11:73	Mtukufu – Kut 24:16-17; Isa 3:8; 2 Wakor 3:18
52 AL-HAQQ - (Mkweli): Q. 6:62; 22:6; 23:116	Mkweli – Kut 34:6; 2 Sam 7:28; Warumi 1:25
57 AL-HAMEED - (Anayestahili sifa): Q. 14:1, 8; 31:12	Anayestahili sifa – Kumb 10:21; Zab 150:1-6; Warumi 15:11
63 AL-HAYEE - (Aliye Hai): Q. 2:255; 25:58; 40:65	Mungu Aishiye – Zab 42:2; Jer 10:10; 1 Tim 3:15
68 AS-SAMAD - (Wa milele): Q. 112:2	Wa milele – Mwanzo 21:33; Kumb 33:27; Warumi 16:26
73 AL-AWWAL - (Wa kwanza): Q. 57:3	Wa kwanza – Isa 41:4; 44:6; Ufu 1:8
74 AL-AAKHIR - (Wa mwisho): Q. 57:3	Wa mwisho – Isa 43:10; 44:6; Ufu 1:8
78 AL-MUTA'ALI - (Aliyeinuliwa sana): Q. 13:9	Aliyeinuliwa sana – Kut 15:1; Zab 97:9; Isa 6:1
81 AL-MUNTAQIM - (Mlipa kisasi): Q. 32:22; 43:41	Mlipa kisasi – Kumb 32:35; Warumi 12:19; Waeb 10:30
83 AR-RAOOF - (Mwenye huruma): Q. 3:30; 9:117	Mwenye huruma – Kut 34:6; Kumb 4:31; Yoel 2:13
93 AN-NOOR - (Nuru): Q. 24:35	Nuru – Zab 27:1; 2 Wakor 4:6; 1 Yohana 1:5

B. Matendo

Kwa kuwa wote wawili Ukristo na Uislamu hushikilia kwamba yupo Mungu mmoja pekee ambaye ni mtawala wa vyote haikanushiki kwamba mengi ya matendo ya Mungu na Allah yaweza kuwa mambo ingawa wao siyo wamoja. Baadhi ya yale yafananayo ni haya yafuatavyo:

- Aliumba mbingu na Nchi na vyote vilivyomo: “Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo” (**Kut 20:11**); “Na bila shaka Tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao kwenye nyakati sita, wala uchovu haukutugusa” (**Q. 50:38**).
- Alimwumba Adamu na kumpulizia uhai ndani yake: “Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai” (**Mwanzo 2:7**); “Kisha Akamsawazisha na Akampulizia roho Yake” (**Q. 32:9**).
- Anao mpango wa mwisho wa Dunia hii: “Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake. Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha kwenye pango na chini ya miamba ya milima, wakiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?” (**Ufu 6:14-17**); “Basi nyota zitakapopotezwa (nuru zao) Na mbingu zitakapopasuliwa, Na milima itakapovunjwa, Na Mitume watakapokusanywa kwenye wakati maalumu, Siku gani imewekwa ajali? Siku ya Hukumu. Na nini kitakujulisha siku ya hukumu ni nini? Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!” (**Q. 77:8-15**).
- Atahukumu kwa Haki: “Naye atahukumu ulimwengu kwa haki; Atawaamua watu kwa adili” (**Zab 9:8**); “Hapana hukumu ila kwa Mwenyezi Mungu, Anahadithia yaliyo kweli; Naye ni Mbora wa mahakimu.” (**Q. 6:57**, Sarwar).

III. Tofauti kati ya Yahweh na Allah

Bila kujali mfanano baina ya Yahweh na Allah, zipo tofauti za kina baina yao. Tofauti hizo ni msingi unaodhihirisha kwamba Yahweh na Allah siyo Mungu mmoja kwa vyovyote. Baadhi ya tofauti za muhimu ni hizi zifuatazo:

A. Yahweh na Allah: majina yao

Mungu alieleza majina yake halisi kwenye **Kut 3:13-15** kama “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Tena Mungu akamwambia Musa, Waambie wana wa Israeli maneno haya, Bwana, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenituma kwenu; hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu langu hata vizazi vyote.” “MIMI NIKO” kwa Kiebrabia ni YHWH, hutamkwa Yahweh, ambalo limetokana na kihusishi hayah (“kuwa” na “kuendelea”). “ni jina linaloeleza ukweli kwamba Mungu wakati wote yupo na atakuwepo wakati wote” (Ndjerareou 2006: 91).

“Allah” lilikuwa jina halisi la mungu wa Kipagani aliyeabudiwa na Waarabu wa kwanza Uislamu (angalia **Q. 29:61-65**; Gilchrist 1994: 4; Morey 1991: 45-53; Nehls na Eric 2009: 133; Shayesteh 2004: 36n.2; Schirmacher 2011: 11). Kwa sababu ya hili, Sundiata anaeleza “Hata kama neno ‘Allah’ ndilo jina pekee ambalo lingeeleza Mungu wa kweli kwa Kiarabu, ukweli kwamba lilikuwa na misingi na mahusiano na miungu ingemfanya Mungu wa kweli kujifunua mwenyewe kwa jinsi nyingine. . . . Unaweza kufikiri kwamba Mungu alimtuma Musa kwa Waisraeli wakati walingali Misri na akaruhusu jina ‘Ra,’ mungu jua wa Wa-misri, kwa mfano, kutumika kwa ajili Yake? Lakini hiki ndicho ambacho Mohamedi alichotaka kumwamini Mungu alifanya kwenye kusudi hili. Mohamedi alitutaka kuamini kwamba yeye aliyemtuma alikuwa Mungu wa kweli, lakini bado aliruhusu Mwenyewe kuitwa ‘Allah’ (linalomaanisha ‘mungu’)—jina la mungu wa Kipagani.” (Sundiata 2006: 311-12)

Kwa namna nyingine, “Allah” ni neno la kiarabu linalomaanisha “Mungu” (Gilchrist 1994: 4; Prince 2011: 4-5; Schirmacher 2011: 11). Kulingana na msomi wa Biblia na mpanga mbinu za umisheni Rick Brown, “jina la Kiarabu *Allâh* ni neno la kuasiliwa kutoka kwenye Kiaramaiki lenye maana ya Mungu, *Alâh* au *Alâhâ*” (Brown 2006d: 80). Maandishi wa zamani yanafunua kwamba Wakristo kabla ya wakati wa Uislamu walitumia neno Allah, tafsiri ya Waarabu –Wakristo ya maandiko kutoka karne ya saba mpaka sasa waliyaondoa matumizi ya Allah, na “hata leo, Allah ni neno la Kiarabu la Mungu ambalo ni la kawaida sana kutumiwa na Wayahudi na Wakristo” (Ibid.: 80-81; Fleenor 2005: 2-4; Greeson 2007: 110; Schirmacher 2011: 11; Thomas 2006: 171-74). Rick Brown anatukumbusha, “Maana ya neno ni utendaji wa jinsi gani watu walivyoamini na kulitumia kuonyesha vitu, siyo jinsi lilivyotumika hapo nyuma. . . . Kila jina linalomaanisha Mungu kwa mtu yeyote humkumbusha mtu huyo anavyofikiri juu ya Mungu. Kile kinachotakiwa ili kulibadilisha ni kupata habari mpya kumhusu Mungu ambazo zitabadilisha wazo lenyewe, na hili ni jukumu la Biblia. . . . Tatizo siyo jina lao kwa

Mungu lakini ni wazo lao kwa Mungu. Wazo la utakatifu, anayependa, linategemea utatu kutokana na matumizi ya mtazamo wa kidunia unaofunuliwa kwenye Biblia. Ni neno la Mungu, lililohuishwa na Roho mtakatifu na ushuhuda wa watakatifu, hilo laweza kumwongoza Muislamu kwenye wazo kamili la Mungu, bila kujali jina wanalolitia kwake.” (Brown 2006d: 81-82, fafanuzi imeongezwa) Hivyo, kama Muislamu akielewa tu neno “Allah” kwa Mungu, Wakristo wanapaswa waweze kulitumia neno hilo kwa ile asili halisi ya Mungu, kama lilivyofunuliwa kwenye Biblia, limewekwa wazi.¹

B. Yahweh na Allah: ujuzi wao

Mungu wa Biblia hupenda kujulikana. Yesu alisema, “*Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma*” (Yohana 17:3; anagalia pia Isa 11:9; Yer 9:23-24; 24:7; Hab 2:14). Yeye mwenyewe Mungu kwenye Yesu Kristo “*alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake*” (Yohana 1:14; angalia pia Waeb 1:1-2).

Tofauti na Mungu wa Biblia, haiwezekani kumjua Allah au hata anamaanisha nini kwa sifa zake. Q. 6:103 msemu wa Allah, “*Macho Hayamfikii, bali Yeye Anayafikia Macho; naye ni Latifu, Mwenye habari.*” Q. 42:11 anasema, “*hakuna cho chote mfano Wake*” (angalia pia Q. 42:1; 112:1-4). Kitengo cha utafiti cha Darussalam Publishers kinasema, “Tunalazimika kuamini sifa zote za Allah . . . bila . . . kuwalinganisha (kuwapa mfanano) kwa kila kiumbe. . . [Kulingana na Q. 42:11,] Aya hii ya kuheshimiwa inathibitisha sifa ya kusikia na kuona kwa Allah bila kumlinganisha/kumfananisha na kiumbe chochote kile.” (Darussalam 2002a: 227-28) Athari anamnukuu Imam Abu Hanifah kama alivyosema, “Hakuna mtu yeyote anayeweza kusema chochote kuhusiana na Roho ya Allah, badala yake wanaweza kumweleza Yeye kama Alivyojieleza Yeye mwenyewe. Hawaruhusiwi kumweleza Yeye kwa mawazo yao wenyewe kuhusiana na Yeye mwenyewe Allah.” (al-Athari 2005: 87) Maoni sambamba na hayo ya Mohamedi Asad, “Jaribio lolote la kumweleza Yeye au “sifa” zake kimantiki haiwezekani na, kutokana na mtazamo wa kimaadili, ni dhambi.” (Asad 1980: Q. 6:100n.88) Athari anaongeza kwamba Muumini wa kweli Muislamu “usijadili sifa za Allah zikoje, kwa sababu hajatueleza chochote kuhusiana naye”; hakika, “Hairuhusiwi kwa vyo vyote vile *au kujaribu kumfananisha jinsi gani Roho ya Allah ilivyo, au ni jinsi gani sifa zake zilivyo*” (al-Athari 2005: 77, 78n.3, fafanuzi imeongezwa).

Ingawa majina 99 ya Allah” hueleza sifa tofauti tofauti za Allah, Mwanazuoni wa Kiislamu anasisitiza kwamba hizi sifa *siyo sawa na sifa za mwanadamu*. Hivyo, Q. 16:74 (Hilali-Khan) inasema, “*Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu Anajua na ninyi hamjui.*” Shaikh Abdul-Aziz bin Abdullah bin Baz kwa kufanana anasema kwamba kumwamini Allah kunakulazimisha kuamini kwenye Jina lake na sifa zake lakini bila “kudai kwamba zinafanana na sifa za Mwanadamu” (bin Baz 2002: 254-55) Njia pekee ya kuzijua sifa kama vile rehema, upendo, msamaha, na ukarimu zilivyo ni kwa kujua kile ambacho watu Wenye rehema, wenye upendo, wenye kusamehe, na wakarimu walivyo au kile wanachokifanya. Hata hivyo, Kroni na Uislamu unakataza kabisa kila kitu kinachojaribu kuelewa Allah na Sifa zake yukoje au anafananaje. Vivyo hivyo, Sifa za Allah siyo lolote bali ni maneno yasiyokuwa na maana. Kwa wote Muislamu yeyote anayejua, sifa za Allah ni kumaanisha kupingana kabisa na maana za kawaida zinazoeleweka kwa maneno hayo.² Mtetezi Muislamu Yahiya Emerick alivyokiri, “Yeye [Allah] hakujifunua yeye mwenyewe kwa watu” (Emerick 2004: 49).

C. Yahweh na Allah: mahusiano yao na wanadamu

Mungu pekee aliongea nao na kuwabariki (Mwanzo 1:28-30). Yahweh wakati wote hupenda kuwa na mahusiano binafsi na watu. Hivyo, maelezo ya kujirudia kwenye Biblia yote (kwa namna tofauti) ni, “*Nitakuwa Mungu wao, na watakuwa watu wangu*” (angalia Mwanzo 17:8; Kut 6:7; 29:45; Walawi 26:12; Yer 7:23; 11:4; 24:7; 30:22; 31:1, 33; 32:38; Ezek 11:19-20; 14:10-11; 36:28; 37:23, 27; Hos 2:23; Zeka 8:8; 13:9; 2

¹ Georges Houssney anaonya kwamba “Matumizi ya Allah kwenye ushuhuda wa Wakristo na tafsiri ya Biblia ni mada ngumu. . . inastahili tu kusema kwamba ingawa Wakristo wanaozungumza Kiarabu hawana neno lingine zaidi ya Allah, haimaanishi moja kwa moja kwamba neno Allah linaweza kutumiwa kwenye lugha nyingine ya Uislamu. Kwa mfano, MuIrani mwenye kutokana na Waislamu alichagua *Khoda*, neno la Ki-Farsi likimaanisha Mungu, kwa sababu ‘Allah’ lina nukuu ya moja kwa moja ya Kiislamu kutoka kwao.” (Houssney 2010: 86n.9) Lester Fleenor anaongeza, “Mamillioni ya Wakristo wenye asili ya Ki-Arabu hawana tatizo kabisa kuomba kwa Mungu kwa jina lake la Kiarabu, Allah. Wanakubaliana kwa moyo wote na ushuhuda wa kiasi kwamba ‘hakuna mungu isipokuwa Allah,’ lakini huongeza kwa haraka ‘ndani ya Kristo.’” (Fleenor 2005: 4)

² Mchambuzi Muislamu Muhammad Madani alipendekeza hili wakati aliposema, “hakuna hata mmoja anayemiliki sifa kama Yey, wala hakuna chochote kinachofanana na Yeye kabisa. Ikiwa yoyote kati ya sifa zake kitapewa kiumbe kingine, *mfanano utakuwa tu kwenye istilahi iliyotumiwa, siyo kwenye kiini na ukweli wa maana ya sifa. . . Hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kulinganishwa na Allah kwa njia yoyote ile.*” (Madani 2005: 4:492, fafanuzi imeongezwa)

Wakor 6:16; Waeb 8:10; Ufu 21:3). Wakati Yesu aliporudi kwa Baba yake mbinguni, Alihakikisha kwamba mahusiano ya Mungu na wanadamu yatakuwa ya karibu kuliko ilivyowahi kuwa, aliahidi “*Sitawaacha ninyi yatima; najia kwenu*” (**Yohana 14:18**). Kwa hiyo, alimtuma Roho Mtakatifu kwa uhakika *kuishi ndani* ya watu na kuwa pamoja nao milele (**Yohana 14:16-17; angalia Matendo 2:1-4; 1 Wakor 3:16; Wagal 4:6**). Wale walioungana na Kristo kwa sasa “*wanaongozwa na Roho wa Mungu*” (**Warumi 8:12-17**).

Mungu hashughuliki na watu wake kama vile Bwana kwa watumwa wake lakini alianzisha moja kwa moja, mahusiano binafsi na sisi (**1 Wakor 1:9; 1 Yohana 1:3**). Yesu alisema, “*Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu*” (**Yohana 15:15**). Hata alituita sisi “*watoto wake*” na “*wana*” kuashiria kina cha mahusiano yake kwetu (angalia **Math 5:9; Yohana 1:12; 11:52; Wagal 3:26; 1 Yohana 3:1**). **Warumi 8:15** anaongeza, “*Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba!*” (angalia pia **Wagal 4:6**) “*Abba*” ni neno la Kiaramaiki linalomaanisha ukaribu, binafsi, mguso wa familia. Mtumwa haruhusiwi kumwita/kumtaja mkuu wa kaya/familia kwa cheo hiki (Vine, Unger, na White 1940: Abba). Kwa maneno mengine, Mungu aliwachukua watumwa na kuwasili kama wana kwa ukaribu, mahusiano binafsi ya mapenzi (**Warumi 8:23; Wagal 4:1-7; Waef 1:5**). Kwa kuwa sisi ni watoto wake, Mungu alitufanya kuwa warithi wa kila kitu (**Math 25:34; Waef 1:11, 14, 18; Wakol 1:12; 3:24; Waeb 9:15; Ufu 21:7**).

Kwenye Uislamu, hali ni tofauti kabisa. Kwenye Korani, watu wote, ikiwa ni pamoja na Yesu, Mohamedi, na manabii wengine, huitwa Watumwa wa Allah” (e.g., **Q. 2:23; 4:172; 14:31; 17:53; 25:63; 39:10, 53**). Njia pekee ambayo mtu yeyote anaweza kumfikia Allah ni kama mtumwa: “*Hakuna ye yote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Rahman hali yu mtumishi*” (**Q. 19:93**, Hilali-Khan). Lester Fleenor analitazama, “Uislamu wengi huamini kwamba ni heshima kuitwa mtumwa wa Mungu, kwa hiyo, mengi ya majina yao huanza na neno *Abd* ambalo kwa Kiarabu humaanisha mtumwa. . . . Haijalishi ni kwa kiwango gani cha uzuri majina hayo yanaweza kutamkwa, kwa ukweli mtumwa hana haki kama ilivyo kwa mwana au binti; na hana haki ya kurithi. . . . Mahusiano ya Baba na mwana ni tofauti sana na yale ya bwana na mtumwa.” (Fleenor 2005: 35-36)

Kinyume na Mungu kumtuma Roho mtakatifu kukaa ndani ya watu ili aweze kuwa na mahusiano binafsi ya moja kwa moja nao, Kitengo cha Utafiti cha Darussalam Publishers kinasema, “*Siyo kama ambavyo baadhi ya watu hufikiri kwamba Allah yupo kila mahali – hapa, pale na hata ndani ya maziwa ya mtu*” (Darusslam 2002a: 229). Muislam Isma’il Al-Faruqi anasema, “*Yeye [Allah] hakujionyesha Mwenyewe kwa yeyote kwa njia yoyote. Mungu aliyafunua mapenzi yake tu.*” (Al-Faruqi 1982: 47-48, alinukuu kwa Geisler na Saleeb 2002: 142). Abdul-Wahhab anasema kwamba “*Kwa habari ya Allah kuwa Aliyeinuliwa sana*” yeye ni “*Hafikiwi kwenye Ukuu wake*” (Abdul-Wahhab 2002: 148). George Braswell analiweka hili kama hivi, “*Uislamu wanafundisha kwamba mtu ni lazima awe na ujuzi wa sheria za Mungu, lakini hakuna hata mmoja mwenye ufahamu binafsi au uzoefu wa ujuzi wa Mungu. Mungu alifunua sheria zake, lakini hakujifunua Yeye Mwenyewe.*” (Braswell 2000: 21)

Georges Houssney anaeleza kwa kifupi kwamba tofauti za kimsingi baina ya Mungu wa Ukristo na Allah wa Uislamu: “*Uislamu na Ukristo kwa pamoja wanatambua ukamilifu wa Mungu, mamlaka yake na sifa za ufalme wake. Bado mawazo ya islamu kuhusu Mungu hupungukiwa na sifa moja kubwa sana kukaa ndani, U-baba wake, Upendo wake, na kujihusisha kwake na maisha yetu ya kila siku. Wakati sisi kama Wakristo ‘tunakaribia kiti cha neema kwa ujasiri,’ Uislamu hukikaribia kwa hofu na kutetemeka. Tofauti hii ina matokeo. Wakati Wakristo wanatamani kuwa na ushirika wa karibu sana na Mungu, Uislamu hawana tumaini hilo – au hata matarajio kwamba tumaini kama hilo laweza kuwepo. Kwa Uislamu, wazo la aina hii ya uhusiano na Allah siyo tu halieleweki, halikubaliki pia. Litaashiria kwamba Allah atajishusha mwenyewe kuhusiana moja kwa moja na wanadamu, jambo litakalo punguza utukufu wake. Mkristo aliyemwuliza Muislamu kama anayo ‘mahusiano binafsi’ na Mungu anauliza kuhusu kitu ambacho siyo tu kwamba hakiwezekani, lakini ni dhahaka.*” (Houssney 2010: 85) Hili ni lazima linagusa matendo ya watu na, muhimu zaidi, sababu au msukumo wa matendo hayo. Muislamu wa awali Daud Rahbar anahitimisha, “*Kwa Ukristo Upendo umekuwa kanuni muhimu ya msukumo wa utendaji wa haki. Kwa nini? Jibu ni rahisi. Kwa Ukristo Mungu ni, kabla ya jambo jingine lolote, Baba. Upendo wake unazidi Haki yake. Kwenye wazo la Kikorani kumwogopa Mungu kumekuwa kanuni-msukumo ya muhimu ya utendaji wa haki. Kwanini? . . . Jibu la kwanini msukumo- woga umeshinda kwenye Korani ni kwamba Mungu wa Korani ni, kabla ya mambo mengine yote, mhukumu mkali. Haki yake ni kutokutulia. Hatamsamehe yeyote lakini wale wanaomwamini na kutii amri zake. Atawaruhusu kujua kwenye ile siku ya hukumu kile walichokifanya.*” (Rahbar 1960: 179, fafanuzi kwenye asili)

D. *Yahweh na Allah: uaminifu wao*

Yesu alisema, “*Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima*” (Yohana 14:6). Ni Yeye yule “*jana na leo na milele*” (Waeb 13:8). Katika Yeye “*unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili*” (Wakol 2:9), na Yeye kwa kuwa ni “*mng’ao wa utukufu wake [Mungu]na chapa ya nafsi yake*” (Waeb 1:3). Tunajua kwamba wakati wote alikuwa mkweli kwa sababu Biblia na Korani vyote vinathibitisha kwamba Yesu hakutenda dhambi.³ Kwa nyongeza, kwa sababu Mungu ni Utatu, “*tunaweza kuamini kwamba Roho Mtakatifu hatuambia kitu ambacho kitapingana na kile Baba au Mwana akijuacho kwamba ni ukweli na kilicho bora kwa ajili yetu*” (Feinberg 2001: 442).

Haya pia siyo kweli kwa Allah. Kwanza, Allah “*aliondoa*” baadhi ya aya kwenye Korani kwa “*ufunuo*” uliokuja baadaye.” Korani yenyewe inalikiri hili (Q. 2:106; 13:38-39; Q. 16:101). Muislamu wa awali, Farooq Ibrahim, anajadili madhara ya kiutendaji ya fundisho la kuondolewa kama ilivyoenezwa kwa kuaminiwa na kukubalika kwa Allah na Korani: “*Wakati ambao Uislamu wa miaka ya 1980, na kuutafuta ukweli ndani ya Uislamu, Nilikutana na mambo mengi kwenye kuitetea Imani yangu. Mojawapo ilikuwa ni fundisho la ‘kuondolewa.’ . . . Nilijua kwamba kutegemeana na Wanazuoni wa Kiislamu, zipo orodha tofauti za aya zililoondolewa (*mansukh*), kama zilivyo zile ambazo ziliongezwa, aya zilizoongezwa (*naskh*). . . . Nilifikia mahali ambapo sitaitetea tena Korani kama tuliyo nayo leo kama ukweli mkamilifu wa ufunuo wa Allah. Hili linaleta mashaka kwa ukubalifu wa Korani ya sasa ya Kiarabu inayodaiwa kwamba ni kamilifu na ufunuo wa mwisho wa Allah.*” (Ibrahim n.d.: n.p.)

Pili, suala la uaminifu wa Allah ni la kina zaidi kuliko kutofautiana kwake kwenye kuondoa au kufuta aya mbali mbali kwenye Korani. Suala linaenda kwenye umuhimu wa tabia za Allah zenyewe. Allah alijiita mwenyewe “*mdanganyifu*.” Q. 3:54 inasema, “*Na (Mayahudi) walifanya hila, na Mwenyezi Mungu Akafanya hila, Na Mwenyezi Mungu ndiye bora wa wafanyao hila.*” Pickthall alitafsiri kishemu cha mwisho cha Q. 3:54 kama “*Allah ndiye mdanganyifu bora zaidi*; Arberrry alitafsiri hii kama “*m-bora kwenye hila.*” Asili ya neno ni *makr*, lenye msingi wake kwenye herufi Miim-Kaf-Ra. Kulingana na “*Jifunze Korani*” Tovuti ya kiislamu (ambayo hutupa kamusi mbali mbali za maneno) Miim-Kaf-Ra linamaanisha, “*Kuuzoelea udanganyifu, kuzoelea kukwepa, kutunga hila, kufanyia zoezi hila, kufanyia kazi sera, kuzoelea uhalifu*” (Study Quran n.d.: Miim-Kaf-Ra). Hii siyo aya pekee ambayo Allah alidanganya: “*Na Aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kwamba amekwisha potea, basi kwa ajili yake hutapata njia*” (Q. 4:88, Hilali-Khan); “*Wala haitawafalieni nasaha yangu ijapokuwa nataka kuwasihini, kama Mwenyezi Mungu Anataka kuwaangamizeni. Yeye ndiye Mola wenu; Na Kwake mtarejeshwa*” (Q. 11:34); “*Kisha Mwenyezi Mungu Anamwacha kupotea Amtakaye, na kumwongoza Amtakaye*” (Q. 14:4, Hilali-Khan); “*Ibilisi (Shetani) akasema: Mola wangu, kwa sababu umenihukumu kupotea, kwa yakini nitawapambia (upotevu) katika ardhi na hakika nitawapoteza wote.*” (Q. 15:39, Hilali-Khan); “*Hakika wao wanafanya hila, Nami pia nabuni hila dhidi ya hila zao.*” (Q. 86:15-16, Arberrry; angalia pia Q. 4:142; 7:16, 99; 8:30, 43-44; 9:115 (Hilali-Khan); 13:42; 27:50; 68:45). Q. 8:30 inasema, “*Na (kumbuka) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakufukuze; na wakafanya hila; na pia Mwenyezi Mungu Akafanya hila, na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wafanyao hila.*” Ibn Ishaq, Mohamedi’s early biographer, anaonyesha kwamba kile hasa anachokisema Allah ni kusema, “*Nimewahadaa kwa hila yangu iliyothabiti (Ibn Ishaq 1955: 323).*”

Mohamedi alitambua udanganyifu wa Allah, kama hadithi inavyoeleza, “*Nabii alikuwa akiomba na kusema: ‘Bwana wangu, nisaidie mimi na usiwasaidie wengine kinyume changu mimi, na unijalie mimi ushindi na usiwasaidie wengine wanishinde, panga hila kwa ajili yangu na usipange hila kinyume changu’ (at-Tirmidhi: 3551 [maneno kwa “hila” ni wamkur na tamkur kutoka kwenye chanzo kile kile tulichokijadili hapo juu]). Jochen Katz anaweka hitimisho la wazi kwa kusema: “Kama udanganyifu ni sehemu ya tabia ya Mungu wa Korani, ni kwa jinsi gani Uislamu wanaweza kuwa na ujasiri kwamba Mohamedi na Korani hawakuwa ‘wadanganyifu wengine wakuu’ kwa Allah (mdanganyifu mkuu) kwa kusudi la kuwapotosha mabilioni ya watu—yaani Uislamu? . . . Ni kwa msingi upi Uislamu wanaweza kuwa na ujasiri kwamba kile Allah anachowaeleza kwenye Korani ni cha kweli—kama Korani kwa vyovyote imetoka kwa Allah?” (Katz, “*Kupita wote*” n.d.: n.p.) Hali ni tofauti kwa Mungu wa Biblia. Yesu alijiita mwenyewe “*njia, kweli na uzima*” (Yohana 14:6). Aliyathibitisha hayo kwa tabia na unyoofu wa maisha yake yote. Hakuwahi kamwe kuondoa; kamwe hakudanganya. Ni wa kuaminiwa kwa sababu, tofauti na Allah, yeye ni “*yeye yule jana leo na hata milele*” (Waeb 13:8).*

E. *Yahweh na Allah: tabia zao*

Biblia inamwonyesha Mungu kama Mwumbaji pekee (Mwanzo 1:1; Isa 40:26) na mtawala (Dan 4:34-

³ 2 Kor 5:21; Waeb 4:15; 7:26; 1 Pet 2:22; 1 Yohana 3:5; Q. 19:19, 31.

35) wa vitu vyote, na ambaye “*ameinuliwa sana*” (Kut 15:1, 21; Zab 47:9; angalia pia Neh 9:5; Ayubu 36:22; 37:23; Zab 57:5, 11; 89:13, 24; 97:9; 99:2; 118:16; 148:13; Isa 6:1; 12:4; 33:5; 57:15). Hata hivyo, zipo sifa nyingine muhimu za asili ya Mungu na Utambulisho wake. Kujifunua Mwenyewe kwa Ukuu wa Yahweh kulikuja kwa Yesu Kristo pekee ambaye ni “*Mwakilishi halisi wa asili Yake*” (Waeb 1:3). Wafil 2:5-11 inaeleza ni jinsi gani Kristo alivyokuwa Mungu (2:5-6) lakini alijivua Mwenyewe na kuwa mwanadamu, hata mtumwa (2:7), na alikuwa mtii hata mauti ya msalaba (2:8); kwa hiyo, Mungu alimwadhimisha sana kiasi kwamba kila mmoja atamwabudu Yeye kama Bwana wa vyote (2:9-11; angalia pia Yohana 3:14-15; 8:28; 12:23, 32-34; 13:31-32; Ufu 4:2-5:14).

Mungu anaweza kujidhihirisha mwenyewe kwa hili linaloonekana kuwa njia iliyo kinyume kwa sababu “*Mungu ni Upendo*” (1 Yohana 4:8, 16). Udhahirisho wa hali ya juu kabisa wa Upendo huu umeandikwa kwenye Yohana 3:16: “*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele*” (angalia pia 1 Yohana 4:9-10). Mungu kwenye Upendo wa Kristo kwetu unazidi hata hayo kwa sababu, kama Warumi 5:7-8 inavyotukumbusha, “*Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi*” Kama Timothy Keller alivyoliweka, “Hapa tunaona nguvu wakati wote—Mungu ambaye anazo nguvu za kutosha kujitolea kuwa dhaifu na kujishusha mwenyewe hadi kwenye kuwa dhaifu Zaidi na giza kutokana na upendo wake kwetu. Na hapa tunauona uwezekano mkubwa wa utukufu mkuu—Utayari wa kuweka kando utukufu wake wote kutokana na upendo wake kwetu.” (Keller 2013: 120) Hakuna dini nyingine duniani yenye Mungu kama huyu. Hakika, “Hakuna dini nyingine kwamba hata iliwahi kufikiria jambo kama hili” (Ibid.).

Allah hayupo kama hivyo. Allah hawezi kujishusha mwenyewe kuwa mwanadamu kwa sababu, kama Q. 19:92 inavyosema, “*Wala haimpasi Rahmani kupanga mwana*” (angalia pia Q. 2:116; 10:68; 17:111; 18:4-5; 19:35, 88-89 [wazo hili ni “uovu”]; 23:91-92; 39:4 [“Yuko juu ya vitu hivi vyote”]; 43:81-82). Kwa Uislamu ni “kuushusha utukufu” wa Allah kuwa mwanadamu, kuteseka, na kufa kwa dhambi za ulimwengu kama Mungu alivyofanya pekee kwa Yesu (Emerick 2004: 46-47). Wakati moja kati ya majina 99 ya Allah ni “AL-WADUD” (“Anayependa”; angalia Q. 11:90; 85:14), “upendo” wa Allah una masharti; siyo wa kujidhabihu mwenyewe kwa upendo wa Mungu kupitia Kristo. Daud Rahbar alihitimisha, “Upendo wa Kiungu usio na sifa kwa mwanadamu ni wazo ambalo ni la kigeni kabisa kwenye Korani. . . . Hakuna mahali tunapopata wazo kwamba Mungu anapwapenda Wanadamu. Upendo wa Mungu una Masharti.” (Rahbar 1960: 172)⁴ Hivyo, hakuna mahali kwenye Korani panaposema kwamba “Allah ni Upendo” kama biblia inavyosema “Mungu ni Upendo.”

Tofauti kati ya asili za msingi au tabia za Yahweh na Allah zinaonekana kuwa zinafanana wakati mmoja anapoziangalia amri zake kuhusiana na kumpenda mwanadamu. Yesu aliulizwa, “*Mwalimu, kwenye torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, MPENDE BWANA MUNGU WAKO KWA MOYO WAKO WOTE, NA KWA ROHO YAKO YOTE, NA KWA AKILI ZAKO ZOTE. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO. Kwenye amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii*” (Math 22:36-40; angalia pia Marko 12:28-31) Yesu alisema kwamba hata watu wanapaswa “*Wapende adui zako na waombe wale wanaokuudhi*” (Math 5:44). Biblia imeliweka wazi kwamba kumpenda Mungu na kuwapenda watu wengine vimeunganishwa kwa karibu sana (angalia 1 Yohana 4:7-21). Allah wa Korani na sheria zake wanapingana na kile Yesu alichokiita “amri kuu mbili.” Kwanza, “Korani haijaagiza kumpenda Mungu. Hii ni kwa sababu Mungu mwenyewe hupenda wale tu ambao wanaamini na kwa ukamilifu kuzitii amri za Allah” (Rahbar 1960: 180). Kwa kweli, kwa kuwa Allah hajulikani “basi kumpenda hakuna maswali, kwa sababu haiwezekani kupenda kitu au mtu ambaye huwezi kumjua” (Sundiata 2006: 427). Pili, hakuna mahali ambapo Allah aliwaambia watu “kumpenda majira jirani kama wewe mwenyewe,” achilia mbali “kuwapenda maadui.” Badala yake, Allah amewaamuru Uislamu *wasichukuliane* na wasioamini, hata ndugu zao wenyewe, kama marafiki (Q. 3:28, 118; 4:89, 144; 5:51; 9:23). Uislamu wanapaswa kuwa “*wakorofi kwa wasioamini, na kurehemiana wenyewe kwa wenyewe*” (Q. 48:29, Hilali-Khan; angalia pia Q. 5:54; 66:9) na kupigana vita na kuwaua maadui zao na wale wasiokuwa Uislamu kwa ujumla (Q. 2:191; 4:89; 9:5, 29, 123, 193). Asili isiyo na shuruti na kiini kamili cha Upendo wa Yahweh, na tofauti wa karibu uliwekwa na vithaminisho vilivyonyeshwa hadharani na amri za Allah kulazimisha hitimisho kwamba Yahweh na Allah wanazo tabia mbili tofauti za wazi. Kwa hiyo, siyo wamoja na hawawezi kuwa Mungu yule yule.

⁴ Rahbar pia anaonyesha kwamba tafsiri ya “‘kupenda’ ni msemu wenye nguvu kulichukulia wazo la ahabba [neni la msingi lililotafsiriwa kama ‘upendo’ kwenye Korani] ambalo laweza kuchukuliwa sawa kama ‘kufanana au kukubali’” (Rahbar 1960: 172). Aliongeza kwamba, kwenye majina 99 ya Allah, “jina la utani (epithet) ‘kupenda’ bila shaka ni neno linalomaanisha Upendo wa Mungu kwa waamini walio wema” (Ibid.: 175).

IV. Utatu

Bila shaka tofauti kubwa baina ya Mungu wa Biblia na Allah wa Korani ni fundisho la Wakristo la Utatu, i.e., kwamba yupo Mungu mmoja tu, lakini amefanywa na watu watatu : Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Korani kwa uwazi inakataa Utatu. Waislamu wanaamin kwamba wazo la Utatu ni muundo wa kuongeza “washiriki-wenza” kwa Mungu; hivyo, inaongeza muundo wa *shirk* au kuabudu miungu wengi, i.e., miungu watatu. **Q. 4:171** inasema, “*Enyi watu wa Kitabu! msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli; Masihi Isa bin Mariamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno Lake tu Alilompelekea Mariamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake; wala msiseme Utatu, jizuieni, itakuwa bora kwenu; bila shaka Allah ni Allah mmoja tu. Utukufu uwe juu yake*”

Alhaj A. D. Ajijola ni aina ya mtetezi Muislamu ambaye alishambulia wazo la Utatu wakati aliposema, “Yesu alikuwa anatafuta kuyatimiza mahitaji ya Mwanadamu. Hatimaye, kama aina za Ukristo zilivyovyoundelea, maadui walimpigilia misumari hadi kufa. Mtu mwenye ukomo kitabia kama ambayo Biblia yenyewe imemwonyesha Yesu kuwa nao, anaweza kuwa Mungu wa Kweli?” (Ajijola 1972: 27) Kwa kweli, kwa sababu Mungu ni Utatu, Mungu kwenye utu wa Mwana (Yesu) hakika anaweza kuuvaa mwili na mwenye ukomo kama mwanadamu na bado akaendelea kubaki kama Mungu. Vivyo hivyo, Yesu anaweza kufa kama mwanadamu na bado akaendelea kuishi kama Mungu (ambaye hawezi kufa). Kifo hakimaanishi kwamba mtu anakoma kuishi; badala yake, inaathiri kutenganishwa kwa roho kutoka kwenye mwili. Sam Shamoun anaeleza, “Mungu mmoja wa kweli wakati wote hudumu kama watu watatu hata wakati wa maziko ya mwili wa Kristo. Na hata mwili wake ulipokuwa umelazwa kaburini, Kristo alikuwa hai na kwenye mamlaka akiundeleza Ulimwengu akiwa na Baba na Roho Mtakatifu.” (Shamoun, “Kama Yesu” n.d.: n.p.) Kama tulivyojadili hapo awali, kwenye muungano huu wa ajabu wa Mungu na mwanadamu kwenye utu wa Yesu ulimwezesha Mungu kuhusika na kuistahimili adhabu ya Kiroho ya dhambi za mwanadamu pale msalabani.

Kwa kuatafakari Utatu, tutajadili kwanza ni jinsi gani Uislamu ulivyo sahihi kuukataa “utatu wa uongo”; pili, tutatafakari misingi ya upotofu au tafsiri mbovu ya Kiislamu ya Utatu; tatu, tutaonyesha jinsi ambavyo wazo la Utatu lilivyo inuka wazi wazi kwenye Biblia; nne, tutajaribu kuonyesha ni jinsi ambavyo wazo la Utatu siyo la kisayansi au lisilo leweka kama mtu anavyoweza kufikiri; na tano, tutatafakari baadhi ya matokeo ya fundisho.

A. Uislamu kwa usahihi unaukataa “utatu wa uongo” wa Allah, Yesu, na Mariamu

Q. 5:116-17 inaeleza “Utatu” kama ilivyohusishwa Allah, Yesu, na Mariamu: “*Na Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Isa bin Mariam! je, wewe uliwaambia watu: Nishikeni mimi na mama yangu kuwa waungu wawili badala ya Mwenyezi Mungu? Atasema: Wewe ndiwe Mtakatifu, hainipasi mimi kusema ambayo sina haki (ya kusema); kama ningalisema bila shaka Ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyomo nafsini Mwako; hakika wewe ndiwe Ujuaye sana mambo ya ghaibu.*” Hili linaashiria kwamba Mohamedi na Korani hawaelewi kiuhalisia kile Wakristo wanachokiamini na wahusika kwenye Utatu. Kwakuwa Korani inakosea kuelezea kanuni za msingi wa Imani ya Kikristo, Korani haiwezi kuwa ya asili ya Kiungu (kwakuwa kama Allah angekuwa Mungu, angalau kwa kiasi angeelewa na kwa usahihi kuelezea kile ambacho Wakristo kwa ukweli wanakiamini). Kwa kiwango kwamba Korani inahukumu kumwabudu Mariamu kama mungu au kama mtu kwenye Utatu, waamini wote wa Kikristo wameunganishwa kwenye hukumu hiyo ambayo haijawahi kuwa sehemu ya Imani ya Kikristo.

B. Upotoshaji wa Kiislamu juu ya Utatu

Msingi wa nafasi ya Uislamu hauishii tu kushambulia “utatu wa uongo” wa Mungu, Yesu, na Mariamu, lakini hushambulia fundisho la Utatu kwenye muundo wowote (angalia **Q. 4:171; 5:72-73**). Dirks aliposema kwamba msingi wa ukiri wa Kiislamu kwamba Allah ni “Mungu mmoja” unamaanisha “siyo tu kwamba Allah ni Mmoja bila wa kufanana naye na bila kuwa na mshiriki kwenye Utawala. Ni Mmoja pia kwenye Umoja wake. Umoja wake haumtambui na haumruhusu Mwenza wala Mshirika. Umoja wake hauruhusu nafasi kwa wazo lolote la Utatu wa Kiungu.” (Dirks 2008: 180) Uislamu unashindwa kuwasilisha ukweli wa Utatu wa Ukristo kwa njia muhimu mbili:

- *Korani haipo sahihi inapodai kwamba Wakristo wanasema, “Allah ni Kristo.” Q. 5:72 inasema, “Bila shaka wamekufuru wale waliosema, Hakika Allah ni Kristo bin Mariamu,”* (angalia pia **Q. 5:17**). Kama tulivyoona hapo juu, “Wengi wa Wakristo wazungumzao Kiarabu—na Waislamu sawa na Wakristo waliokulia huko—hutumia ‘Allah’ kama kiwakilishi cha Mungu” (Schirmacher 2011: 11; angalia pia Fleenor 2005: 2-4). Vivyo hivyo, kama Sundiata alivyoonesha, “kwenye ufahamu wa Wakristo, Allah litakuwa sawa na ‘Utatu’ au Mungu wa Utatu, siyo Kristo. Kwa hiyo ni kosa kwa Korani kudai kwamba

Wakristo wanaamini kwamba ‘Allah ni Yesu mwana wa Mariamu’—hatuamini hivyo.” (Sundiata 2006: 184; angalia pia Reynolds 2018: 194 [“Tangazo (mst. 17; cf. 5:72) ‘Mungu ni Masihi’ halikuwahi kusemwa na Wakristo (wao husema ‘Kristo ni Mungu’ lakini siyo ‘Mungu ni Kristo’).”])

- *Korani haipo sahihi inapodai kwamba Utatu huongeza “kuwaabudu miungu watatu” au “kuunganisha miungu wengine au washiriki wenza kwa Allah.” Q. 5:72-73 inasema, “Kwa yakini anayemshirikisha Allah, hakika Allah Amemharimishia Pepo, na mahali pake ni Motoni; na wadhalimu hawatakuwa na wasaidizi. . . . Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: Hakika Allah ni watatu wa Utatu, hali hakuna mungu ila mungu mmoja.”* Korani huwawakilisha kwa makosa Wakristo kama “kuunganisha miungu mingine na Allah” na kama kumwabudu Allah kama mmoja wa miungu hiyo mitatu, i.e., kuamini kwenye utatu. Maelezo hayo yana msingi wa kanuni za uongo. Fundisho la Utatu lilikuwepo kwa karne nyingi kabla ya Mohamedi na halikuwahi kubadilika. Wakristo siyo kwa sasa na kamwe hawakuwahi kuamini kwenye miungu mitatu. Vyote viwili Agano la Kale na Agano Jipya kwa msisitizo na kwa kurudia hueneza kwamba yupo Mungu mmoja pekee (**Kumb 4:35, 39; 6:4; 32:39; 1 Wafal 8:59-60; Zab 86:10; Isa 43:10-13; 44:6; 45:14, 18, 21-22; 46:9; Marko 12:29, 32; Yohana 17:3; Warumi 3:29-30; 1 Wakor 8:4; Waef 4:3-6; 1 Tim 2:5; Yak 2:19**).

Utatu siyo tangazo kwamba kuna miungu watatu au kwamba Mungu Mmoja anao washiriki wawili; badala yake, Utatu ni tangazo la *umoja* wa Mungu—lakini umoja ambao unafika mbali zaidi na mgumu zaidi ya wazo la dhaifu la umoja wa Allah wa Uislamu: “Mungu wa Biblia SIYO sehemu ya utatu, kama ambavyo kwa makosa Korani inaashiria; baadala yake, Mungu Mwenyewe ni Utatu, ambao ni maelezo ya uhusika wa uwepo wa Mungu kwenye kiwango chake cha Uungu. Kosa la Korani hapa lipo wazi. Ni kwenye kujichanganya huku kunakofanya kutokuwezekana kwa Uislamu kutofautisha kati ya miungu watatu na fundisho la Utatu.” (Sundiata 2006: 183-84)⁵

Uislamu kutokuweza kutafakari Utatu kama kitu kingine chochote zaidi ya miungu mitatu huanzia kutokana na sababu mbili zinazohusiana: (1) mtazamo wake kwamba Kristo ni mwanadamu wa kawaida tu, na (2) mtazamo finyu wa “umoja” wa Allah. Mitazamo hii hupelekea hitimisho la uongo kwamba wazo la Wakristo la Utatu ni lazima lishirikishe “kumuongezea Mungu wenzi.”

- *Mtazamo wa uongo wa Uislamu kwa Kristo hupelekea hitimisho la uongo kwamba Utatu unahusika na “kumuongezea Mungu wenza.”* Uislamu humtazama Kristo kama mtu wa kawaida tu; wao basi hudai kwamba Wakristo humwinua Yeye kwenye Uungu pamoja na Allah (sawa na wazo la kutokuamini lililo kwenye **Q. 5:116-17** kwamba Mariamu aliinuliwa kwenye Uungu). Wazo kwamba Kristo ni mwanadamu wa *kawaida tu* ni la uongo. Wakristo “hawakumwinua Yeye kwenye Uungu”; badala yake, Yeye ni, na wakati wote atakuwa ni Mungu. Kwakuwa Kristo ni, na wakati wote amekuwa ni Mungu na yupo Mungu mmoja pekee, Wakristo kumwabudu Kristo haimaanishi “kumuongezea Mungu wenzi.”

- *Wazo dhaifu la Uislamu la “umoja” wa Mungu linapelekea hitimisho la uongo kwamba Utatu hulinganishwa na “miungu watatu.”* Kukubaliana na mtazamo wao dhaifu juu ya “umoja” wa Mungu. Mara nyingi Uislamu huunda sentensi kama vile, “wakati mtoto wa elimu ya awali anajua kwamba $1+1+1=3$, Wakristo kwa Utatu, huamini kwamba $1+1+1=1$ ” (Sundiata 2006: 195). Ulinganisho huu wa kimahesabu ni *ulinganisho wa uongo* kwa Utatu. *Huchukulia mbeleni* kwamba watu watatu wa Utatu ni miungu watatu (au miungu mmoja mwenye washiriki wawili). Halitolei maelezo kwamba “*Mungu ni Roho*” (**Yohana 4:24**), na Roho hawezi kugawanywa kwenye visehemu. “Kwanini ni lazima tatizo la shule yao ya awali lianze kama $1+1+1$ badala ya $1 \times 1 \times 1$ [au, kwa suala hilo, $1 \div 1 \div 1$]? Kwanini iwe ni kujumlisha badala ya kuzidisha? Zaidi sana, kwanini hesabu za namba moja (1) ziwe ndizo maelezo ya hesabu ambazo zinawakilisha Mungu? Kama kila namba ya hesabu inaweza kuwakilisha wazo la Wakristo kumhusu Mungu, litakuwa la milele! Na kama tujuavyo, milele x milele x milele = milele, na milele + milele + milele = milele, kama vile Mungu x Mungu x Mungu = Mungu, na Mungu + Mungu + Mungu = Mungu.” (Ibid.: 196) W. A. Pratney anaongeza, “Umoja wa Uungu siyo muungano wa kawaida au Muungano rahisi lakini ni Umoja unaotegemeana. Kuelezea kimahesabu haiwezekani kamwe kuwa $1 + 1 + 1 = 1$, kwa Muungano huru hauwezi kamwe kutupa usawa wa kweli; lakini $1 \times 1 \times 1 = 1$, kwa muungano unaotegemeana unatupa majibu sahihi na ya usawa, na kuondolewa kwa sehemu moja au muungano huo unaotegemeana hupelekea kupotea kwa zao lote ($1 \times 1 \times 0 = 0$).” (Pratney 1988: 261)

C. Maelezo juu ya fundisho la Utatu

Mungu ni kiumbe kigumu tofauti na kitu kingine chochote na ni tofauti na kitu chochote ambacho

⁵ Sundiata anaangazia, “Kama Korani ni kile ambacho Uislamu wanadai kuwa, basi angalau ingeziwakilisha kweli sahihi za kile Wakristo wanachokiamini kuhusu Mungu kabla ya kuyahukumu. Ni jinsi gani Uislamu unavyoweza kudai kuendelea Zaidi ya Ukristo wakati hauwezi hata kulielewa fundisho la msingi la Ukristo kwa usahihi?” (Sundiata 2006: 185)

chaweza kufikiriwa na kuotwa na mwanadamu mwenye ufahamu wenye ukomo. Fundisho la Utatu ni jitihada za kufahamu au kuelezea asili ya Mungu ambaye kwa asili yake halisi ni wa kipekee na Zaidi ya uwezo wetu wenye ukomo kumfahamu na kumwelezea ipasavyo. “Wakati wote Wakristo huamini kulingana na maandiko yao, kwamba Mungu hudumu kama Mungu wa Utatu. Hili siyo jambo ambalo Wakristo wameliumba au kulasili kutoka kwenye chanzo kingine—ni fundisho tunalolishikilia kama matokeo ya Ufu wa Kiungu. Itakuwa rahisi Zaidi kwenda na wazo la Kiislamu la Allah kama kiumbe pekee kisichoonekana (ambacho kina mizizi yake kwenye Upagani wa Kiarabu) kuliko kutamka fundisho la Utatu. Lakini ‘wazo rahisi’ hilo siyo la kweli siyo tu kwamba halistahili bali ni la hatari, kwa sababu kama litaendeleza mtazamo Hasi wa Mungu, Uumbaji wake, Makusudi yake, na mwelekeo wa mwanadamu. Kama ni rahisi kumwona mungu wako, basi upo uwezekano mkubwa kwamba wewe au mababu zako mlimwumba mungu huyo.” (Sundiata 2006: 181)

“Imeelezwa kwa kifupi, fundisho la Utatu linadai kwamba Mungu ni Mmoja kama kwa Roho [Kigiriki = *ousia*] na tatu kama kwa mtu [Kigiriki = *hypostasis*]” (Feinberg 2001: 437). Ghabril anaeleza, “Nafsi ya Mungu siyo vitu bali ni Roho. Roho haiwi chini ya mazingira yoyote, kuruhusu mgawanyiko. Hivyo Baba, na Mwana na Roho mtakatifu huheshimiana kwenye *hypostasis* yao kwa Nafsi ile ile. Kila mmoja hufurahia Nafsi ya Uungu mmoja bila mgawanyiko wala mfarakano. Kwenye lugha yetu hatuna ulinganifu wa maana ya *hypostasis* ili iwe rahisi kuelezea Utatu Mtakatifikwa urahisi zaidi.” (Ghabril 2003: 39) Cornelius Van Till anaongeza, “Kwa Mungu moja na nyingi wakati wote ni sawa. Umoja katika Mungu siyo wa Msingi kuliko utofauti, na Utofauti katika Mungu siyo wa Msingi kuliko Umoja. Watu wa Utatu ni wa karibu sana kwa mmoja na mwingine. Mwana na Roho wapo kwenye asili ya kuwepo au kuwa] kwenye usawa na Baba.” (Van Til 1979: 25) Mahali pengine alisema, “Wakati maandiko yanapoelezea kazi Fulani maalum kwa Baba, nyingine maalum kwa Mwana, na bado nyingine maalum kwa Roho Mtakatifu, tunawiwa kukubali uhalisia wa tofauti kati ya Uungu kuturudisha kwenye utambuzi. Kwa maneno mengine, kazi iliyoelekezwa kwa mtu yeyote yule ni kazi ya mtu huyo moja kwa moja.” (Van Til 1974: 228)

Kama kwa hili la mwisho, John Feinberg anaeleza: “Kwakuwa ipo Nafsi moja tu ya Kiungu inayoshirikisha kwa usawa kwa watu wote watatu, ipo busara ambayo watu wote watatu ‘hufanya’ chochote kile mmoja wao anachokifanya. Kwa namna nyingine, kwa jinsi hiyo kama inavyofanya kwa kila mmoja kuzungumza kwa mtu tofauti, i.e., njia tofauti ambazo kwamba Nafsi ya Kiungu hujidhihirisha, pia huifanya Nafsi kuashiria tendo maalum kwa mmoja tu kati ya hao watatu. Hivyo, ni mjumbe wa pili wa Uungu (siyo wengine) aliyeuvaa mwili wa mwanadamu na kuwa Yesu wa Nazarethi, yaani Kristo. Kama ilikuwa ni Roho ya Uungu pekee yake (hatukupanga hiyo Nafsi kama mbadala wa mtu maalum kwenye Uungu) kwamba alikuja kuuvaa mwili wa mwanadamu kama Yesu Kristo, basi tungeweza kusema kwamba wahusika wote wa Uungu walikuja kuuvaa mwili wa mwanadamu ndani ya Kristo.” (Feinberg 2001: fafanuzi imeongezwa)

D. Ulazima wa fundisho la Utatu tunaupata kutokana na kweli tulizopewa kwenye Biblia

Lester Fleenor anaonyesha, “Kama lilivyo neno la Uislamu la ‘Tawheed’ (linaloelezea fundisho la Umoja wa Mungu) halipatikani kwenye Korani, hivyo pia Neno la Kikristo la ‘Utatu’ (linaloelezea fundisho la Asili ya Mungu mmoja kwenye Utatu [muungano wa watu watatu]) halipatikani kwenye Biblia. Wazo la Tawheed msingi wake ni mafundisho ya Korani na siyo neno ‘Tawheed lenyewe; na wazo la Utatu msingi wake ni kwenye mafundisho yapatikanayo kwenye Biblia yote, lakini siyo kwenye neno ‘Utatu.’” (Fleenor 2005: 174)

Tumekwisha kulijadili mara nyingi na kwa uwazi kwamba Biblia kwa wazi na kwa kurudia imethibitisha kwamba yupo “Mungu mmoja tu.” Hata hivyo, kama W. A. Pratney alivyoonyesha, “kuna aina mbili za muungano au ‘umoja’ kwenye Kiingereza na Kiebrania; *umoja uliokamilika* na *umoja wa vitu*. Umoja uliokamilika ni ule wa kitu kimoja tu; Ninakupa chungwa moja, na unapata chungwa moja. Lakini kama ukiomba ‘fungu moja la machungwa, huwezi kupewa chungwa moja! ‘moja’ kwenye suala hili ni neno linalowakilisha vitu vingi vikiwa pamoja, vingi ni moja [fungu].” (Pratney 1988: 258-59) Hili ni la kweli, kwa sababu vipo viashiria vingi kwenye Agano la Kale vinavyoashiria Uungu, Yahweh, ni muundo wa wingi kwenye umoja, siyo ule muundo wa umoja dhaifu. Hivyo, Agano la Kale limesheheni Utatu kwenye huo Mungu alitumia maelezo yanayoashiria umoja kwenye wingi na wingi kwenye umoja. Agano Jipya limeliweka hili wazi na moja kwa moja kufunua kwamba umoja kwenye wingi na wingi kwenye umoja unapatikana ndani ya watu watatu wa Utatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

1. Neno la Kiebrania kwa “moja” lilitumika kumwelezea Mungu. Pratney anakumbusha: “*Yachead* ni neno la Agano la Kale lililotumika kwa kuelezea umoja uliokamilika; Hesabu au namba moja. Limetumika kama mara 12 kwenye Agano la Kale, lakini kamwe halikuelezea Umoja wa Mungu (Mwanzo. 22:2, 12; Zek. 12:10). *Echad* hata hivyo huzungumzia vitu au mkusanyiko wa vitu kwa umoja. Kwenye ndoa ‘wawili watakuwa mwili mmoja’ (Mwanzo. 2:24); Mkutano unaweza kukusanyika kuwa ‘kama mmoja’ (Ezek. 3:1); kuwa na moyo mmoja au ufahamu mmoja: ‘Waisraeli wote walikuwa na moyo mmoja kwenye kumfanya Daudi

kuwa mfalme wao' (1 Nyakati. 12:38). Hivi ni vitu vingi ambavyo wakati wote hutumiwa na Mungu wakati anapoitwa 'Bwana Mmoja.' (Pratney 1988: 259)

2. Neno la Kiebrania linalomwakilisha "Mungu." Neno la Agano la kale kwa Mungu ni *elohim*, ambalo ni neno la wingi (Feinberg 2001: 448). Limetumika takribani mara 2500 kwenye Agano la Kale (Pratney 1988: 259). Vipo vitu vitatu vya kufurahisha kwenye hili. Kwanza, umoja wa neno *elohim* ni *eloah* ambalo lilitumika mara chache sana kumwelezea Mungu. "Ni mpaka pale ambapo ilikusudiwa kuzungumzia wingi, kwanini hawakutumia neno la umoja ambalo ni *eloah*?" (Feinberg 2001: 449) Pili, wakati wingi wa *elohim* kiasili lilitumika kwa Mungu, ni kwa mara chache sana lilitumika na kihusishi cha umoja. Kwa kawaida, kijina na kisifa hukubaliana kwenye namba, hivyo hili kifasihi siyo la kawaida. Mara chache, hata hivyo, "wingi wa kisifa ulitumika na *elohim* kuzungumzia Mungu wa Israeli [Mwanzo 20:13; 35:7; 2 Sam 7:23]" (Ibid.). Tatu, wakati huo huo kwa kawaida matamshi ya umoja kama (e.g., "Mimi," "Yeye," "Wangu") hutumika kumtaja Mungu, mara chache wingi hutumika ambao huonekana kushauri wingi wa aina hiyo kwenye Uungu" (Ibid.). Kwa mfano, kwenye Mwanzo 1:26 ("Na tumfanye mtu kwa mfano wetu") "kisifa 'kufanya (na') aseh' ni wingi, na hivyo ni 'wetu'" (Ibid.: 450; angalia pia Mwanzo 3:22; 11:7; Isa 6:8).

3. Kwenye ufunuo timilifu wa Agano Jipya, Biblia imeweka wazi kwamba Mungu ni Utatu, akijumuisha, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Biblia imefanya hivyo kwa kuyatumia majina yale yale, vyeo, na sifa za Uungu kwa kila mmojawao. Kwenye jedwali lifuatalo, ^{x,y} inaashiria nukuu ya moja kwa moja.

Jina/Cheo/sifa	Mungu Baba	Mungu Mwana	Mungu Roho Mtakatifu
Mungu	Zab 45:6-7 ^x ; 1 Wakor 8:6	Waeb 1:8-9 ^x ; Yohana 1:1, 14, 18; 20:28	Matendo 5:3-4
Bwana Wa Milele Muumbaji	Isa 40:3 ^x ; 45:23-24 ^y Zab 90:2; Isa 43:10, 13 Mwanzo 1:1; Zab 102:25-27 ^x	Marko 1:2-4 ^x ; Wafil 2:10-11 ^y Mic 5:2 Yohana 1:10; Wakol 1:16; Waeb 1:10-12 ^x	2 Wakor 3:17-18 Waeb 9:14 Mwanzo 1:2; Ayb 33:4; Zab 104:30
Mjuvi wa vyote	Ayubu 21:22; Zab 33:13-15	Yohana 16:30; 21:17	Yohana 16:13; 1 Wakor 2:10-11
Mwenye nguvu Aliyeko wakati wote Mtenda miujiza na ishara	Isa 46:9-11; Nah 1:3-6 Mith 15:3; Jer 23:24 Kut 14:22; Dan 3:23-27	Waef 1:20-22; Heb 1:3 Math 18:20; 28:20; Waef 4:10 Marko 6:45-52; Yohana 20:30	Luka 1:35 Zab 139:7-10 Warumi 15:19; 1 Wakor 12:7-11
Aliyemfufua Yesu toka kwa wafu	Wagal 1:1; Eph 1:17, 20	Yohana 2:19	Warumi 8:11
Mwenye mapenzi Mkweli	Math 26:39; Waef 1:11 Yohana 7:28	Math 11:27; Luka 10:22 Yohana 14:6	1 Wakor 12:11 1 Yohana 5:6
Mtakatifu Mwema	1 Sam 2:2; Yohana 17:11 Zab 34:8	Matendo 3:14; Waeb 7:26 Yohana 10:11	Yohana 14:26 Zab 143:10
Mtoa Maisha ya kiroho	Waef 2:4-5	Yohana 1:4; 5:21	Yohana 3:8; Warumi 8:10
Hutia watu nguvu Hukaa ndani ya waamini	Zab 28:7-8; 46:1-2; 133:3 2 Wakor 6:16	Wafil 4:13 Waef 3:17; Wakol 1:27	Waef 3:16 Yohana 14:17; Warumi 8:9
Hufungamana na waamini	1 Yohana 1:3	1 Yohana 1:3	2 Wakor 13:14
Hutakasa waamini Huzungumza na watu	Yohana 17:17 Math 3:17; Luka 9:35	Waef 5:26; Waeb 10:10 Yohana 12:48-50; 16:1, 4, 19-25	1 Pet 1:2 Yohana 16:13; Matendo 8:29; 13:2
Huhuzunika	Mwanzo 6:6; Zab 78:40	Isa 53:3; Marko 3:5	Isa 63:10; Matendo 4:30

Kumbuka kwamba sifa kumi na moja za mwisho ni binafsi na za kipekee. Hizi zinaashiria kwamba Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni "watu," siyo "nguvu fulani" au sifa za nje au muungu tulivu.

4. Watu wote watatu kwenye Uungu hueleza na kuungana pamoja kwenye mistari tofauti.

- **Isa 61:1:** "*Roho ya Bwana Mungu i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta.*"⁶
- **Math 28:19:** "*Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.*"
- **Luka 3:21-22:** "*Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimepende zwa nawe*" (angalia pia Math 3:16-17;

⁶ Yesu alinukuu Isa 61:1-2 in Luka 4:18-21 kama maalumu zinazomtaja Yeye mwenyewe (i.e., Yeye ni "mimi" inaashiria kwake).

Marko 1:10-11).

- **Yohana 14:26:** “Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.”
- **Yohana 15:26:** “Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami.”
- **Warumi 8:8-9:** “Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaufuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.”
- **Waef 4:4-6:** “Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.”
- **Tito 3:4-6:** “Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu.”
- **Yuda 20-21:** “Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele.”

E. Ingawaje hautaeleweka kwa ufasaha, Utatu siyo fumbo ni uhakika na wa kuelezeka

Fundisho la Utatu halijajichanganya (i.e., kujipinga lenyewe ndani kwa ndani) wala la kutokueleweka Marehemu Papa Shenuda wa III wa Kanisa la Coptic alianza kuelezea jinsi ambavyo Mungu wa Utatu asivyohusisha mgawanyiko wa miungu kwa mfano huu: “Kama Kristo alivyosema kwenye Injili ya Yohana, ‘Mimi na Baba tu wamoja.’ (Yohana 10:30) Mwana alitoka kwa Baba bila kumwacha. Alitoka Kwake na bado alibaki Ndani Yake, kinachopelekea swali, kwa njia gani? Nitawaelezea kwa msaada wa mfano: Unapofikiri na mawazo yako yanatokea kama sauti, mawazo hayo hufikia masikio ya watu, bado mawazo hayo yanabaki kwenye ufahamu wako. Inawezekana pia mawazo kuuacha ufahamu wako na kuingia kwenye kitabu ambacho kitasambazwa Marekani mahali ambapo wengi watakisoma. Kwa busara hiyo mawazo yalitoka kwako na bado yalibaki kwako.” (Shenuda 2010: 4)

Mifano mbali mbali inaweza kuufanya Utatu kueleweka kwa wazi zaidi:⁷

1. Idadi ya abiria wa ndege na mtu. Abiria wa ndege Smith alifanya safari tatu kwa ndege ile ile kwa kipindi cha miezi mitatu tofauti: “Smith alihesabiwa kama abiria watatu tofauti, lakini kwa hakika, kwenye kila safari alikuwa ni mtu yuleyule. Hivyo wapo watatu kama tukiwahesabu abiria, lakini ni mmoja tu kama tukichambua kwa kuwahesabu watu. . . Kwa suala la wasafiri wa ndege, kila abiria kwenye kila safari ni mtu, lakini wakati mtu yuleyule anaposafiri safari tofauti tofauti, idadi ya watu haiongezeki lakini hesabu ya abiria inaongezeka. Vivyo hivyo, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (watu wote wa Uungu) ni Mungu, lakini haimaanishi kwamba ipo miungu mingi kama watu wa Uungu. Ni Mungu yuleyule anayejidhihirisha kwa watu watatu tofauti vile kama ilivyo kwa mtu yule yule mmoja ‘kudhihirika’ kwenye orodha tatu tofauti za safari za ndege.” (Feinberg 2001: 497-98, fafanuzi imeongezwa)

⁷ Hakuna mfano ulio mkamilifu. Huu ndio ukweli halisi tunapotaka kumwelezea Mungu asiye na Ukomo! Brower na Rea wanajadili mapungufu na matatizo ya mifano mikubwa iliyozeleka: “Miongoni mwa mifano iliyosikika sana kwa Utatu, miwili kwenye hiyo iliyozelewa zaidi; na mingine yake inafanania. Mifano hiyo miwili ni mfano wa ‘maji’ na mfano wa ‘yai’. Kulingana na wa kwanza, kama vile ambavyo maji yanaweza kuwa kwenye maumbo matatu (kimiminika, mvuke, na barafu), hivyo pia Mungu anachukua muundo wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kulingana na wa pili, kama vile ambavyo yai linavyoweza kuhusisha vitu vitatu (kaka, kiini, na ute mweupe), hivyo Mungu anaweza kuonekana kwenye watu watatu. Tatizo lililoko kwenye mifano yote miwili ni kwamba badala ya kuelezea mtazamo wa Imani, kiukweli inatuelekeza kwingineko. Kimiminika, mvuke na barafu ni udhihirisho wa kitu kimoja, ambacho ni Maji; hii ni kusema kwamba watu wa Mungu ni kama hao kuangukia tu kwenye muundo [mtazamo kwamba Mungu siyo watu Watatu lakini ni mtu yule yule akijidhihirisha kwenye muundo tofauti kwa nyakati tofauti]. Hata hivyo, katika “aina zake tatu” mfano wa “maji” unaweza kuletwa kwa karibu sana na maelewano au ulinganifu wa Utatu. Hili litazungumziwa kwenye maandiko. Kwa namna nyingine, kaka, kiini, na ute mweupe ni sehemu tatu za yai; lakini siyo kaka, kiini, wala ute mweupe ndivyo yai. Hivyo mfano huu haushauri kwamba ni Baba, Mwana, wala Roho Mtakatifu ni Mungu—ni sehemu ndogo tu ya Mungu.” (Brower na Rea 2005: 4) Bila kujali ukomo wa mifano hii, mifano kwenye maandiko haya kwa kiasi kikubwa hutusaidia kuona kwamba wazo la Kibiblia la Mungu Mmoja kuhusisha watu watatu halijichanganyi wala halikosi maana.

2. Sanamu ya mabo ambayo hutumiwa kama nguzo kwenye jengo. Mkandarasi wa majengo hutengeneza nguzo za sanamu za mabo ambazo hutumika kama nguzo kwenye ujenzi: “Sanamu na nguzo zote ni moja na vilivyotengenezwa na vifaa vilevile, siyo viwili. Na bado ni tofauti. Mmomonyoko wa ardhi wa juu juu utaziangusha sanamu lakini hauwezi kuzingusha nguzo. Uharibifu wa ndani ambao huhifadhi mwonekano wa nje lakini ukidhoofisha uwezo wa sanamu kushikilia uzito wa jengo utaangamiza nguzo lakini (kama sanamu ikiondolewa kwenye nafasi yake kama kibebeo cha uzito wa jengo) haitaiharibu sanamu. Hivyo, kile tunachotaka kukisema ni kwamba sanamu na nguzo vitu *vimetengenezwa kwa vifaa vile vile*, ingawaje *havifanani*. . . . Kufikia sasa uwazi wa haya yote kwenye Utatu utakuwa wazi: . . . Kila mtu wa Kiungu . . . ni tofauti na mwingine [hivyo kuwaweka kwenye makundi kumeepukika]. Lakini halikadhalika wao ni vifaa vile vile. . . . Kwa kuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanahesabika, kwa mtazamo huu kama tarakimu zinazofanana bila kujali utofauti wao . . . Tatizo la Utatu limetatuliwa” (Rea 2009: 712-15, fafanuzi imeongezwa)

3. Suluhisho la kimiminika. Suluhisho ni mbili au tofauti za msingi au mchanganyiko ambao umechanganywa pamoja lakini hakuna kemikali iliyohusishwa. Mifano itakuwa ni maji ya chumvi na chai ya limao. Kwenye maji ya chumvi, chumvi inayeyushwa kwenye maji. Vyote maji na chumvi iliyoyeyuka haviwezi kutenganishwa na kulijaza eneo lote na maji ya chumvi, bado vyote ni tofauti. Vivyo hivyo, chai ya limau ni mchanganyiko wa maji, chai, na juisi ya limau. Vyote vitatu hukijaza kikapu. Hata hivyo, haviwezi kutenganishwa, vyote viko tofauti. Vyote vitatu ni vya lazima; kukiondoa kimojawapo maana yake ni kwamba hakuna tena chai ya limau. Hivyo, kipo kikombe kimoja tu cha chai, lakini kimesheheni vitu vitatu tofauti, kila kimoja kimechangia kikombe kizima, na kila kimojawapo kina nafasi ya kipekee kuifanya chai ya limau ikamilike.

4. Ala tatu za Muziki au Sauti za vifaa vya Muziki. Mtaalamu wa vyombo vya Muziki Victor Zuckerkandl anaelezea muunganiko wa ala za muziki: “Aina tatu za sauti. . . . Hakuna kimojawapo kilichopo kwenye nafasi; au bora, vyote vipo kwenye eneo moja, hii ni kusema, kila mahali. Mahali tofauti, vitu tofauti vilivyowekwa kila kimoja kikiwa karibu na kingine, havina maswali. Lakini bado vina utaratibu, usiopingika wala kukosewa: vitu vitatu. Utaratibu wa mwendelezo wa mguso huhusisha nafasi, utaratibu ambao tunaousikia, siyo tu wa kufikirika: utaratibu wa ala tatu bila kuwa na mahali tofauti, bila vitu tofauti vilivyowekwa kila kimoja kikiwa karibu na kingine. . . . Ala ya kwanza, kama inavyosikika, inaenea maeneo yote. Kuungana na ya kwanza, ala ya pili, huongeza mengi itakiwavyo kuwa, haiwezi kuruhusu kuacha nafasi pembeni yake: nafasi zote zinazoonekana kuwa wazi zimeshamilikiwa na ile ya kwanza. Vivyo hivyo, haijafunikwa na ile ya kwanza: ile ya kwanza hubadilishwa kuwa kama ilivyokuwa, ikiwa wazi kwake. Sauti ya pili ni na imabaki kusikika *kupitia ile ya kwanza*. Vivyo hivyo ni kweli kama ilivyo ile sauti ya tatu: sauti iliyounganishwa kwenye ala ya sauti tatu, *kila moja kupitia kwa nyingine*. Au ngoja tuseme zinaingiliana moja na nyingine.” (Zuckerkandl 1956: 297, 299, fafanuzi imeongezwa; angalia pia Williams 2012: Mifano ya Utatu)

5. Asili ya nafasi: tofauti kati ya kitu chenye kipimo cha moja, mbili, na tatu. Kwa kila kitu chenye vipimo vitatu, kila kimoja cha vipimo hivyo vitatu—urefu, kimo, na upana—siyo tu kwamba ni “sehemu” ya kitu hicho lakini huhusika na umbo lote. Ingawa tunaweza kuzungumzia na kupima urefu, kimo na upana kama vile ni vitu tofauti vilivyotenganishwa, kama kimojawapo kikiondolewa kutoka kwenye umbo hilo huwezi kupata kaumbo kadogo, badala yake umbo zima linakuwa halipo tena.

Kuamua nafasi au kitu chochote chenye vipimo vitatu hatujumlishi kimo +urefu + upana; badala yake huwa tunazidisha (kimo x urefu x upana): “Mpaka unakuwa na umbo la vipimo vitatu, kuzidishwa kila kimoja na kingine, hakuna nafasi. . . . Kwenye $1 + 1 + 1$ kila kimoja ni sehemu ya umbo lote. Kila kimoja ni moja ya tatu ya umbo lote. *Lakini kwenye $1 \times 1 \times 1$ kila kimoja ni umbo lote!* Kwa hesabu hizi kila kimoja huzidishwa na kwa kila sehemu yote ya umbo husika lote.” (Wood 1978: 175-77, fafanuzi imeongezwa)

6. Asili ya ulimwengu. “Ulimwengu uliombwa kwa hakika ni wenye maeneo matatu ya Nafasi, Maada na Muda, kila kimojawapo huwakilisha Ulimwengu wote. Hata hivyo, ulimwengu haujaumbwa kwa visehemu vya nafasi, visehemu vya Maada, na visehemu vya muda . . . lakini ni Muunganiko wa vitu vitatu, ambavyo kila kimoja hujumuisha umbo lote, bado yote matatu yanahitajika kuunda umbo lote. Hivyo, Ulimwengu wote una nafasi, Wote una muda, na wote ni Maada (ukijumuisha nguvu kama umbo la Maada). . . . Zaidi ya hayo, Kumbuka usambamba baina ya Utatu Mtakatifu na Utatu wa Ulimwengu kwa kigezo cha ufahamu wa kawaida na vihusishi vyake vitatu. Nafasi haionekani, Historia ya uwepo wa wakati wote wa kila kitu kwenye Ulimwengu. Maada-na-Nguvu hufunua ukweli wa Ulimwengu. Muda huufanya Ulimwengu kueleweka kutokana na matukio yanayotokea humo. Kumbuka kwamba kwa uhakika sentensi hiyo hiyo inaweza kutumika kama maneno Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu vingekuwa badala ya maneno, Nafasi, Maada, na muda.” (Morris 2005: n.p.) Sundiata anaongeza, “Hakuna kimojawapo cha vitu hivi kinachounda kingine au kinachoweza kuishi bila uwepo wa hivyo vingine. . . . Hata hivyo muda siyo kama nafasi, ambao kwa namna

nyingine siyo sawa na Maada/Nguvu. . . . Hatuwezi kuvitenganisha vitu hivi vitatu au kuhesabu kimojawapo kuwa kidogo kuliko kingine au kuwa ndicho mkuu wa vingine na bado tukawa na Ulimwengu. Hata hivyo, kwa kurahisisha kwetu, tunahesabu muda, kwa mfano, kama unajitegemea tofauti na Nafasi na Maada/Nguvu. Hata hivyo tunahesabu Muda, Nafasi, na Maada/Nguvu kila kimoja kivyake. Hakika, Mungu wa Utatu ameacha ushahidi wa upekee wa uwepo wake kwenye muundo wa uumbaji Wake wa msingi—kama ishara kwamba Yeye siyo uwepo rahisi usio na shirika.” (Sundiata 2006: 194; angalia pia Wood 1978: 48-49)

7. Nuru. Ingawaje nuru inajitokeza kirahisi, isiyo na rangi, na sawa na sisi, kwa uhalisia inahusisha vitu vitatu tofauti: *mwanga usiokoma*, *mstari wa mwanga usiokoma*, na *mstari unaofyonza mwanga* inategemeana na chanzo cha mwanga (Evans 2013). Moja ya madhihirisho ya hili ni kwamba kitu kama kibao angavu husambaza nuru kwa mng’ao wa wazi au nuru “nyeupe” kwenye upinde wa mvua ambao upo kila mahali pamoja na mwanga.

Kwa nyongeza, “Nuru huweza kufanya kama vyote chembe chembe na mawinbi kwa wakati uo huo, na wanasayansi waliweza kuchunguza pande hizi mbili zikiwa kwenye matendo kwa kutumia kiona mbali cha umeme kiendacho kwa kasi zaidi. . . . Mawimbi ni matukio ya tofauti sana kwenye ulimwengu wetu, kama chembechembe. Na tunayo makundi ya hisabati kuelezea kila kimojawapo. . . . Chembe chembe ni, huwa na ubora kama nitakavyoweza kuiweka, kitu. Ni kidogo, kimoja, kitu chenye ukomo. . . . Kwa upande mwingine, mawimbi ni tofauti sana. Hayana ukomo.” (Sutter 2019: n.p.) Kwa maneno mengine, Utatu kama vioo ni kwamba Mungu anaweza kufanyaa kote kote kama “chembe chembe” (kitu chenye ukomo, i.e., Mwanadamu Yesu Kristo) na bado *kwa wakati uo huo* akafanya kama “wimbi” (i.e., Roho).⁸

8. Alama tatu za maji. “Alama tatu” ni “pale ambapo alama za ugumu, kimiminika, na gesi au hewa zinapounda kitu kilicho hai kwenye usawa. . . . Hili linamaanisha kwamba uwepo wa barafu, mvuke, na maji vinaweza kutokea tu katika moja ya hali maalumu ya joto na hali maalum ya msukumo.” (Bozack 1987: 39). Zaidi, “alama tatu zinaonyesha kitu kimoja kinaweza kuishi kwenye muundo wa misingi mitatu kwa wakati uo huo, kila kimoja kikiwa kamili kwenye asili yake bado kikiwa kimejitenga kwa kiwango cha kuwa na mwingiliano wa kimoja na kingine, hozi tofauti, na matumizi tofauti” (Bozack 1993: 67).

9. Tabia za Molikuli au Masi. “Tofali la kujengea kwa kila kitu cha kimwili ni atomi au atomi, likiwa na hisia chanya za kiini kilichopangiliwa kwa chembechembe ndogo sana, ikiwa na hisia hasi za elektroni. Atomi hushikamana moja na nyingine kwa kushirikishana elektroni zao, kuunda molikuli. Mpangilio tofauti wa elektroni kwenye molikuli Fulani zinaitwa ‘muundo wa tabia.’ Baadhi ya molikuli, kama maji, hazina tabia wakati nyingine zina muundo wa tabia tatu au zaidi, kama [madini].” (Qureshi 2016: 194) “Madini ya chuma yanaweza kuonekana *kama vile* yanasoma baina ya . . . mfumo mitatu tofauti. . . . Mfumo wa kubuni unaogeuka kutoka tabia moja kuwa nyingine unaitwa *tabia*. Ni muhimu kukazia kwamba madini ya chuma siyo kweli kwamba yanabadilika kutoka mfumo wa tabia moja kuwa nyingine. . . . Kwenye uhalisia, chuma hutenda kama vile ni mchanganyiko wa miundo ya tabia tatu.” (“Resonance” n.d.: n.p.) Kwa maneno mengine, tafakari za molikuli zipo kwenye miundo mingi wakati wote, kila muundo una mchanganyiko ule ule wa kemikali. Hivyo, madini yana muundo wa tabia tatu na hudumu kwenye miundo yote hiyo wakati wote. Kisha hili ndilo tukio lililomfanya Muislamu Nabel Qureshi kuona kwamba wazo la Utatu lilikuwa la kufaa. Aliandika, “Molikuli moja ya madini ni muundo wa tabia zote tatu wakati wote na kamwe siyo kimojawapo. Vitu vitatu vimetenganishwa lakini ni kitu kile kile, na vyote ni kimoja. Ni vitatu ndani ya kimoja. Hili ni wakati linapobofywa: ikiwa kuna vitu kwenye ulimwengu huu ambavyo vinaweza kuwa vitatu ndani ya moja, hata bila kueleweka hivyo, basi kwanini asiwe Mungu?” (Qureshi 2016: 195-96)

10. Muundo wa kweli wa utatu. Watu watatu wa Uungu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu), ingawa wanashiriki nafsi moja kila mmoja na mwingine, hudhihirisha utendaji tofauti, hasa hasa kwenye kuingiliana na Ulimwengu na watu, e.g., Baba alimtuma Mwana kuwa Mwokozi wa Ulimwengu (**1 Yohana 4:14**), Mwana akaja kuwa hai kwa mwanadamu Yesu Kristo (**Wafil 2:5-8**), na Roho mtakatifu akaja kukaa na kuwaongoza waamini (**Yohana 14:16-17, 26**).⁹ Kwa sababu Mungu ni Utatu, siyo ajabu kwamba kiuhalisia kila sehemu ya Ukweli kwa namna moja ama nyingine huashiria muundo wa Utatu—kwa njia nyingine tukiangalia utendaji wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Mfano unahusisha:

a. *Jua*. Jua limehusisha moto (plasma, halisi), nuru, na joto. Haya yote matatu yanahusisha jua lote, bado kila kimoja ni tofauti. Bila uwepo wa vyote hivyo jua halitakuwepo.

⁸ Bozack anaorodhesha alama saba za mfanano baina ya muunganiko safi wa Uungu wa Kristo na asili ya mwanadamu na asili mbili za mawimbi na chembe chembe (Bozack 1993: 72-76).

⁹ Hiki ni kitu kama mwanaume ambaye anaweza kuwa Baba, Mwana na mume kwa wakati uleule. Yupo mwanaume mmoja tu. Siyo kwa sehemu baba, kwa sehemu mwana, na kwa sehemu mume. Yeye ni baba kamili, yeye ni mwana kamili, na yeye ni mume kamili kwa wakati wote. Hata hivyo, wajibu wake hubadilika, hasa kwenye mwingiliano wake na dunia na watu, hutofautiana anaposimama kwenye jukumu la baba, mwana na la mume.

b. *Maada*

- Nguvu—Ya kawaida, chanzo kisichoonekana, chenye uwezekano.
- Msukumo—Hasa ambao umeambatana na nguvu hiyo.
- Matukio—Hasa msukumo unapogusana vitu vingine vilivyopo.

“Ni asili ya nguvu kuzalisha mwendo [msukumo]. Kama kwa msukumo, hauwezi kuwepo bila kusukumwa na nguvu nyuma yake. Wala hauwezi kuchukua nafasi bila kuwepo na tukio lisiloepukika linaloanzishwa nalo. Itakuwa vigumu kuwepo na msukumo bila kuwa na *aina* tofauti za msukumo, na hili linamaanisha Matukio. Na inakuwa kwamba tukio haliwezi kuwepo bila kuwepo na msukumo, na nyuma ya msukumo iwepo nguvu, kutoka kwa hayo tukio linatukia. . . . Kila kimojawapo miongoni mwa vitatu hutegemea kingine. Hakuna kati ya vitatu hivyo ambacho chaweza kuwepo bila kingine. Viwili pia haviwezi kufanya bila cha tatu.” (Wood 1978: 35)

c. *Muda*

- Ujao—Chanzo cha wakati wote, chenye nguvu kwenye matukio.
- Uliopo—Hasa uliunganishwa, kutambua mambo yajayo kuyajua na kuyashika
- Uliopita—husimulia na kuungana na uliopo wenyewe kwa nyakati zingine.

“Hakuna hata kimoja ambacho chaweza kuwepo bila hivyo viwili vingine. Hakuna viwili kati ya vitatu vinavyoweza kuwepo bila kile cha tatu. Kwa muda/nyakati haziwezi kuwepo bila ya hivyo vingine vyote vitatu. Kama hakuna mambo yaliyopita, nyakati hazijawahi kuwepo mpaka sasa, na baadaye kidogo hivi vilivyopo navyo vitakoma. Kama mambo ya wakati uliopo, hapatakuwepo na chochote cha sasa ambacho nyakati zilikuwepo. Kama hakuna yajayo, muda/nyakati zikikoma sasa, na kwakweli zingelikuwa zimekoma muda mrefu uliopita. . . . Ni utatu uliokamilika.” (Wood 1978: 41) Zaidi, “*Nyakati zote zilizopita au zitakazokuja*. Yajayo huhusisha zote hizo. *Nyakati zote zilizopo au zitakazokuwepo sasa*. Yaliyopo huhusisha hizo zote. *Nyakati zote zilizopo au zilizopita*. Nyakati zilizopita zilihusisha hizo zote. Pale mwanzoni nyakati zote ni zile zijazo. Baina yake, nyakati zote ni sasa. Hapo mwisho, nyakati zote zitakuwa zilizopita. Kila moja ni kamilifu. Zipo zote kama moja kana kwamba moja ni zote tatu. Ni Utatu mkamilifu.” (Ibid., fafanuzi imeongezwa)

d. *Mtu binafsi*

- Nafsi—Upekee wa mtu asiye na asili ya mwilii (ufahamu, hisia, Utu).
- Mwili—Upekee wa mtu mwenye asili ya mwili (umbo, jinsi/jinsia, DNA).
- Roho—Ambayo humwezesha mtu kuwasiliana na Mungu.

Kila sehemu hujihusisha na nyingine kwa karibu sana na kuwezeshana. Zote tatu ni za lazima ziwepo au “Ubinadamu” wa mtu utakoma kuwepo (kitu kisicho na uhai kinao mwili pekee; wanyama wanao mwili na nafsi pekee; ni mwanadamu pekee ambaye anavyo vyote Mwili, Nafsi, na Roho). Hata hivyo, humfanya mtu mmoja tu, siyo watu watatu.

Sehemu ya Utatu inaonekana kwenye muundo wa Ulimwengu na maisha ya mwanadamu kwa njia ambayo asili ya umoja dhaifu wa Allah haupo hivyo. Hili halikutokea kwa ajali. Biblia inasema, “*Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu*” (**Zab 19:1**, ESV). Asili ya ukweli imefanya hivi kwa kuashiria asili ya Mungu. Hakika, yapo mambo ya miujiza kwenye hili; lakini “Miujiza haikosi kuwa na maana, lakini uwepo wa maana nyingi ambazo hatuwezi kuzielezea/kuzifahamu” (Yancey 2000: 96). Tunapoanza kulishika wazo la Utatu, “kwa wakati huo, kwa mara ya kwanza kwenye maisha yetu, huanza kupata mawazo chanya, hata hivyo hudhoofisha, vitu ambavyo ni Zaidi ya mtu” (Lewis 1996: 143). “Vitu hivyo” ni Mungu wa kweli: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu: Mungu mmoja ndani ya watu watatu.

F. *Matokeo*

Kwamba Mungu wa Biblia ni Utatu kuna matokeo muhimu, ikiwa ni pamoja na yafuatavyo:

1. Kwa sababu ni Utatu, Mungu mwenyewe, tofauti na Allah, anajitosheleza mwenyewe. Kama Mungu angekuwa kirahisi mpweke kama mawazo ya Kiislamu kwa Allah na siyo Utatu, asingekuwa anayejitosheleza mwenyewe. Kama Mungu kirahisi angekuwa mpweke *angetakiwa* kuumba viumbe wengine ili awe na mahusiano. Hata hivyo, kwa sababu Mungu ni Utatu, hahitaji kuumba chochote (angalia **Matendo 17:24-26**). Kwa ulazima inamaanisha kwamba Allah ni *kiumbe kisichojitosheleza ambacho kinategemea uumbaji*. Kwa maneno mengine, ukweli kwamba Allah ni pekee “umoja mtupu” kwamba anakosa msingi muhimu wa wingi, hii ni kumaanisha kwamba “hawezi kufanya bila msaada wa kusaidiwa na wingi wa vilivyomo ulimwengu” (Frame 1995: 64; angalia pia Schaeffer 1982: 289 [Allah “anatakiwa kuumba ili aweze kupenda na kuwasiliana”]; vivyo hivyo, Allah “anahitaji ulimwengu kama ambavyo ulimwengu unamhitaji [yeye]”). Kwa hiyo, kwa umuhimu, Allah ni mdogo kuliko Yahweh; hivyo, Allah hawezi kuwa Mungu wa kweli juu ya ulimwengu.

Yapo matokeo muhimu kwenye hili. Kwa sababu Allah hawezi kuelezea wala kuzihisi sifa zote za (e.g., kupenda, furaha, mawasiliano) mpaka pale ambapo ulimwengu wa nje utakapokuwepo, ni *Uislamu unamiliki fundisho la Mungu*, siyo kwa ulazima wa Ukristo “wanaounganisha mwenzi” kwa Allah. “Mwenza” huyo ni ulimwengu wa nje wenyewe. Ni Mungu wa Biblia tu ambaye hana uhitaji wa “mwenza”—kiufupi kwa sababu Yeye ni Utatu.

2. Kwa sababu Yeye ni Utatu, Mungu pekee, tofauti na Allah, ni binafsi na mwenye mahusiano kwa msingi wa uwepo wake. Biblia (tofauti na Korani) inatueleza kwamba “*Mungu ni Upendo*” (1 Yohana 4:8). Hili linachipuka kutokana na ukweli kwamba Mungu ni Utatu na kwa umilele wote anao upendo mkamilifu na mahusiano miongoni mwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kwa sababu ni Utatu, Kwa asili Mungu ni Mungu pekee; kwa maneno mengine, yote ya Mungu ni “pekee” au sifa ya “mahusiano” humsukuma kutoka na ni msingi wa sehemu ya asili yake. Kwa namna nyingine, Allah siyo na, kwa sababu ya asili ya umoja wake mpweke, hawezi kuwa na mahusiano yoyote mpaka aumbe kiumbe kingine ambacho kwacho atakuwa na uhusiano nacho; hawezi kuhisi au kuelezea “upekee” wowote au sifa ya “uhusiano” isipokuwa mpaka atakapoumba ulimwengu. Vivyo hivyo, hakuna kimojawapo cha “pekee” au sifa ya “mahusiano” aliyo nayo, au atakayokuwa nayo, sehemu ya msingi wa kuwepo kwa Allah. Hili linamaanisha kwamba, ndani yake na kwake mwenyewe, Allah ni kiumbe kisicho na sifa ya kuwa mtu, Siyo miongoni mwa wenye uhai.

Hata hivyo, Utu hauwezi kutokana na kitu kisicho na utu. Mkandamizo au mkandamizo wa hewa au kitu kisicho na sifa ya utu hakiwezi kuumba, kuelezea, au kuwa na mahusiano na uwepo wa “Utu” au “pekee”. Kwa hiyo, Allah hawezi kujihusisha na utu wa mwanadamu, kwa kuwa wanadamu ni “pekee” [halisi]. Mafundisho ya Kiislamu kwamba Allah haeleweki ni kiashiria cha asili yake kitu kisicho na asili.

3. Kwa sababu Mungu ni Utatu, tunaweza kuwa na uhakika wa wokovu wetu. Mwanzoni tuliona kwamba Uislamu wote—ikiwa ni pamoja na Mohamedi mwenyewe—hawana uhakika na, na hawawezi kuwa na uhakika, kwamba wataweza kuokolewa. Pamoja na Ukristo, hali ni tofauti sana. Kulingana na Biblia, kwa sababu dhambi ya mwanadamu pamoja na kushtakiwa na dhamira mbele za Mungu, adhabu ya fidia kwa dhambi ni kifo cha milele. Hakuna mwanadamu ambaye anaweza kufidia hata dhambi yake mwenyewe kwa sababu ya tabia yake ya kutenda dhambi. Bali Mungu kupitia Kristo alichagua kufanya kile ambacho sisi wenyewe tusingeweza kufanya: kuyaishi maisha ambayo tulipaswa kuyaishi, kufa kifo ambacho tulipaswa kufa, na kulipia fidia ya dhambi zetu ambayo vinginevyo tulipaswa kulipia lakini hatukuweza. Kwenye hili, siyo tu kwamba fundisho la Utatu ni muhimu bali ni la lazima kabisa: “Kama Yesu ni mdogo kuliko Mungu (akiwa juu ya mwanadamu na hata Malaika, lakini bado hayuko sawa na Baba na Roho), ni kwa namna gani anaweza kuhudumu kama sadaka ya fidia kwa waote? . . . Kama Roho Mtakatifu, kama siyo Mungu kamili, matokeo ya wokovu tena ni makini. Maandiko yanafundisha kwamba Roho Mtakatifu huwahuisha waamini na kukaa ndani yao na kuwajaza, lakini kama Roho Mtakatifu ni mdogo au siyo Mungu kabisa, ni jinsi gani tunaweza kuwa na uhakika kwamba anaweza kufanya mambo haya? . . . Fundisho la Utatu huzuia uwezekano wa upotoshaji. Mmoja aliyefia msalabani ni Mungu kamili kama alivyokuwa mwanadamu kamili. Wokovu siyo tu wazo lake, wazo la anayestahili lazima laweza kumshawishi Baba; ni mpango wazi ya Uungu wote. Roho Mtakatifu anao uwezo wa kuhuisha, na kukaa kwake ndani ya waamini huuleta uwepo wa Mungu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu) ndani ya maisha yetu.” (Feinberg 2001: 440-41)

4. Utatu pekee yake hutupa jibu la wakati wote kwa uwepo na kwa ubinadamu. Ulimwengu ukihusisha vyote vyenye uhai na visivyo na uhai, visivyokuwa binafsi na tabia na hisia binafsi za mtu (i.e., vitu ambavyo vina ufahamu, utambuzi, kujijali). Kwa nyongeza, umoja (ikiwa na misingi ya usawa kwamba yaweza kupokelewa na kujifunzwa) na tofauti (hasa za kibinafsi) zinapatikana kwa viwango vyote ulimwenguni. Huo ni ukweli kwa viumbe vilivyo hai na visivyo na uhai na kutoka kwenye viwango vya atomiki hadi kwenye mfumo wa nyota kubwa kwenye ulimwengu. Kuueleza ukweli kama ulivyo, ukihusisha umoja na utofauti pamoja na utu, chanzo ni lazima kiwe angalau kikubwa kama ulimwengu na ni vipengele (Wood 1978: 22-23). Kama Francis Schaeffer alivyoliweka, ili kuwa na msingi wa kutosha kuelezea uhai, “tunahitaji vitu viwili. Tunahitaji binafsi –Mungu asiye na mwisho (au asiye na mwisho-Mungu binafsi), na tunahitaji umoja binafsi na utofauti katika Mungu” (Schaeffer 1982: 286).

Allah kama uhaba rahisi anaweza kuelezea umoja kwenye ulimwengu lakini haufai kwa utofauti. Zaidi, kwa sababu kwenye kiini chake Allah ni m-binafsi, Allah hana utu. Kwa maana nyingine, “Wakristo wa Judeo walitosheka na neno ambalo Mungu aliwapa kwenye Agano la Kale na Agano Jipya kwamba linatosheleza hitaji la kile kilichopo—Uwepo wa ulimwengu kwenye utata wake na mwanadamu kama mwanadamu. Na utoshelevu huo ninini? Inaeleza Mungu binafsi asiye na mwisho, ambaye ni muungano binafsi wa hali ya juu na utofauti kwenye utaratibu wa Utatu. . . . Bila utaratibu wa hali ya juu wa muungano binafsi na utofauti tupewao na Utatu, hakuna jawabu.” (Schaeffer 1982: 287-88, fafanuzi imeongezwa) Ni Mungu wa Utatu wa Biblia pekee ambaye ni sababu ya utoshelevu na fafanuzi ya uwepo kama ilivyo, akijumuisha umoja wake, utofauti, na utu.

V. Yahweh na Allah: Hitimisho

Wakati Yahweh na Allah ni “Mungu mmoja” ambaye hana “mwenzwa,” Umoja wa Allah ni umoja mpweke pale ambapo Umoja wa Yahweh ni umoja wa Utatu. Kimsingi Allah ni Mungu wa kipimo kimoja—mungu ambaye humchukulia Mohamedi kila msukumo, lakini ambaye Mohamedi anaweza kumwogopa na hawezi kumjua kibinafsi. Mungu wa Biblia, kwa maana nyingine, ni “vipimo vitatu” Mungu ambaye hawezi kushawishiwa/kutumiwa lakini ambaye anaweza kujulikana kibinafsi. Kwa ujumla, kinyume na **Q. 29:46**, Mungu wa Biblia na Allah wa Korani siyo Mungu mmoja na wala hata hawapo karibu kuwa Mungu mmoja.

5. BIBLIA NA KORANI

I. Utangulizi

Biblia ni kitabu kitakatifu cha Ukristo. Korani ni kitabu kitakatifu kwa Uislamu. Vyote vinaangaliwa kuwa ni neno la Mungu au Allah. Biblia haisemi chochote kuhusu Korani. Hata hivyo, Korani inavitaja vitabu mabali mbali, watu, na simulizi za Biblia. Karibu kila nabii aliyetajwa kwenye Korani ni takwimu toka kwenye Biblia (Emerick 2004: 89). Hivyo, Uislamu hawawezi kuidharau Biblia. Tatizo la Uislamu linainuka pale wanapojaribu kujihusisha na mikanganyiko mingi ya wazi baina ya Biblia na Korani.

II. Maendeleo ya Biblia

Ingawa inafikiriwa kwamba Biblia ndicho kitabu kikubwa zaidi, kwa hakika ni maktaba ndogo yenye “vitabu” 66: Vitabu 39 kwenye Agano la Kale (i.e., Biblia ya Kiebrania; maandiko matakatifu ya Wayahudi) na vitabu 27 kwenye Agano Jipya. “Neno la kiingereza ‘Bible’ limetokana na neno la Kigiriki *biblia* (likitamkwa kwa wingi), kifupi likimaanisha ‘vitabu.’ Kama ambavyo makusanyo ya maandiko ya Kiyahudi na Kikristo yalivyozidi kuongezeka na kuonekana kama kitu kimoja, neno hilo hilo ambalo kwa mashariki ya kati lilimaanisha wingi lilianza kueleweka kwa mapana kutumika kwa umaarufu wa ajabu kwa kufananishwa na mwanamke, halikuendelea kumaanisha ‘Vitabu’ lakini ‘Kitabu’” (Metzger 1993: 78-79). Vitabu vya Biblia viliandikwa kwa takribani na waandishi 40 kwa kipindi cha Zaidi ya miaka takriban 1500 (Agano la Kale likiwa limeanza kuandikwa takriban mwaka 1450 BC hadi mwaka 430 BC na Agano Jipya kutoka takriban AD 50-95). Wakati vingi vikiandikwa kuhusiana na jinsi ambavyo maandiko ya Agano la Kale na Agano jipya yalivyopatika na kutambuliwa kwamba yalitoka kwa Mungu na kukusanywa kwenye kitabu kimoja, kwa kusudi letu ukweli wa muhimu sana ni kwamba Biblia nzima ilitambuliwa, kukusanywa, kupatikana, na kutumika muda mrefu sana kabla Mohamedi hajazaliwa na miaka mingi kabla ya kuwepo kwa Korani.

Biblia ya Kiebrania (Agano la Kale) na baadhi ya maandiko yanayofanana nayo yalitafsiriwa kutoka kuwa ya Kiebrania na kuwa ya Kigiriki, tafsiri iliyojulikana kama Septuagint (LXX), iliyoanzia karne ya 3rd BC na kukamilika mwaka 132 BC (“Septuagint” 2019: History; angalia pia Bruce 1988: 43). Hata Uislamu wanakubali kwamba kanuni ya Agano la Kale ilianzishwa kabla ya Josephus kuandika mwishoni mwa karne ya kwanza AD (Dirks 2008: 41-42).

Ili kuweza kuongezwa kwenye Agano Jipya, vitabu vilitakiwa kufikia sifa mbalimbali: (1) *Mamlaka ya Kitume*: kiwe kimeandikwa na Mtume au, kama siyo, “kiwe kwa muundo wa kukubalika na Mitume” kingeunganishwa/kubalika (Bruce 1988: 258; angalia pia Carson na Moo 2005: 736; Sproul 1992: 23). (2) *Zamani za mababu*: “Kama maandiko yalikuwa kazi ya Mtume au ya mtu aliyekuwa karibu akifuatana na mtume, ni lazima iwe ya nyakati za mitume. Maandiko ya baadaye, bila kujali uthamani yake, visingeweza kuongezwa miongoni mwa kanuni au vitabu vya Utume.” (Bruce 1988: 259) (3) *Imani*: maandiko yalitakiwa kuwa yamethibitishwa na “Imani ambayo haikuwa na shaka ya maandiko ya mitume na kuhifadhiwa na kanisa ambalo lilianzishwa na Mitume” (Bruce 1988: 260; angalia pia Carson na Moo 2005: 736). (4) *Katoliki*: “Ni wazi kwamba viwango vya nyaraka zao ambazo zilisambaa duniani pote zina umuhimu mdogo na zimeendelea kukubalika na kutumiwa na Kanisa kila mahali” (Carson na Moo 2005: 737). Kwa maana nyingine. “Kazi ambayo ilipokelewa na kutambuliwa kwa uchache haikutambuliwa kama sehemu ya kanuni za Kanisa Katoliki [i.e., kanisa la kiulimwengu, siyo Kanisa la Katoliki la Rumi la sasa].” (Bruce 1988: 261; angalia pia Sproul 1992: 23).

“Ukweli kwamba kwa uwazi mkubwa Kanisa lote lilikuja kuvitambua vitabu vilevile ishirini na saba kama kanuni ya maandiko maarufu wakati ilipokumbukwa kwamba matokeo yake hayakujitokeza. . . . Wakati tofauti za kitamaduni zilipozingatiwa na kwa kuzingtia umhimu wa Imani ya Kikristo Makanisani, makubaliano yao ya kawaida kuhusiana na ni vitabu gani viwepo kwenye Agano Jipya vinasaidia kushauri kwamba maamuzi haya ya mwisho kimsingi hayakutokana na viwango vya Ubinadamu.” (Barker, Lane, na Michaels 1969: 29) Baadaye, kwa majibu ya kuinuka kwa mambo tofauti tofauti na mapingamizi, Kanuni za Agano Jipya

“zilithibitishwa na baraza la Hippo mwaka 393 CE, Sinodi ya Carthage mwaka 397 CE, na Baraza la Carthage mwaka 419 CE” (Dirks 2008: 43). “Kuthibitishwa” ni neno la kiutendaji kwa sababu, kama Sproul alivyosema, “Kanisa linatambuliwa, kukubali, kupokelewa, na kuwasilishwa kwenye kanuni za maandiko. Neno lililotumiwa na Kanisa kwenye baraza ni *recipimus*, ‘Tumepokea.’” (Sproul 1992: 23)

III. Mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia

Jerald Dirks anaeleza kiwango cha mtazamo wa Uislamu kwa Biblia kama ifuatavyo: “*Korani* imeonyesha vitabu hivyo vitano hivyo vya Ufu: vitabu alivyopewa Ibrahimu; kitabu (*Torati* au *Sheria*) alivyopewa Musa; kitabu (*Zaburi*) alivyopewa Daudi; kitabu (*Injili*) alivyopewa Yesu;¹⁰ na kitabu (*Korani*) alivyopewa Mohamedi. Uislamu wanaamini kwamba vitabu vyote hivi, kama ambavyo vilipokelewa kwa asili ya muundo wake kwa Wajumbe ambao baadaye waliviwakilisha kwa wanadamu, vilikuwa halisi, neno la Allah halisi. Hata hivyo, msembo wa kiutendaji ni ‘kama lilivyopokelewa kwenye muundo wake wa asili’. . . . Vitabu vya Ibrahimu uwepo wake havijulikani tena, na hakuna mwonekano uliobakia kwa ajili ya watu wa kizazi cha sasa. . . . Kama tunavyoheshimu vitabu vya Musa, ‘*Sheria* iliyopokelewa [*Torah*], kama inavyopatikana sasa kwenye vitabu vya Biblia vya *Mwanzo*, *Kutoka*, *Mambo ya Walawi*, *Hesabu*, na *Kumbukumbu la Torati*, ni mwiito wa mbali kutoka kwenye asili ya *Sheria*, ingawa mtazamo na vipengele vya asili ya *Sheria* vinaweza kuendelea kupatikana, zikiwa zimetawanyika hapa na pale kwenye ‘*Sheria* iliyopokelewa’. . . . Vivyo hivyo, Kitabu cha zaburi kwenye Biblia ya sasa ni mfanano dhaifu wa *Zaburi* za Asili za Daudi, ingawaje sura za matukio au mistari kwenye ‘zaburi zilizopokelewa’ zaweza kuwa sehemu ya *Zaburi* za asili. . . . Hatimaye, ni lazima ikumbukwe kwamba injili ya asili ya Yesu haiwezi kupatikana popote kwenye makundi ya *Biblia*, ingawa misemo tofauti iliyohusishwa na Yesu kwenye *Biblia* yaweza kuwakilisha vipande vilivyopotoshwa kutoka kwenye injili halisi.” (Dirks 2008: 189; angalia pia A’la Mawdudi n.d.: Q. 3:4n.2) Suhaym anadumisha kwamba “mengi ya yaliyomo kwenye kitabu hiki yalipotea na kuwa haitofu, na tafsiri na mabadiliko kuvingilia” (As-Suhaym 2006: 153-54).

Kwa jinsi gani, lini, kwanini, na kwa nani haya yalitokea? Uislamu hawawezi kusema. Kile chote anachoweza kufanya Emerick ni kufananisha mazingira na “kucheza mchezo ambao mtu mmoja ananong’oneza ujumbe kwa mwingine na mwishoni sisi kuona ni jinsi gani ujumbe utakavyomfikia mtu wa mwisho. Sasa ongeza hili kwa karne nyingi za kutangazwa na utaona ni jinsi gani hadithi na mila mpya zitakavyokuwa sehemu ya imani, ingawa bila kuwa na mamlaka yeyote kutoka kwa mjumbe wa asili.” (Emerick 2004: 88) Suhaym anaufananisha uharibifu huu na ujinga na mahali pa kupumzikia na kupaita kwa jina, “Kama kwa Wayahudi na Wakristo, vitabu vilivyofunuliwa kwa Manabii wao vilipotea kama matokeo ya ujinga wao wa kile kilichokuwa kwenye vitabu vyao; kwa wao kumchukulia mtu kama mungu badala ya Allah na muda mrefu uliopita baina yao na urafiki/uhusiano wao na vitabu hivyo. Hivyo makuhani wao waliandika vitabu ambavyo walidai vimetoka kwa Allah wakati ambao havikutoka kwa Allah lakini ikiwa ni dhana potofu tu na uongo na uvurugaji wa kilokole” (As-Suhaym 2006: 78)

IV. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia

Kimsingi Korani haitumii neno “Biblia” lakini huitamka kama “Kitabu” (angalia Q. 2:113; 6:20, 89, 114, 156; 10:94; 28:52; 37:117) na kuiita “maandiko” (Q. 2:113, 144-46; 3:19-20, 23, 65; 4:47, 51, 131, 136; 5:48, 57; 6:20, 114; 17:2; 23:49; 28:43, 52; 29:46-47; 32:23; 37:117; 40:53; 41:45; 46:12, Hilali-Khan). Inatambua kwamba Biblia “ilifunuliwa,” “iliteremshwa,” au “kutolewa” kutoka mbinguni kwa ajili ya Wayahudi na Wakristo (Q. 3:3, 19-20, 23, 65, 100, 187; 4:44, 47, 131, 136; 5:57; 6:20, 89, 91, 114, 156-57; 11:110; 13:36; 17:2; 23:49; 28:43, 52; 29:47; 32:23; 37:117; 40:53; 41:45, Hilali-Khan) Kwa kiasi kikubwa, kulingana na korani, Biblia “ilifunuliwa,” “iliteremshwa,” au “kutolewa” (“Kamusi ya Korani” 2009-2017: Q. 4:136, *nazzala*; Adelphi na Hahn 1993: pt.1.2). Korani inaongeza kwamba watu walioipokea Biblia walikuwa “wamevuviwa” au kupewa “ufunuo wa Mungu” kwa namna ile ile ambayo Mohamedi aliipokea Korani (“Kamusi ya Korani” 2009-2017: Q. 42:3, *yūhī*; Adelphi na Hahn 1993: pt.1.2).

Korani huwaita Wayahudi na Wakristo “watu wa kitabu” (Q. 3:23, 65, 69, 72, 75, 98, 99, 110, 113, 187,

¹⁰ Wazo la Kiislamu kwamba “injili” ni kitabu alichopewa Yesu halina msingi wa kihistoria wala wa kimaandiko. Kwanza, kama Robert Spencer alivyoonyesha, “Hakuna kiashiria kwamba hicho kitabu kiliwahi kuwepo: hakuna ushahidi wa kimaandishi popote kutoka kwa Uislamu wenye asili ya Kikristo ambao unaashiria Imani ya Kiislamu kuhusiana na Yesu au hata manabii wa Biblia. Kwa sababu Ukristo unaheshimu ‘injili’ kama ujumbe wa Yesu na siyo kitabu.” (Spencer 2009: 150) Hata mtetezi wa Uislamu Dr. Mohamedi bin Abdullah As-Suhaym anakiri “Hakuna mamlaka ya kihistoria inayojulikana kwa vitabu vya zamani” ambavyo Uislamu wanadai ni “vitabu” walivyopewa Musa, Daudi, na Yesu (As-Suhaym 2006: 183). Pili, Korani haielezi wazi wazi kwamba Injili ni kitabu alichopewa Yesu.

199; 4:47, 123, 131, 153, 159, 171; 5:5, 15, 19, 59, 65, 68, 77; 29:46). Kwa kweli, **Q. 6:156** (Hilali-Khan) kwa uwazi anasema, “*Hakika Kitabu kiliteremshwa juu ya makundi mawili kabla yetu (Wayahudi na Wakristo).*” Kwa kuwa “Kitabu” ni kimoja na kinahusisha kufafanua makala (“the”), hili linaweza tu kuwa kumbukumbu kwa Biblia yote. “Neno la Kiarabu lililotumika kwa Biblia ndiyo lile lile lililotumika kwenye Korani, *al-Kitab al-Muqaddas, Kitabu* kitakatifu. Hivyo, *Kitab* kinachojulikana kwenye Korani ni sawa na *Kitab* kilichotumiwa na Waarabu Wakristo wakati na baada ya wakati wa Mohamedi (Shamoun, “Quranic Witness,” n.d.: n.p.) Hakika, tafsiri ya Korani ya Sarwar **Q. 2:146** kimsingi inakitambulisha “Kitabu” kama “Biblia” (**Q. 2:146; 3:3, 78; 4:136; 5:41, 48; 6:114; 10:37; 57:16, 29**, Sarwar). Tafsiri ya Korani ya Mohamedi Asad inafanya vivyo hivyo (**Q. 3:78; 5:15, 19, 64-65, 68**, Asad).

Korani pia inafanya/kuonyesha kumbukumbu nyingi kuhusiana na “Torati”, **Q. 2:87; 3:3, 65; 5:44; 53:36; 87:19**, na “Injili”, **Q. 3:3, 45-48, 65; 5:46, 110; 57:27**. Neno “Torati” na “Injili” mwanzoni haikutumika ikiwa limegawanywa kwenye sehemu kama Agano la Kale na Agano Jipya lakini lilikuwa ni Agano la Kale na Agano jipya kama Biblia yote. Kulingana na Torati na Agano la Kale, Mwanazuoni Muislamu Dr. Mohamedi Laylah anaeleza, “Vitabu vitakatifu vya Wayahudi vimetajwa kwenye Korani kwa ujumla kama Torati; hii inajumuisha vitabu vitano vya Musa, vinavyoitwa Pentateuch au Sheria, ambavyo ni asili au jiwe la pembe la Biblia ya Kiebrania. Hata hivyo, Ibn Taymiyah anaeleza kwamba Wayahudi walitumia neno Torati kuizungumzia Biblia yote. Huu ni uwezekano muhimu. . . . Hata hivyo, Korani kwa uhakika haiwekei ukomo Torati ya Wayahudi na kimsingi haikatai uwezekano.” (Laylah 2005: 101-02)

Kwa wakati wa Mohamedi, neno “Injili” (Kiarabu = *Injil*) limekuja kuwa jina la Agano Jipya lote zaidi kama neno “Torati” lilivyotumika na Wayahudi kuliita Agano la Kale lote. Mwandishi Muislamu Mohamedi Abu Laylah anatambua kwamba neno *injili* bila shaka limetokea Syria au Ethiopia, “na inawezekana lilienea sana Uarabuni kabla ya wakati wa Mohamedi” (Laylah 2005: 102-03). Sundiata anaongeza, “Maneno Torati na Injili yalikuwepo kabla ya Uislamu na yalitumika bila ya mafafanuzi ya kwenye Korani. Kwa hiyo yaweza kufafanuliwa kulingana na hao ambao liliazimwa kwao. . . . Kwa hiyo kumbukumbu za Kikorani kwa maneno haya yanaweza kupatikana tu kwenye mazingira ya Wayahudi na Wakristo—badala ya kumbukumbu kutoka kwenye baadhi ya vitabu vya phantom ambavyo havipo tena. Korani haisemi kwamba yametoholewa kutoka kwenye maandiko ambayo yaliharibiwa kabla ya wakati wa Mohamedi.” (Sundiata 2006: 70). Walter Eric anahitimisha, “Kwenye Korani yote Torati imezungumzwa kama maandiko ya Kiyahudi na Injili kama maandiko ya Wakristo na maandiko hayo yote yanakubalika kwamba yalitoka kwa Mungu” (Eric 2011: 14).

Madai ya Waislamu kwamba Biblia ilipotea au kuharibiwa na Wakristo na Wayahudi ni sawa na madai ya Waislamu kwamba Yesu Kristo hakusulubiwa wala haufufuka—ni madai ambayo hayana ukweli wowote wa misingi wa Kihistoria lakini ilifanywa hivyo kwa sababu za Kitheolojia, kwa sababu maelezo, kweli, na theolojia ya Biblia huichanganya Korani. Hili linaonekana kwa njia nyingi:

A. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu Korani inathibitisha uwepo wake, uhalisia wake, na kuaminika kwake

Kiwango cha mtazamo wa Waislamu kwamba Neno la Allah “halisi”—Biblia—lilipotea au kuharibika ni *kinyume na Korani yenyewe*. Maelezo mengi kwenye Korani yamejikita kwenye msingi kwamba Biblia ni ufunuo wa kweli kutoka kwa Allah na “haikuharibika”

1. **Waislamu wameamriwa kuamini Biblia.** **Q. 3:3** inaeleza kwamba zote Agano la Kale (*Torati*) na Agano Jipya (*Injili*) haviwahusu tu Wayahudi na Wakristo lakini liliteremshwa “*kama mwongozo kwa Wanadamu*” (angalia pia **Q. 3:187; 6:92; 28:43**). **Q. 4:136** aliwaagiza Waislamu wote kuamini maandiko ambayo yaliitangulia Korani: “*Enyi mlioamini! mwaminini Allah na Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha juu ya Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha zamani; na mwenye kumkataa Allah na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake na Siku ya Mwisho, basi bila shaka amepotea upotevu wa mbali*” (angalia pia **Q. 2:136; 2:285; 4:136**). Amri hiyo ni ya wakati uliopo (i.e., wakati ambao Korani yenyewe ilifunuliwa kwa Mohamedi). Inaleta maana pale tu ambapo Biblia ilikuwepo na haikuwa imeharibika.

Q. 29:46 inawazungumzia Uislamu wale ambao wanapingana na Wakristo na Wayahudi: “*Wala msibishane na watu wa Kitabu ila kwa yale yaliyo bora, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja; nasi ni wajitupao Kwake*” (angalia pia **Q. 2:4; 3:3-4, 119; 5:59; 42:15**). Kumbuka kwamba migogoro ni kuwa raia mwema kwa sababu Wakristo na Wayahudi wana “Kitabu” ambacho kilifunuliwa na Allah. Pili, Uislamu wanapaswa “*kuamini katika huo ufunuo . . . ambao uliletwa kwenu.*” Maelezo hayo yote yasingetolewa kama Biblia haikuwepo tena au ikiwa ilikwisha kuharibika.

2. **Korani inatambua kwamba Biblia ilikuwepo na ilikuwa ikifundishwa.** **Q. 2:44** inasema, “*Je, mnawaamuru watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu hali mnasoma maandiko? Basi je, hamfahamu?*” (

angalia pia **Q. 7:169-70** **Q. 2:113** uthibitisho unasema kwamba Biblia ilikuwepo wakati wa Mohamedi na ilikuwa ikifundishwa na Wayahudi na Wakristo: “*Na Mayahudi husema: Wakristo hawakufungamana na cho chote; na Wakristo husema: Mayahudi hawakufungamana na cho chote; na hali wote wanasoma Kitabu.*”

Kuhusu Wayahudi, **Q. 5:43** (Hilali-Khan) anasema, “*Na watakuwekaje kuwa hakimiu nao wanayo Taurati yenye hukumu za Allah? Kisha baada ya hayo wanakengeuka; na hao si wenye kuamini.*” Mgogoro kama huo umefanywa kuhusiana na Wakristo kwenye **Q. 5:47** (Hilali-Khan): “*Na watu wa Injili wahukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah ndani yake; na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah basi hao ndiyo waasi.*” Adelphi na Hahn anaeleza kwa kifupi maana ya aya hizi: “Ndani ya hizi aya tunakumbushwa kwamba Wayahudi wanazo Torati halisi kwenye hifadhi yao (*‘indahum*); kwamba Wakristo pia wanayo injili yao halisi kwenye hifadhi yao. Tena hakuna ukweli wowote kwamba Wakristo waliibadilisha injili kwa njia ya kuitafsiri, kuiondoa au mabadiliko mengine ndani ya andiko lenyewe. Kama, kwa maana nyingine, tunadhani kwamba maandiko ya Torati na Injili yaliharibika, kuondolewa au hayapo tena duniani kwenye usafi wake, hili halipunguzi hukumu za kijinga za Korani kwamba Wayahudi wanajihukumu wenyewe kwa mujibu wa Torati kwamba ‘watu wa Injili wanahukumiwa kwa kile ambacho Allah alikifunua ndani yake’? Ni kwa namna gani watajihukumu wenyewe kwa kitu ambacho kimeondolewa au kwa maandiko yaliyoharibiwa? Na ni jinsi gani watatangaza kwamba ni “waishio kwenye uovu” (*fasiqun*), kama hawahukumu kwa kile ambacho hawana?” (Adelphi na Hahn 1993: pt.1.10)

3. **Korani inasema kwamba Biblia ni mwongozo toka kwa Allah na inapaswa kufuatwa. Q. 5:68** inasema, “*Sema: Enyi watu wa Kitabu, hamko juu ya cho chote mpaka msimamisha Taurati na Injili, na yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Bwana wenu*” “*Kusimamisha*” linamaanisha “kusishika [Torati na Injili] kwa uaminifu na kuzifanya kuwa sheria za maisha yenu” (A’La Mawdudi n.d.: Q. 5:68n.97). *Tafsir al-Jalalayn* inasema, “Enyi watu wa maaandiko, hamna msingi kwenye dini, ambao mtautegemea, mpaka pale mtakapozishika Torati na Injili na kile kilichofunuliwa kwenu na kutoka kwa Bwana wenu, kwa kutndea kazi kile kilichopo ndani yake (Jalal 2017: Q. 5:68, maoni , angalia pia Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 5:68, comment). Onyo la Ayah ii linaleta maana tu pale ambapo Torati na Injili zitakuwepo kwenye hali ya kutokuharibika kusomwa na kutendewa kazi. Kwa maana hiyo, sura 5 inahesabika kama moja ya ufunuo wa mwisho wa Korani (angalia **NYONGEZA A—MPANGILIO WA KIJIOLOGIA WA SURA**).

Q. 5:44 Inasema, Torati ni “*Kitabu cha Allah*” na kitawahukumu Wayahudi: “*Hakika Tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu, nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu bali Niogopeni (Mimi), wala msiuze Aya Zangu kwa bei ndogo: Na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndiyo makafiri.*” (Angalia pia **Q. 11:17; 17:2; 19:12; 21:48; 28:43; 32:23-24; 40:53-54; 66:12**) Ali anatolea maoni, “Wao [Waalimu] ni mashahidi hai kwa ukweli wa Maandiko, na watashuhudia kwamba waliwafundisha watu na wakazielewa” (Ali 2006: Q. 5:44n.752).

Vivyo hivyo, Korani inaikubali Injili. **Q. 5:46-47** inawaambia Wakristo kuyahukumu mambo kwa Injili pekee: “*Na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu katika nyayo zao, kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na Tukampa Injili iliyomo ndani yake mwongozo na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na mwongozo na mauidha kwa wamchao. Na watu wa Injili wahukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake; na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndiyo waasi.*” **Q. 3:187** inaenda mbali Zaidi na kueleza kwamba Biblia haikuwekewa ukomo kwa Wayahudi na Wakristo tu, lakini kuenezwa kwa kila mwanadamu: “*Na (kumbuka) Mwenyezi Mungu Alipofunga ahadi na wale waliopewa Kitabu: Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtakificha*” (angalia pia **Q. 3:3-4; 28:43**).

Michael na McAlister wanafupisha kwamba kutoka kwenye aya hiyo hapo juu “tunaona kwamba Korani inatambua kwamba Allah alitangaza Torati kuwa mwongozo na nuru kwa watu wake, na kwamba Allah alimtuma Yesu kuthibitisha Sheria ambazo zilikuja kabla yake. Korani pia inaitazama Injili kuwa mwongozo na Nuru, na yeyote atakayeshindwa kuamini Torati na Injili ataonekana kuwa ni muasi. Kwenye mtazamo wa kihistoria hii inamaanisha kwamba kulingana na Korani, Torati na Injili zikingali maandiko yenye mamlaka, yasiyoharibiwa na mwanadamu, takriban mwaka AD 624 wakati Korani ilipokuwa inafunuliwa kwa Mohamedi. Kwa hiyo, Uislamu wanaodai kwamba Biblia iliharibika kabla ya Korani haijafunuliwa wanapaswa kujitathmini kwa karibu ninini ambacho Korani inasema juu ya Biblia na siyo kujengea Imani yao kwenye mila ya mdomo na mawazo tofauti tofauti ya viongozi wao wa dini.” (Michael na McAlister 2010: 132)

Kwa nyongeza, Mohamedi mwenyewe aliambiwa afuate mwongozo wa Biblia. **Q. 6:84-88** inajadili manabii kwenye Biblia, kutoka Nuhu hadi Yesu. **Q. 6:89-90** basi inasema, “*Ni hawa ambao Tuliwapa Kitabu na uwezo wa kuhukumu na Unabii; kwa hiyo kama hawa (vizazi vyao) wakiwakataa hao, Tazama! Tumekwisha yaweka kwa watu wapya wasioyakataa. Hao ndiyo (manabii) ambao walipokea mwongozo wa Allah: Nakala ya*

mwongozo walioupokea.” “Kitabu” pekee ambacho yawezekana kinazungumziwa ni Biblia. Kile ambacho Allah alimwambia Mohamedi ni kwamba kama kizazi cha watu wa nyakati za Biblia watakataa kuifuata Biblia, basi Allah atawakabidhi watu ambao hawatakataa—hivyo Mohamedi angekuwa miongoni mwa wale wa mwisho watakaofuata mwongozo wa kizazi cha kwanza cha watu waaminifu. Hivyo, Mohamedi mwenyewe alikuwa ameagizwa kufuata mwongozo wa Biblia ambao ulipewa watu waaminifu ambao walimtangulia. Maelezo hayo na maagizo ambayo Mohamedi alipewa vinatupa maana ya kwamba kama Biblia ilikuwepo bado na ikiwa inapatikana na bila kuharibiwa, hivyo basi inapaswa kufuatwa kama mwongozo (jambo ambalo kwa kweli ndilo lililokuwa linatazamwa).

4. Korani inaiita Biblia Kitabu cha Allah na Neno lake ambalo haliwezi kubadilika. **Q. 5:44** inasema Torati ni “*Kitabu cha Allah*” (angalia pia **Q. 2:75; 3:23**). Kwenye maoni yake kwenye **Q. 3:23**, Mawdudi anadumisha, “Waliambiwa wakitambue Kitabu cha Mungu kama hukumu yao ya mwisho kwa mambo yote, na kuitii hukumu yake, kuikubali kama kweli kwa kile ambacho kitabu hiki kitasema kwamba ni sawa, na kosa kile ambacho kitabu kinasema kwamba ni kosa. *Kitabu cha Mungu kinachozungumziwa hapa ni Torati na Injili*, wakati maelezo ya ‘wale waliopewa sehemu ya Kitabu inawataja Wasomi wa dini wa Wayahudi na Wakristo.” (A’la Mawdudi n.d.: Q. 3:23n.22, fafanuzi imeongezwa) Hili linatambua mamlaka na kuaminika kwa Biblia.

Wachambuzi wengi huenda mbali Zaidi na kudumisha kwamba “Kitabu” hutaja *vitabu vyote vilivyofunuliwa na Allah* (ikiwa ni pamoja na Biblia), siyo Korani tu. (Ali 2006: Q. 3:23n.366; angalia pia Q. 10:94n.1475) Kwenye maoni yake **Q. 5:48**, Mawdudi anasema kwamba “Korani na vitabu vyote vilivyoteremshwa na Mungu kwa nyakati mbalimbali na lugha tofauti tofauti kwa ukweli vinaunda kimoja na kitabu kilekile” (A’la Mawdudi n.d.: Q. 5:48n.78; angalia pia Ali 2006: Q. 3:23n.366; Q. 10:94n.1475).

Hili ni la muhimu kwa sababu **Q. 18:27** inasema kwamba hakuna atakayeweza kubadilisha au kuliharibu neno la Mungu kwenye Kitabu chake “*Na usome yaliyofunuliwa kwako katika Kitabu cha Mola wako; hakuna awezaye kubadilisha Maneno Yake; nawe hutapata kimbilio kinyume Chake.*” **Q. 15:9** lina matokeo yale yale: “*Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha; na hakika Sisi ndio tuyalindao.*” **Q. 6:34** inasema, “*Na hakuna abadilishaye maneno ya Mwenyezi Mungu.*” (angalia pia **Q. 6:115; 10:64**) Kwa maneno mengine, Ahadi ya Allah kulilinda neno lake kutokana na uharibifu haiishii tu kwenye Korani lakini inahusisha Biblia pia. “Vivyo hivyo, kama Torati na Injili ziliharibiwa, basi Korani itakuwa inadanganya inaposema, ‘Neno la Allah haliwezi kubadilishwa’” (Sundiata 2006: 61).

5. Korani inadai kuithibitisha na kuilinda Biblia. Aya nyingi za Korani zinaeleza kwamba Mohamedi na Korani wanathibitisha ufunuo wa Biblia uliotangulia (angalia **Q. 2:41, 89, 97; 3:3; 4:47; 5:15, 48; 6:90, 92; 10:37; 12:111; 35:31; 41:43; 46:9, 12, 30**). Mawdudi anaeleza, “Mungu hakufunua Kitabu chochote ili kukikataa kilichotangulia; kila kimoja kinathibitisha na kukisaidia kinachoendelea” (A’la Mawdudi n.d.: Q. 5:46n.76). **Q. 5:48** anahitimisha kwa kusema, “*Na Tumekuteremshia maandiko kwa haki, kinachosadikidha yaliyokuwa kabla yake kwenye maandiko, na kukihifadhi, basi uwahukumu baina yao kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao kwa kuacha haki iliyokufikia.*” Kama Biblia ilibadilishwa au kuharibiwa, basi Korani itakuwa inadanganya au ilishindwa kwenye kazi yake ya kuthibitisha na kuwa mlezi wa Kitabu. Yupo Muislamu yeyote ambaye ameandaliwa kukiri moja ya majukumu hayo? Adelphi na Hahn wanaeleza kwa kifupi, “Msomaji anaweza tu kuhitimisha kutoka kwenye kifungu hiki kwamba Korani inaangalia ufunuo wa awali ulitolewa tu kwa ajili ya watu wa Kitabu kuwa kwenye umiliki wao na kwenye jaa lao. Hakuna kiashiria kwamba maandiko haya yalitwaliwa kwenda mbinguni, kwamba yaliondolewa au kwamba yaliharibiwa. Kinyume cha hayo, uwepo wa maandiko siyo tu kwamba unatambuliwa; umeelezewa kwa kina. Kwa hakika, Korani siyo tu inathibitisha maandiko haya; ni mlinzi, mtazamaji, mhifadhi wa maandiko ya awali (5:48), siyo mwondoaji wa maandiko ya awali.” (Adelphi na Hahn 1993: pt.1.6)

6. Mohamedi mwenyewe aliambiwa aiangalie Biblia. **Q. 10:94** inamwambia Mohamedi mwenyewe, “*Na kama unayo shaka juu ya hayo Tuliokuteremshia, basi waulize wale wasomao Kitabu kabla yako.*” **Q. 21:7** (Hilali-Khan) anaongeza, “*Na Hatukuwatuma kabla yako ila wanaume Tuliowafunulia. Basi waulizeni wale wanaoyajua vyema maandiko matakatifu wapo ninyi hamju!*” (angalia pia **Q. 3:93; 16:43**).

Maelezo yaliyotolewa hapo juu kwenye Korani, kwa Waislamu kudai kwamba Biblia ilikuwa imepotea au kuharibiwa inaongeza mashambulizi kwa Mungu (Allah) na kwa unyofu wa Korani yenyewe. Sundiata anahitimisha, “Kwa matokeo hayo wanasema kwamba Allah hajali, hafai, siyo mwaminifu, na hajali chochote kwa kile kilichotokea kwenye ufunuo wake au hana nguvu ya kutatua wala kuyalinda. Hili halikutokea kwao kwamba walimfanya Allah kuwa Mwongo, kwakuwa Yeye ndiye aliyesema kwenye Korani kwamba neno Lake Halitaharibiwa? Kama Allah alichukuwa muda wake kuwainua manabii na kuwa sababisha kuandika Ufu wake ili kuruhusu ufunuo wake huo kupuuzwa na kuharibiwa, basi Waislamu hawana sababu ya kumwabudu yeye.” (Sundiata 2006: 68)

B. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu Mohamedi anathibitisha uhalisia na kuaminika kwake

Mohamedi mwenyewe alitambua asili ya kutokuharibika kwa Biblia na kuufanyia kazi ukweli huo. **Q. 3:23** (Hilali-Khan) anasema, “*Je, hawaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu, wanaitwa kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili awahukumu baina yao, kisha taifa moja miongoni mwao hukengeuka, nao wamekwenda upande.*” Mchambuzi wa Kiislamu anaeleza kwamba aya hii iliteremshwa na Allah ikiunganishwa na tukio ambalo Wayahudi wawili walizini na kumwuliza Mohamedi ahukumu jambo hilo; Mohamedi akahukumu kwamba wapigwe kwa mawe wote mwaname na mwanamke (Jalal 2017: Q. 3:23, maoni; Ibn Abbas 2016: Q. 3:23, maoni; Ali 2006: Q. 3:23n.367). Ibn Ishaq mwandishi wa Mohamedi alisimulia tukio hili. Inasema kwamba, ili kuifikia hukumu, Mohamedi aliwauliza “watu wasomi sana walioishika Torati,” na “wakati mtume alipotoa hukumu iliyowahusu aliuliza kwenye Torati.” Mwalimu alisoma kutoka kwenye Torati lakini aliweka mkono wake juu ya aya inayozungumzia kupiga watu mawe (**Mambo ya Walawi 20:10**) mpaka alipoiona. (Ibn Ishaq 1955: 266-67) Baada ya hili, Mohamedi alisema, “Mimi ni wa kwanza kupokea amri ya Mungu na Kitabu chake na kuitendea kazi” (Ibid.: 267). Mohamedi asingefanya hivyo au kusema chochote kama hicho kama alikuwa anaamini kwamba Biblia ilikuwa “imeharibika.” Badala yake, kwa hakika alikiita “Kitabu cha Mungu wake.” Tukio hili pia limeandikwa kwenye Hadithi (al-Bukhari: 6841; angalia pia 6819). Maelezo ya Abi Dawud kuhusiana na hili yamebeba kweli za kina: “Kundi la Wayahudi walienda na kumwalika Mjumbe wa Allah huko Quff. Hivyo aliwatembelea shuleni kwao. Walisema: Abul Qasim, wenzetu wamejinajisi na wanamke; hivyo tangaza hukumu juu yao. Wakamwekea Mto Mjumbe wa Allah ambaye aliukalia na kusema: Leteni Torati. Ilietwa. Aliuvuta mto kutoka alikokuwa ameukalia na akaweka Torati juu yake na kusema: Ninaiamini hii na Yeye ambaye aliifunua.” (Abi Dawud: 4449, fafanuzi imeongezwa) Sam Shamoun anaeleza, “Mohamedi siyo tu kwamba anaamini unyofu wa maandiko ya Wayahudi, lakini aliiheshimu kiasi cha kuiweka kwenye mto!” (Shamoun, “Mashaidi wa Korani,” n.d.: n.p.) Waislamu wa kisasa ambao wanadai kwamba Biblia iliharibiwa au kubadilishwa na watu hao ndio waliomchanganya Mohamedi mwenyewe!

Mohamedi pia alithibitisha uhalali na kuaminiwa kwa Torati kwenye **Q. 28:48-49** (Hilali-Khan): “*Lakini ilipowafikia haki kutoka Kwetu, wakasema: Mbona hukupewa kama yale aliyopewa Musa? Je, hawakuyakataa yale aliyopewa Musa zamani? Walisema: Ni wachawi wawili wanaosaidiana; na wakasema: Hakika sisi wote tunawakataa Sema: Basi leteni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu ambacho kina mwongozo ulio bora kuliko hivi viwili - Taurati na Korani ili nikifuate kama ninyi ni wakweli..” Kwenye aya hizi, Torati na Korani ziko sawa kama “mwongozo.” Kwenye aya ya **49** Kimsingi Mohamedi anasema, “Hakuna mwongozo ulio bora kuliko Torati na Korani, na kama upo, ulete nami nitaufuata.” Angeseema hivyo tu kwamba Torati ilikuwa mwongozo kwake kama ilikuwepo na haikuwa imeharibiwa.*

C. Kwa sababu Yesu ni “mjumbe wa mapenzi ya nguvu” (Q. 46:35) na kuaminiwa kwenye unyofu wa Agano la Kale, Uislamu pia unapaswa kuamini unyofu wa Agano la Kale

Yesu ni mmoja wa wale watano tu, ambao ni “wajumbe wa mapenzi ya nguvu” (**Q. 46:35**). Zaidi, “Waslamu wanaamini kwamba nabii wa Mungu hawezi kudanganya, kwa kuwa manabii wote wa Mungu hawawezi kukosea” (Al-Kahtani 1996: 16). **Q. 4:150-52** pia inasema kwamba wajumbe wote wanaaminiwa na hakuna tofauti ya kuwekwa kati yao (angalia pia **Q. 2:136, 285; 3:84**). Kwa kuwa huu hasa ni ukweli wa Yesu, kama tulivyooona mwanzo, Yesu ndiye nabii pekee ambaye hakutenda dhambi kabisa na Yeye mwenyewe ndiye “Neno” la mungu (**Yohana 1:1, 14; Q. 3:39, 45; 4:171**). Steve Moyise anaonyesha, “Injili nne zinazopatikana kwenye Agano Jipya zinawakilisha takriban nukuu 60 tofauti za aya za maandiko [i.e., Agano la Kale] na alifanya angalau aligusia mara mbili ya idadi na Zaidi ya kumbukumbu za jumla” (Moyise 2010: 3-4). Nukuu hizi zote zinatoka kwenye Agano la Kale lote, zikijumuisha nukuu 26 kutoka kwenye sheria, 16 kutoka kwenye fasihi, na 15 kutoka kwa manabii (ikiwepo moja toka kwa Daniel ambaye alikuwa miongoni mwa manabii kwenye LXX lakini miongoni mwa maandiko ya Biblia ya Kiebrania) (Ibid.: 4). Hili ni muhimu kwa sababu Yesu aliamini kwamba Agano la Kale lilikuwa ni Neno la Mungu na kwamba neno lake halikuwa limeharibiwa. Aliliita Agano la Kale “Neno la Mungu” (**Marko 7:13**) na “amri za Mungu” (**15:3**). Alisema “Maandiko hayawezi kutanguka” (**Yohana 10:35**) na kwamba “Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya torati” (**Luka 16:17; angalia pia Math 5:18**). “Hitimisho ni rahisi. Kama mtu anamwamini Yesu Kristo [hata kama nabii], anapaswa kuwa imara na kuamini kwamba Agano la Kale na yale yaliyomo ni sahihi. Wengi wanataka kumkubali Yesu [kama nabii], lakini pia wanataka sehemu kubwa ya Agano la Kale. Uchaguzi huo haupo. Ama Yesu alijua kuhusiana na alichokuwa akikizungumza au Hakuelewa. Ushahidi uko wazi kwamba Yesu aliliona Agano la Kale kuwa ni Neno la Mungu; Mtazamo wake kulielekea ulikuwa siyo kingine Zaidi ya kuliamini kabisa.” (McDowell na Stewart 1986: 31)

D. Biblia haikuwa imepotea wala kuharibika kabla ya wakati wa Mohamedi kwa sababu nakala nyingi za kabla na baada ya Mohamedi zipo na hazijabadilika

Maandiko asili yaliyoandikwa na waandishi wa Agano la Kale na Agano Jipya hayapo tena, lakini maandiko mengi yanashuhudia uhakika wa Biblia kama tuliyo nayo sasa na hasa kwenye ukweli kwamba haikuwa imebadilishwa au kuharibiwa kabla au baada ya wakati wa Mohamedi. Maandiko ya Masoretic ni maandiko ya kimamlaka ya Biblia ya Kiebrania (Agano la Kale). “Maandiko ya Masoretic yalikuwa nakala za msingi, zilizohaririwa na kusambazwa na kundi la Wayahudi lililojulikana kama Masoretetes kati ya karne za 7th na 10th” (“Masoretic Text” 2019: n.d.) Vitabu vya Bahari mfu, viligundulika kwenye mapango kwenye jangwa la Qumran karibu na Bahari mfu, ambavyo vilikuwa vya karne ya tano hadi ya pili kabla ya Kristo. Miongoni mwake ilikuwa ni kitabu cha Nabii Isaya, ambacho kilikuwa ni “kikubwa zaidi (734 cm) na kilichokuwa kimehifadhiwa kwa ubora kuliko vitabu vyote vya Biblia, na kitabu pekee ambacho kilikuwa karibu kukamilika chote. Nguzo 54 zilizobeba sura zote 66 za toleo la Kiebrania za kibiblia za kitabu cha Isaya. Zenye tarehe kutoka. 125 BCE, pia ni mojawapo ya vitabu vya zamani vya Bahari mfu, yapata miaka elfu moja Zaidi ya maandiko ya Biblia ya Kiebrania tuliyojua kabla ya kugundulika Vitabu.” (“Maandiko makuu ya kitabu cha Isaya” 2019: n.p.)

Geisler na Nix wanakumbusha kwamba “kwa ugunduzi wa vitabu vya Bahari mfu, wasomi wa maandiko wamevipa miaka elfu moja mapema Zaidi ya yale makuu ya Masoretic, iliwawezesha kukagua uaminifu wa Maandiko ya Kiebrania. Matokeo ya kujifunza kwa kulinganisha yanafunua kwamba kuna utambulisho wa neno – kwa- neno kwa Zaidi ya asilimia 95 ya yale yaliyoandikwa, na tofauti ya asilimia 5 ikihusisha Zaidi makosa ya kalamu na maneno.” (Geisler na Nix 1986: 265) Josh McDowell na Don Stewart wanasema, “Vitabu vya Bahari mfu vinaonyesha kwa wazi ukweli kwamba Wayahudi walikuwa waaminifu kwenye kuweka kumbukumbu za Kibiblia” (McDowell na Stewart 1980: 26). Robert Wilson alifanya uchunguzi wa kina kuhusiana na maandiko ya Agano la Kale. Alihitimisha hivi, “Uchunguzi wa maandiko ya Kiebrania tuliyonayo kwa sasa yanaonyesha kwamba kwenye Agano la Kale lote zipo tofauti ndogo ndogo zinazoendelezwa na Zaidi ya maandiko kati ya 200 hadi 400, kwenye kila kitabu kilichopatikana, isipokuwa kwenye matumizi makamilifu na makosa na uandishi wa vokali. Ukamilifu, au makosa ya uandishi wa vokali havina madhara kwenye sauti au mguso wa neno.” (Wilson 1926: 69, 72, 82)

Kutokana na “ujumbe wa kunong’oneza” wa Emerick wa nadharia ya kuhamisha au mtazamo wa kuharibiwa kupitia “ujinga” na “ushabiki” ya Suhaym, Geisler na Nix wanaonyesha, “Kwa heshima ya maandiko ya Wayahudi, hata hivyo, siyo kwa usahihi wa uandishi tu ambao unatuhakikishia uzalishaji wao. Badala yake, ilikuwa ni mshangao unakaribia sawa na ushirikiano wa Biblia. Kulingana na Talmud, kulikuwa na sheria siyo tu kwa aina ya ngozi ya kutumiwa na ukubwa wa nguzo, lakini pia hata hivyo kulikuwa na ulazima wa Ibada ya kidini kwa Waandishi kufanyika kabla ya kuandika jina la Mungu. Sheria ziliongoza aina ya wino iliotumika, iliamuru nafasi kati ya neno na neno, na kukata kuandika chochote kutoka kwenye kumbukumbu. Kama maandiko yalikutwa na hata kosa moja tu, yalikuwa yakikataliwa na kuteketezwa.” (Geisler na Nix 1986: 263-64) Walihitimisha, “Maelfu ya maandiko ya Kiebrania, na uthibitisho wake wa baraza la wazee LXX [i.e., the Septuagint] na Wasamaria wa Vitabu vya Sheria (the Samaritan Pentateuch), na wengi wa wakaguzi wengine kutoka nje na ndani ya maandiko walitoa msaada mkubwa kwa kuegemea maandiko ya Agano la Kale” (Ibid.: 265).

Kulinganana Agano Jipya na Biblia kwa ujumla, “Uaminifu wa maandiko ya Agano Jipya . . . ikiegemea kwenye ushahidi mwingi wa maandiko. Ukihesabu nakala za Kigiriki pekee, maandiko ya Agano jipya yamehifadhiwa kwa kiasi cha nakala 5,366 kwa sehemu na sehemu ya maandiko iliyokamilika ambayo ilinakiliwa kwa mkono kutoka karne ya pili hadi ya tano. Kwa njia tofauti, vingi ya vitabu kutoka ulimwengu wa zamani vilipatikana nakala chache tu tena kwa kuchelewa.” (Geisler na Nix 1986: 267) “Hakuna maandiko mengine ya zamani ya kizazi hicho hicho ambayo yana ushahidi wa maandiko kama yalivyo ya Agano Jipya la Kigiriki” (Gilchrist 2002: 19). Sam Shamoun anaangalia: “Zinakaribia nakala 25,000 zilizokamilika au visizokamilika za kila kitabu cha Biblia kwenye maktaba yetu leo, ambavyo baadhi yake vilikuwa vya karne ya nne, sita, na hata ya nane kabla ya kukusanywa kwa Korani. Kulingana na kweli kwamba kila kitu kilinakiliwa kwa mkono, maelfu ya vigezo yaliinuka. Bado wakosoaji wa waandishi, ambao siyo lazima kuwa ni Wakristo, walivichunguza kwa makini vigezo hivyo na kuhitimisha kwamba tunayo asilimia 98.33% ya maandiko halisi, yenye asilimia 1.67% ambayo yamebaki bila kukosewa ndani ya vigezo husika. Hivyo, tunayo karibia asilimia 100% ya maandiko halisi ambayo yamehifadhiwa kwa uaminifu kupitia nakala za Maandiko. Zaidi, wakosoaji pia wameanzisha ukweli kwamba hakuna hata moja ya vigezo hivyo ambacho kimegusa fundisho lolote kuu, kwa kuwa mengi yake siyo chochote Zaidi ya makosa ya maendeleo, kutofautiana kwa namba, na kumbukumbu za waandishi ambazo zilidhaniwa kuwa sehemu ya maandiko ya waandishi waliofuata.” (Shamoun, “Mashahidi wa Korani,” n.d.: n.p.; angalia pia Habermas na Licona 2004: 85)

Kwa nyongeza ya uhakika wa maandiko ya Biblia, “Kazi za Wakristo wa kwanza kama Clement wa Rumi, Polycarp, Ignatius, na Papias yamebeba karibia kila aya ya Agano Jipya. Hili linatupa ushahidi wa uhakika kwamba Agano Jipya la sasa lilikuwepo wakati hao Wakristo wa kwanza walipokuwa wanaandika. Wakristo hao wa kwanza walizaliwa kabla ya mwaka AD 75, kabla ya kifo cha Mtume Yohana—mmoja wa wanafunzi wa Yesu ambaye aliandika sehemu ya Agano Jipya. Hivyo, Agano Jipya linaweza kufuatiliwa kirahisi hadi karne ya kwanza na kukubaliana na kile tulicho nacho leo. Ni Agano Jipya lile lile ambalo Wakristo wa Syria wa wakati wa Mohamedi waliloliita Injili na Korani ilibariki kama Halisi.” (Sundiata 2006: 74-75)

Siyo tu kwamba maelfu ya maandiko ya kibiblia yapo, lakini Biblia yote iliwekwa kwenye muundo wa kitabu muda mrefu kabla ya wakati wa Mohamedi. Andiko la Vatican, Andiko la Sinai, na Andiko la Alexandria, ya kutoka tarehe takriban mwaka AD 325-440, ikiwa ni pamoja na karibia Biblia yote (Agano la Kale na Agano Jipya) kwa Kigiriki.¹¹ Kanisa la Katholiki la Roma lilitafsiri Biblia yote kwa lugha ya Kilatini karne ya nne (Biblia toleo litwalo Vulgate) Maelfu ya maandiko ya kibiblia, barua za mababa wa Kanisa zikilinuwa Agano Jipya, na tafsiri kamili ya Kigiriki na Kilatini yanathibitisha kikamilifu kwamba Biblia haikupotea, kubadilishwa au kuharibiwa ama kabla au baada ya wakati wa Mohamedi.

E. Hakujawahi kutokea mtu aliyekusudia, aliyekuwa na msukumo, uwezo au nafasi ya kuiharibu Biblia hata kuthubutu kufanya hivyo

Mwanahistori Myahudi wa zamani aitwaye Josephus alizungumzia mtazamo ulioletwa na Wayahudi kuhusu kukinakili kitabu cha Biblia ya Kiebrania: “Ni kwa uimara kiasi gani ambao tumevitukuza vitabu hivyo vya taifa letu wenyewe, ni ushahidi kwa kile tukifanyacho; kwa kuwa kwa miaka mingi ambayo tayari imeshapita, hakuna mtu hata mmoja ambaye alishakuwa na ujasiri wa ama kuongeza chochote kwenye vitabu hivyo, kupunguza chochote, au kufanya mabadiliko yoyote; lakini limekuwa jambo la asili kwa Wayahudi wote, kwa haraka mara tu baada ya kuzaliwa, kuheshimu vitabu hivyo kubeba mafundisho ya Kiungu, na kuendelea kwenye hayo, na kama likitokea tukio kuwa tayari kufa kwa ajili yake” (Josephus c.97: 1.8). Wakristo hulitazama Agano la Kale na Agano Jipya kwa mtazamo sawa. Sundiata anaeleza, “Kwa kipindi cha miaka mia tatu ya Ukristo, wafuasi wa Kristo walidharauliwa kwa uchache kwenye dola ya Rumi ya zamani—hawakuwa na nguvu ya kuandika au kurudia kuandika historia. Wale waliokuwa na nguvu na walioupenda Ukristo walikuwa na orodha ya vitabu ambavyo waliviweka kama maandiko. Ni dhahira kufikiri kwamba kundi hili la masalia waliokuwa wamekusudia wangemruhusu mtu yeyote kuongeza au kuondoa kutoka kwenye maandiko ambayo yaliwasaidia kuendelea kwa karne nyingi.” (Sundiata 2006: 71-72)

Wayahudi na Wakristo kwa pamoja huichukulia Biblia ya Kiebrania (Agano la Kale) kawaida na kwa pamoja kuiheshimu kuwa ni Neno la Mungu. Wao hawakubaliani kabisa ikiwa Yesu Kristo aliyetabiriwa kwenye Biblia hiyo ndiye au siye Masihi. Walter Eric anaonyesha, “Uislamu lazima kwa makini wafikirie juu ya ukweli huu – Agano la Kale linachukuliwa kuwa ni Neno la Mungu na Dini mbili ambazo ni tofauti sana na kwa makini hulihifadhi kila mmoja huru na mwingine. Kwa sababu hiyo haupo uwezekano wa uharibifu wa maandiko kwa ama moja ya Imani hizi, kwa jaribio lolote la kubadilisha la mojawapo ya makundi haya kwa haraka sana uharibifu huo ungewekwa wazi na mwenzake.” (Eric 2011: 9-10)

Zaidi, “Kwa Nyakati za Mohamedi, Maandiko ya Wayahudi na Wakristo yalikuwa yanapatikana kwa wingi. Wayahudi na Wakristo hawakuwa kwenye eneo dogo la Kijiografia, mahali ambapo nakala za maandiko yao zingeweza kupatikana kwa pamoja, kubadilishwa na kuwekewa viwango. . . . Kwa hiyo, hata kama baadhi ya Wayahudi na Wakristo walibadilisha maandiko yao kwa mapungufu ya Mohamedi, mabadiliko yangukuwa kwa upana mdogo sana na nakala hizo zingeweza kutambuliwa kiurahisi. Maelfu ya nakala na sehemu ya Biblia zilizohuishwa kutoka maeneo mbali mbali hazikuzibadilisha nakala hizo.” (Sundiata 2006: 71)

Madai ya Waislamu kwamba Biblia ilibadilishwa na kuharibiwa kiwango cha kudai kwamba Wayahudi na Wakristo hawaaminiki na ni wadanganyifu wa watu. Sultan Mohamedi Khan anaonyesha, “Hii ni makini na mashtaka halali. Wakristo wanaamini Biblia kama Neno la Mungu kama ambavyo Waislamu wanaamini Korani. Hivyo, kama hakuna Muislamu anayeweza kuyabadilisha maandiko ya Korani, ni kwa jinsi gani ambavyo Wakristo wanaweza kubadilisha maandiko ya Kitabu cha Mungu mwenye hekima yote, yaani Biblia Takatifu? Kama baadhi ya Waislamu wabaya wanakuwa wapumbavu kiasi cha kama kubadilisha aya yeyote ya Korani, Waislamu wote je hawatamhesabu kuwa nje ya mwanga wa Uislamu na kueneza ukweli wote kuhusu mtu huyo? Kwa njia hiyo hiyo, kama baadhi ya Wakristo wabaya watabadilisha aya yoyote kwenye maandiko, Wakristo wengine wakweli je wote hawatamhesabu kuwa nje ya mwanga wa dini yao (Ukristo) na kueneza

¹¹ Vitabu hivi bado vipo. Maandiko ya Vatican yaliyopo kwenye maktaba ya Vatican; Maandiko ya Sinai na maandiko ya Alexandrinus yapo kwenye Maktaba ya British iliyopo London.

ukweli wote kuhusu mtu huyo? Bila shaka watafanya! Kutokana na hili utaona kwamba madai ya Uislamu kwamba Neno la Mungu lilibadilishwa hayana msingi wowote na ni yasiyofaa. Ninaamini kwamba madai haya hufanywa na Uislamu ambao kwa ujumla hawajui kabisa Biblia na Imani na mafundisho ya Wakristo.” (Khan 1992: 6)

John Gilchrist anasema kwamba mtu anapaswa kuwachangamoto Uislamu walete ushahidi wa kihistoria kuthibitisha madai yao kwamba Biblia ilibadilishwa: “Asili yake ilikuwa nini? Kwa usahihi upi, uliobadilishwa kukifanya kitabu tulicho nacho leo? Ni nani aliyeyafanya mabadiliko hayo? Yalifanywa lini? Mara unapomchangamoto Muislamu yeyote kuwatambulisha watu halisi ambao wanadaiwa kuiharibu Biblia, kwa wakati gani kwenye historia tukio hilo lilifanyika na mahali gani, na kwa uhalisia ni maandiko gani yalifanyiwa mabadiliko kwenye maandiko ya asili, utaona kwamba hawataweza kabisa kujitetea wala kuthibitisha madai yao. Kwa ufupi tu ushahidi huo haujawahi kuwepo.” (Gilchrist 2002: 20)

F. Hitimisho

Madai ya Uislamu kwamba Biblia iliharibiwa au kupotea na Wayahudi na Wakristo ambao ndio walioipokea hayana uhalali wowote wa kihistoria au msingi wa kweli. Kwamba madai haya yalifanywa tu na kwa sababu za kitheolojia kwa sababu maelezo, kweli, na theolojia ya Biblia inashindana na Korani. Baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu wanalitambua hili. Mahmoud Ayoub anakiri, “Kinyume na mtazamo wa jumla wa Kiislamu, Korani haiwahukumu Wayahudi na Wakristo kwa kulibadilisha maneno ya maandiko yao, lakini badala yake kubadilisha ukweli ambao uko ndani ya maandiko hayo. Watu hufanya hayo kwa kufunika baadhi ya maandiko matakatifu, kwa kutokuzitendea kazi kanuni zake, au kwa ‘kulibadilisha neno kutoka kwenye nafasi yake halisi [imenukuliwa Q. 4:26; 5:13, 41; angalia pia Q. 2:75].’ Hata hivyo, hili linazungumzia Zaidi tafsiri kuliko ukweli wa kuongezwa au kufutwa kwa neno kutoka kwenye vitabu vitakatifu.” (Ayoub 1986: 5)

V. Je Mohamedi alitabiriwa kwenye Biblia?

Q. 61:6 Yesu alisema “*Na aliposema Isa bin Mariamu! Enyi wana wa Israeli, mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad.*” **Q. 7:157** inamtaja “*Nabii asiyejua kusoma wala kuandika, ambaye wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili.*” Hilali-Khan halisi inatambulisha nabii mbili za msingi ambazo Waislamu hushindana kwamba zinatabiri ujio wa Mohamedi kwa kutafsiri **Q. 7:157** kama: “*Nabii ambaye ama hawezi kusoma wala kuandika (i.e. Mohamedi SAW) ambaye walimkuta ameandikwa kwao kwenye Torati (Torah) (Kumbukumbu, xviii, 15) na injili (Gospel) (Yohana xiv, 16).*”

A. Je Mohamedi ni “nabii” anayetajwa na Musa kwenye Kumb 18:15-19?

Kwenye **Kumb 18:15-19** Musa alisema, “*15Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye. Kama vile ulivyotaka kwa Bwana, Mungu wako, huko Horebu, siku ya kusanyiko, ukisema, Nisisikie tena sauti ya Bwana, Mungu wangu, wala nisiuone tena moto huu mkubwa, nisije nikafa. Bwana akaniambia, Wametenda vema kusema walivyosema. Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.*”

Sababu za msingi kwanini Waislamu wanadai kwamba hili linamtaja Mohamedi ni lugha iliyotumika “kutoka kwa/ndugu” zao mstari wa. **15, 18**. Laylah anahitimisha hivi kutokana na hili, “Miongoni mwa ndugu zao’ ni muhimu –hili linamaanisha kutoka kwa ndugu za Wayahudi, lakini siyo kutoka kwa Wayahudi wenyewe” (Laylah 2005: 42; angalia pia Abdul-Mohsin 2006: 93, 210-11). La pili, Waislamu wameleta tofauti mbalimbali baina ya Yesu na Musa sawasawa na baina ya Mohamedi na Musa, kuhitimisha kwamba Yesu siyo “nabii kama mimi” (i.e., siyo kama Musa) lakini kwamba Mohamedi ni sawa na Musa. Kwa mfano: “Musa alikuwa na Baba na Mama, kama Mohamedi, lakini Yesu alizaliwa kwa Miujiza. Musa na Mohamedi waliona na kuzaa watoto, lakini Yesu alibaki kutokuwa na mke maisha yake yote. Mohamedi na Musa walitambuliwa kama manabii na watu wao wenyewe wakati wa maisha yao. Kama kwa Yesu, ‘Alikuwa kwa waliokuwa wake na wale waliokuwa wake hawakumpokea’ (Yohana 1:11). Musa na Mohamedi walikuwa manabii na watawala, na waliyafanyia kazi mamlaka yao maishani mwao. Yesu alisema kwamba Ufalme wake siyo wa Ulimwengu huu, na alikataa kutoa hukumu. Musa na Mohamedi walileta sheria mpya kwa watu wao. Yesu alisema sikuja kuitambua torati bali kuitimiza. Wote wawili Musa na Mohamedi walikufa vifo vya asili, wakati Yesu alisulubiwa msalabani, kulingana na Imani ya Wakristo, na kupaa mbinguni kulingana na Korani na utamaduni Waislamu, bila kusulubiwa. Mungu hakumwinua nabii miongoni mwa ndugu wa wana wa Israeli isipokuwa Mohamedi.” (Laylah 2005: 43-44; angalia pia Abdul-Mohsin 2006: 93-94, 211-12) Matumizi haya ya

Waislamu kwa Biblia ni makosa kwa karibu kila kitu.

1. Biblia kwa wazi inasema kwamba Yesu Kristo ndiye Nabii aliyetabiriwa kwenye **Kumb 18:15-19**.

Kwa kuwa hata **Q. 2:113** inasema kwamba Wayahudi na Wakristo “*hujifunza kitabu kile kile,*” kwa uwazi utafsiri mzuri wa maandiko ni maandiko yenyewe, i.e., kitabu kile kile. Agano Jipya, siyo mara moja lakini mara nne, imemtambulisha Kristo kama nabii aliyetabiriwa. Kwenye **Yohana 1:45**, baada ya kukutana na Yesu, Philipo alipomkuta Nathanaeli na kumwambia, “*Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti.*” Kwenye **Yohana 6:14**, baada ya Yesu kutenda ishara na miujiza, watu walioshuhudia miujiza walisema, “*Hakika huyu ndiye Nabii yule ajaye Ulimwenguni.*” “Nabii” pekee ambaye anaweza kutajwa ni nabii aliyetabiriwa kwenye **Kumb 18:15-19. Matendo 3:22** na **Matendo 7:37** Wote wananukuu unabii ambao ulitimizwa na Yesu. Hotuba ya Petro kwenye **Matendo 3:11-26** ni kuhusiana na Mungu kumwinua Yesu ambaye Wayahudi walimwua (kama ambavyo ilitabiriwa) na jinsi Yesu alivyoutimiza unabii wa Agano la Kale; vivyo hivyo, watu wanatakiwa kutubu au wataangamizwa wakati Kristo atakapokuja tena. Kwenye **Matendo 7**, Stephano aliangalia historia ya Wana wa Israeli kwa viongozi wa Wayahudi. Baada ya kuunukuu unabii wa Kumbukumbu la Torati alihitimisha, “*Enyi wenye shingo gumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo.*”

Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule Mwenye Haki, ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti wake, mkamwua.” (**Matendo 7:51-52**) “Mwenye haki,” bila shaka, siyo mwingine zaidi Yesu ambaye alisulubiwa na kuuawa kwa uchochezi wa viongozi wa Wayahudi.

2. “Ndugu” waliotajwa ni Wayahudi wenzao na siyo Waarabu. **Kumb 18:15-19** wote ni unabii mmoja.

Kumb 18:15 linaweka wazi kwamba “ndugu” wanaotajwa siyo Waarabu, kama alivyo Mohamedi, lakini ni Wayahudi wenzao, kwa kuwa Biblia inasema kwamba Mungu atawainulia nabii “*kutoka miongoni mweni.*” Uislamu hufikiria juu ya neno “ndugu”. Kile kinachoonekana walishindwa kukitambua ni kwamba “Agano la Kale lote, maelezo ‘ndugu zao’ limetokea mara nyingi na kila lilipotokea lilimaanisha kwa moja ya makabila ya Israeli kama tofauti na mtu mmoja halisi kutajwa” (Gilchrist 2002: 123-24). Mazingira yote ya **Kumbukumbu la Torati 18** ni Musa alikuwa akitoa maelekezo kwa Kabila la Walawi kwa sababu lilikuwa Kabila la Kikuhani na kile watakacho kifanya Waisraeli baada ya kuingia nchi ambayo Mungu aliwaahidia (angalia, e.g., **Kumb 17:2, 14-15, 18, 20; 18:6, 9, 14; 19:1-3, 7-10, 12, 14**). Kwenye **Kumb 18:15-19**, Musa alikuwa akisema kwamba Mungu atawainulia nabii siyo kutoka miongoni mwa Walawi lakini kutoka kwenye moja ya makabila mengine ya Israeli. Unabii huu unatumika kwa Yesu kwakuwa alitoka kwenye kabila la Yuda. Kwa kweli, kulingana na mazingira ya **Kumbukumbu la Torati 18, Waeb 7:11-16** inatofautisha Ukuhani wa Walawi na Ukuhani mkuu wa Yesu.

Wakati Wayahudi na Waarabu wote wakifuatilia wazee wao hadi kwa Ibrahimu (Waarabu kupitia Ishmael na Wayahudi kupitia Isaka), kamwe Biblia haiwataji Wayahudi na Waarabu kama “ndugu.” Kwenye historia ya Kibiblia ya kuuzwa Yusufu utumwani, “wana wa Yakobo, ambao kupitia wao kabila kumi na mbili za Israeli zimeitwa, Wamejitaja wenyewe kama ‘ndugu’ na kwa Waarabu ambao walimnunua Yusufu kama ‘Muishmaeli’” (Sundiata 2006: 262). Kwa kweli, Isaka na Ishmael wenyewe kamwe hawajawahi kiukweli kuitwa “ndugu” kwenye Biblia ingawa walikuwa watoto wa baba mmoja. Hili lilithibitishwa kwenye **Kumb 17:14-15** ambayo inasema, “*Utakapokwisha kuingia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako ukaimiliki, na kukaa humo; nawe utakaposema, Nitaweka mfalme juu yangu mfano wa mataifa yote yaliyo kando-kando yangu; usiache kumweka yule atakayechaguliwa na Bwana, Mungu wako, awe mfalme juu yako; umweke mmoja katika ndugu zako awe mfalme juu yako; usimtawaze mgeni juu yako, ambaye si ndugu yako.*” Kwenye mazingira ya **Kumbukumbu la Torati 17** na **18**, neno “ndugu” linatumika kwa Waisraeli wenzao, siyo Waarabu au “wageni.” Wengine, kwa nyongeza, Mohamedi isingewezekana kuwa ndiye nabii aliyetabiriwa kwa sababu hata hakuwa amezaliwa hadi baada ya miaka 500 *baada ya Israel kukoma kuwepo* kama Nchi ya Wayahudi.

3. “Nabii kama Mimi”: Yesu pekee ndiye kama Musa kwenye hisia muhimu. Ulinganifu na utofauti

ambao Uislamu huweka baina ya Musa, Mohamedi, na Yesu kwa hakika ni upumbavu na kuonyesha jambo la uwakilishi/mbadala kuwa jambo dogo. Kwa mfano, Deborah, Samuel, Daudi, and Solomon wote walikuwa manabii, watawala (pengine waamuzi au wafalme), walioa, walizaliwa kwa njia ya kawaida, walikufa vifo vya asili, walitambuliwa kama manabii kwa kipindi cha maisha yao, na walieneza neno la Mungu kwa watu. Mungu alizungumza nao kwa njia ya moja kwa moja (angalia **Waamuzi 4:6-7; 1 Sam 3:10-14; 23:2, 4; 1 Wafal 3:5, 11-14**) kama alivyofanya na Musa (e.g., **Kut 33:12-23**) lakini tofauti na Mohamedi (ambaye alipokea ujumbe wa Allah tu kupitia kwa Gabriel). Hivyo, madai yao ni Zaidi ya yale ya Mohamedi, hasa kwakuwa wote wametoka kwenye uzao wa Agano wa Isaka.

La muhimu zaidi, Uislamu hupuuza kutaja kwamba Yesu alijiita mwenyewe “nabii” (**Luka 13:33**) na alitambuliwa na wengine kuwa nabii (**Math 21:11; Luka 7:16; 24:19; Yohana 4:19; 6:14; 7:40; 9:17**). Yeye pia alikuwa Mfalme (**Math 21:1-11; Marko 11:1-11; Luka 19:28-40; Yhn 1:49; 12:12-16:1; 12:13; Ufu 17:14; 19:16**). Yesu aliyatumia mamlaka ya Ufalme wake na kuutangaza ufalme wake wakati akiwa ulimwenguni (**Math 12:28; Luka 10:9; 11:20**); ameketi kwenye kiti cha Enzi na anatawala sasa (**Matendo 2:29-36; Waef 1:21**). Yesu pia alioa: yeye ni Bwana harusi (**Marko 2:19**) na watu wake, kanisa, ndio Bibiarusi na mke (**Ufu 19:7; 21:2, 9-10**). Kama tulivyoona kwenye kipengele cha pili hapo juu **2.VIII.J. Yesu alifundisha kwa mamlaka ya Kiungu na siyo Mohamedi**, Mohamedi alisema kwamba hajaleta jambo jipya lolote (**Q. 46:9**), lakini Yesu alileta “sheria ya Kristo” (**Luka 22:20; 1 Wakor 11:25; 2 Wakor 3:6; Waeb 8:8-13; 9:15**) na alikuwa na uwezo wa kuzibadilisha sheria za Mungu kwa mamlaka yake mwenyewe (**Q. 3:50; Math 5:21-22, 27-28, 31-34, 38-44; Marko 7:18-19**). Alikuwa na uwezo wa kufanya haya kwa sababu, tofauti na Mohamedi ambaye alidai kupokea Korani kutoka kwa Malaika, kila kitu Yesu alichokisema na kutenda kilikuwa kile tu ambacho baba alimtaka afanye (**Yohana 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**) kwa sababu yeye ni “neni la Mungu” (**Q. 3:39, 45; 4:171; Yohana 1:1, 14; Ufu 19:13**).

Yesu pekee anaweza kuwa nabii aliyetabiriwa kwenye **Kumb 18:15-19** kwa sababu siyo tu kwamba maisha yake yanaendana na yale ya Musa, lakini ni Zaidi sana ya Musa. **Waebrania** inaelezea jinsi ambavyo Kristo ni kama Musa, lakini mkuu kuliko Musa (**Waeb 3:1-6**): Kristo ni “*Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba*” (**Waeb 3:3**); na pale ambapo “*Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi . . . bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu;*” (**Waeb 3:5-6**). Tunayaona haya sambamba kutoka kuzaliwa hadi kifo:

- *Musa alikuwa mtangulizi wa Masihi*: Musa alikuwa wa kipekee miongoni mwa manabii, kwenye kazi kuu alizozifanya na ukweli kwamba Mungu hakuzungumza naye kwa maono na ndoto lakini “*mdomo kwa mdomo*” na “*uso kwa uso*” (**Hes 12:6-8; Kumb 34:10-12; Q. 4:164**) kama mtu azungumzavyo na rafiki yake (**Kut 33:11**). Hata hivyo, Yesu alikuwa mkuu Zaidi kuliko Musa. Yesu ni Masihi (**Math 1:1, 16-17; 2:4; Yohana 1:41; 4:25-26; Q. 3:45; 4:157, 171-72; 5:72, 75; 9:30**). Yesu alitenda miujiza mikuu kuliko Musa, ikiwa ni pamoja na kufufua wafu na yeye mwenyewe kufufuka kutoka kwa wafu. Yesu ni Zaidi ya Musa kwa sababu ni yeye pekee ambaye alimwona Baba, kwa kuwa alikuja kutoka kwa Baba (**Yohana 6:46**) na ni yeye mwenyewe “*Mwakilishi halisi*” wa Mungu (**Waeb 1:3**). Na Yesu siyo tu alizungumza neno la Mungu mara kwa mara; badala yake, hakuanzisha chochote kwa mtazamo wake mwenyewe, lakini kila kitu alichokifanya na kusema ni kile ambacho Baba alimwambia afanye (**Yohana 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Sababu ni kwamba Yesu hakulisema neno la Mungu tu lakini Yeye mwenyewe alikuwa ndiye Neno la Mungu lililokuja duniani kama mwanadamu (**Yohana 1:1, 14; Ufu 19:13; Q. 3:39, 45; 4:171**).
- *Kama mtoto mchanga aliyajaribu maisha yao*: Kuna uwazi sambamba baina ya jaribio la Farao na Herode kuwauwa watoto wa Kiebrania (**Kut 1:16; Math 2:16**). Wote Farao na Herode walikuwa watawala wasiomjua Mungu ambao waliogopa kuinuka kwa nguvu ambayo ingeweza kupinga au kuwaondoa wao (angalia **Kut 1:8-12; Math 2:1-3**).
- *Kurudi kutoka Misri*: Wote Musa na Yesu walitoroka kutoka nchi nyingine (**Kut 2:15; Math 2:13-15**). Wote wawili kwenye suala hilo waliambiwa kwa njia isiyokuwa ya kawaida lini warudi, kwa sababu wale waliokuwa wanatafuta kuwaua walikuwa wamekwisha kufa (**Kut 4:19-20; Math 2:19-21**).
- *Uhuru toka utumwani*: Musa aliwaongoza watu wake kutoka utumwani Misri kwenda kwenye maisha mapya yenye uhuru (**Kut 12:29-32**). Yesu aliwaongoza watu wake kutoka kwenye utumwa mkuu wa dhambi, kifo, shetani na utumwa wa sheria, ili kwamba “*Naye alipokuwa akisema hayo, wengi walimwamini. Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa kwenye neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.*” (**Yohana 8:30-31**).
- *Manna*: Kama vile ambavyo Bwana alivyotoa manna wakati Musa akiwaongoza Wana wa Israeli Jangwani (**Kut 16:1-21**), hivyo Yesu alisema, “*Amin, amin, nawaambieni, Siye Musa aliyewapa chakula kile cha mbinguni, bali Baba yangu anawapa ninyi chakula cha kweli kitokacho mbinguni. . . . Mimi ndimi chakula cha uzima.*” (**Yohana 6:32, 35**) Manna ilikuwa ya kimwili na ya muda. Mkate ambao Yesu alitoa (Yeye mwenyewe) hutoa uzima wa milele kwa kila aulaye (**Yohana 6:48-58**).
- *Maji kutoka mwambani*: Musa aliupiga mwamba jangwani, na kuwapa watu maji (**Kut 17:6; Hesa 20:11; Zab 78:15**). Kwenye **1 Wakor 10:4**, Paulo anaonyesha kwamba Waisraeli halisi “*waliunywea mwamba wa Kiroho . . . na mwamba huo alikuwa ni Kristo.*” Ingawa maji yaliyotoka kwenye mwamba ambao Musa aliupiga jangwani yalitoa uzima wa mwili kwa watu, Yesu anatoa “*maji yaliyo hai*” kwa

uzima wa milele (**Yohana 4:10-14; 7:36-39**). Typolojia haikuishia hapo. Musa hakuruhusiwa kuwaongoza watu wake kuingia nchi ya ahadi kwa sababu aliupiga mwamba kwa mara ya pili ili kupata maji badala ya kuuzungumzia mwamba kama ambavyo Mungu alimwagiza (**Hes 20:8-12**). Siyo tu kwamba ilikuwa ni kutokumtii Mungu, lakini ilikuwa ni kuitafsiri vibaya/kuipotoshia Injili. Sababu ni kwamba, kama mwamba, Kristo alipigwa kwa fimbo ya haki ya Mungu mara moja tu, siyo mara mbili: alifanya “*alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele*” (**Waeb 10:12**; angalia pia **Waeb 10:10, 14**).

- *Sheria za Mungu Mlimani*: Kama ambavyo Mungu alimpa Musa sheria zake mlimani (**Kut 19:20**), hivyo Yesu alitoa sheria zake mlimani (**Math 5:1-2**). Viyo hivyo, zote mbili zilikuwa kwenye viwango tofauti, kama ambavyo mtume Yohana anavyosema: “*Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*” (**Yohana 1:17**).
- *Sadaka na Upatanisho*: Ingawa Musa alitoa na kufanya upatanisho na sadaka kwa ajili ya dhambi za watu wake (**Kut 32:30-32**), Hakika Yesu alifanya upatanisho na kujidhabihu mwenyewe kwa ajili ya dhambi za watu wake (**Warumi 3:23-25; 5:6-8; Waeb 9:26-28; 10: 11-12; 1 Yohana 2:2**).
- *Nyuso kung’aa*: Kama ambavyo uso wa Musa uling’aa alipokuwa akirudi kutoka mlima Sinai baada ya kupokea Amri kumi kwa mara ya pili (**Kut 34:29**), hivyo uso wa Yesu na mavazi yake kwenye mlima wa uhamisho (ugeuko) (**Math 17:2; Marko 9:2-3; Luka 9:29**). Luka anaeleza kwamba kwenye mlima wa uhamisho (mgeuko) Yesu, Musa, na Elia walikuwa wakijadili “*kutoka*” kwa Yesu mwenyewe [Neno la Kigiriki limetafsiriwa kama “kuondoka”] (**Luka 9:30-31**).
- *Wapatanishi*: Kama ambavyo Musa alivyokuwa mpatanishi kati ya Mungu na Wana wa Israeli (**Kut 20:19; Kumb 5:5; Wagal 3:19**), hivyo Yesu ni “*na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja*” (**1 Tim 2:5**).
- *Agano*: Kwenye karamu ya mwisho Yesu alisema “*hii ni damu yangu ya Agano*” (**Math 26:28; Marko 14:24**). Hili linafanana na neno la Musa kwenye **Kut 24:8**. Hata hivyo, Musa alilihuisha Agano la Mungu na Musa kwa damu ya wanyama (**Kut 24:8**), lakini Yesu alikuwa zaidi ya Musa kwa kuliweka Agano jipya kwa damu yake mwenyewe (**Math 26:28; Marko 14:24; Luka 22:20**; angalia **1 Wakor 11:25; Waeb 8:7-13; 9:11-14**), ambalo liliondoa kabisa agano la Musa. Zaidi, agano la Musa halikusamehe dhambi au kutoa uzima wa milele; Agano jipya ambalo Yesu alilianzisha kwa damu yake husamehe dhambi na kutoa uzima wa milele.
- *Wokovu kutoka kwenye kifo*: Yesu alikilinganisha kifo chake na Musa. Yesu alisema, “*Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa*” (**Yohana 3:14**; angalia **Hes 21:9**). Kumwangukia nyoka wa shaba kule jangwani kuliyahifadhi mtu kutokana na kifo cha mwili; kumtazama Yesu kunampa mtu uzima wa milele na kumwokoia mtu na mauti ya pili.
- *Miili iliyokufa*: Miili iliyokufa ya wote wawili Musa na Yesu haiwezi kupatikana. **Kumb 34:6** inasema kwamba Musa alizikwa kwenye nchi ya Moabu, “*lakini hakuna mtu ajuaye mahali alipozikwa hata leo.*” Yesu pia alizikwa, lakini mwili wake hauwezi kupatikana kwa sababu alifufuka! Kama ambavyo Malaika alimwambia Mariamu Magdalene, “*Hayupo hapa, kwani amefufuka, kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa*” (**Math 28:6**).

B. Je Mohamedi ni “Msaidizi” anayetajwa na Yesu kwenye Yohana 14:16; 15:26; 16:7?

Kwenye **Yohana 14:16** Yesu alisema, “*Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele.*” Kwenye **Yohana 14:26** Yesu alisema, “*Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundishayote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.*” Kwenye **Yohana 15:26**, vivyo hivyo alisema, “*Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapeleka kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia.*” Kwenye **Yohana 16:7** aliongeza, “*Lakini mimi nawaambia iliyokweli; yawafaaninyimimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu.*” Neno la Kigiriki lililotafsiriwa “Msaidizi” ni *Paraklētōs* ambalo linamaanisha “mtu aliyeitwa kwa karibu ili kusaidia; au *Mfariji, Wakili, Mwombezi*” (NASB 1995: Yohana 14:16n.1; angalia Danker 2000: *paraklētōs*, 766; Zodhiates 1992: *paraklētōs*, 1107). Haya hizi ni sehemu ya mjadala wote uliogubika eneo lote la **Yohana 14-16**.

Yusuf Ali anaelezea msingi wa nafasi ya Uislamu: “Kwenye Agano Jipya kama lilivyo kwa sasa, Mohamedi alitabiriwa kwenye Injili ya Mtakatifu Yohana, 14:16, 15:26, na 16:7; Mfariji ajaye asingekuwa ‘Roho Mtakatifu’ kama ilivyojulikana na Wakristo, kwa sababu Roho Mtakatifu tayari alikuwepo, kumsaidia na kumwongoza Yesu. Neno la Kigiriki lililotafsiriwa ‘Mfariji’ ni ‘Paracletos’, ambalo ni rahisi kuharibiwa kutokana na neno ‘Periclytos’, ambalo linakaribia usahihi wa tafsiri ya ‘Mohamedi’ au ‘Ahmad.’” (Ali 2006: Q. 3:81n.416)

Laylah anatoa sababu zifuatazo za kwanini Uislamu hung’ang’ania kwamba “Paraclete” aliyeahidiwa na

Yesu ni Mohamedi, siyo Roho Mtakatifu: “Msemu ‘mfariji mwingine’ linaashiria kwamba Yesu mwenyewe alikuwa mfariji aliyetumwa na Mungu. Hii ni kusema kwamba Paraclete siyo Roho Mtakatifu wa Mungu kama ambavyo Wakristo wangetamani iwe. Maelezo na utendaji aliyopewa mfariji kwenye Injili ya Yohana yanawiana na nabii, na siyo Roho Mtakatifu. Kama hili likiwa hivyo, Yesu alikuwa nabii, kama ambavyo aliitwa mara na tena kwenye Injili nne. Hapa ninataka kusisitiza kwamba neno ‘mwingine’ kwenye maelezo ya Yesu kwa njia yeyote hayawezi kumhusu Roho Mtakatifu, kwa kuwa yupo Roho Mtakatifu mmoja tu, siyo wawili wala zaidi. Hivyo ni nje ya mazingira kusema kwamba Yesu alimwomba Mungu amtume Roho Mtakatifu mwingine. Ni muhimu kuonyesha kwamba Yesu aliainisha kazi za msaidizi ajaye, nabii, kama kuwafundisha wafuasi wake kila kitu, kuwakumbusha yale yote aliyoyasema, na kuwa shahidi wake. Kwa mafafanuzi haya Nabii Mohamedi ndiye nabii pekee atakayekuja baada ya Yesu na kuuchukua ushahidi wake.” (Laylah 2005: 50-51; angalia pia Abdul-Mohsin 2006: 202-07; Hilali na Khan 1998: 909-10; Emerick 2004: 224)

Nasema tena, Muislamu yeyote mwenye madai kama hayo kwenye mistari hii hayuko sahihi.

1. Biblia kwa uwazi inamtambulisha “Msaidizi” (“Mfariji”; “Wakili”) kama Roho Mtakatifu. Yohana 14:17, 26; 15:26; na 16:13 kwa wazi anamtambulisha “Msaidizi” ambaye Yesu aliahidi kumtuma kama “*Roho wa Kweli*.” Roho huyo—Msaidizi—ndiye mwenyewe ambaye kwa wazi alitambulishwa kama “*Roho Mtakatifu*” kwenye **Yohana 14:26**. Uislamu wanadai kwamba kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuwepo tayari na akitenda kazi duniani Msaidizi aliyeahidiwa hawezi kuwa Roho Mtakatifu. Wanakosea kwa sababu Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu angekuja kwa njia nyingine mpya: Kwa sasa angekuja *kukaa ndani* ya Waamini jambo ambalo halikuwahi kuwa kweli kabla. Yesu anasema kwenye **Yohana 14:17** kuhusiana na Roho Mtakatifu (i.e., “*Roho wa kweli*”), “*ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.*”

Hapo mwanzo kimsingi watu walikuwa wakiongozwa na sheria za nje, Sheria za Musa; Roho alikuwa anakuja juu ya watu maalum kuwawezesha kwa kazi maalum lakini baadaye aliondoka. Sasa, Yesu anaahidi kwamba Roho kwa hakika atakaa na, kudumu ndani na kuwaongoza wale wote ambao wameunganishwa na Kristo kwa njia ya Imani. Hii ndiyo sababu **Warumi 8:14** inasema, “*Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.*”

2. Yesu’ kumtaja msaidizi “mwingine” (Paraclete) alimaanisha Roho Mtakatifu. Laylah yupo sahihi kusema, “Msemu ‘Msaidizi mwingine’ inaonyesha kwamba Yesu mwenyewe alikuwa Msaidizi aliyetumwa na Mungu” na “Yupo Roho Mtakatifu mmoja tu, siyo wawili au zaidi” (Laylah 2005: 50-51). Hata hivyo, alikosea sana kwenye hitimisho lake. Kwa uwazi kabisa Yesu hakudai kwamba yeye ni Roho Mtakatifu; alikuwa Mwana. Lakini kama ambavyo Yesu ni Mungu, vivyo hivyo na Roho ni Mungu. Kama tulivyoona kwenye majadiliano ya Utatu, wahusika wote wa Utatu wanayo asili moja au kiini; kama Feinberg alivyoliweka, “kwakuwa kipo kiini kimoja tu cha Ungu hushiriki sawa kwa watu wote watatu, zipo hisia ambazo watu wote watatu ‘hufanya’ chochote mmoja wao afanyacho” (Feinberg 2001: 495). Hivyo, kwa kila kifungu mahali ambapo Yesu aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu (**Yohana 14:17**), pia alisema, “*Naja kwenu*” (**Yohana 14:18**). Kwenye hali hiyo, uwepo wa Yesu ni uwepo wa Roho Mtakatifu na *kinyume chake*. Kwa nyongeza, Carson anaieleza, “Msaidizi mwingine’ kwa mazingira ya Yesu kuondoka inamaanisha kwamba Wanafunzi tayari wanaye mmoja, mmoja ambaye anaondoka. Ingawa kamwe kwenye Injili nne Yesu hakuelezwa kama msaidizi (*paraklētōs*), cheo hicho kinatumika kwake kwenye 1 Yohana 2:1.” (Carson 1991: 500) Zodhiates anaongeza, “Kristo anamweleza Roho Mtakatifu kama Msaidizi (Paraclete) (Yohana 14:16), na kumwita Yeye *allos*, mwingine, ambaye anamaanisha mwingine mwenye sifa sawa na Yeye na siyo *heteros*, mwingine mwenye sifa tofauti na Yeye. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu aliyeelezwa na Yesu Kristo kama mwenye uwezo sawa na Yeye mwenyewe, i.e., Mungu (1 Yohana 2:1). . . . Roho Mtakatifu anaitwa Msaidizi kwa sababu Aliipokea Ofisi ya Kristo hapa ulimwenguni wakati ambao Kristo hayupo hapa ulimwenguni kama Mungu- kwenye mwili wa mwanadamu. Kwa nyongeza, Roho Mtakatifu anaitwa Msaidizi kwa sababu anatenda kama Mbadala wa Yesu hapa duniani. Wakati Kristo kwenye Yohana 14:16 alipojieleza mwenyewe kama Msaidizi, sawasawa na kama Roho Mtakatifu, Ulimwengu hauwezi kumuelewa kama ilivyofanyika kwa Kristo kwenye hali sawa kama 1 Yohana 2:1 ambapo inamtaja wakili wetu mbadala ambaye anatumbea mahitaji yetu kwa Baba. Badala yake inaweza kuchukuliwa kama Yeye ambaye humwomba Mungu kwa ajili ya mahitaji yetu (angalia Yohana 14:7-9).” (Zodhiates 1992: *paraklētōs*, 1107)

3. Yesu angemweleza tu Paraclete kama Roho Mtakatifu, siyo nabii. Uislamu wanashindana kwamba “Yesu aliainisha kazi za Msaidizi ajaye, nabii, kama kuwafundisha wafuasi wake mambo yote, kuwakumbusha yale yote ambayo aliyasema, na kuwa shahidi wake. Kwa mafafanuzi hayo Nabii Mohamedi ndiye nabii pekee ambaye angekuja baada ya Yesu na kuwa ushuhuda wake.” (Laylah 2005: 51) Msaidizi hawezi kuwa nabii kwa sababu zifuatazo:

- Kwanza, wakati Yesu akiwa Nabii alikuwa Zaidi ya Nabii—alikuwa Mungu. Aliahidi kumtuma “Msaidizi mwingine” (“mwingine mwenye sifa kama zake,” Zodhiates 1992: *paraklētōs*, 1107) akimaanisha kwamba Msaidizi pia ni lazima awe Mungu.
- Pili, Yesu aliwaambia Wanafunzi wake, “*Nitampeleka kwenu*” (Yohana 16:7). Hakuahidi kumtuma mtu Arabuni miaka 600 baadaye, ambaye asingefanya chochote chema kwa wanafunzi au kwa wafuasi wa Yesu.
- Tatu, Yesu alisema Msaidizi “*atakuwa nanyi milele*” (Yohana 14:16). Hakuna Nabii mwanadamu atakayekaa na watu “milele”; ni Mungu asiye na mwisho pekee, kwenye utu wa Roho Mtakatifu, ambaye anaweza kuwa na watu milele.
- Nne, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba “*bali ninyi mnamtambua, maana anaka kwenu*, (Yohana 14:17). Roho Mtakatifu, kwenye Utu wa Yesu, kweli alikuwa tayari “pamoja” na Wanafunzi; lakini hawakujua na wala wasingemjua Mohamedi ambaye hakuwa amezaliwa ni mpaka baada ya zaidi ya miaka 500 iliyofuata.
- Tano, Roho “*atakuwa ndani yenu*.” Mohamedi kwakweli hawezi kukaa ndani ya watu.
- Sita, Yesu alisema, “*Ulimwengu hauwezi kumpokea [Msaidizi], kwa sababu haukwona Yeye au Kumjua Yeye*” (Yohana 14:17). Hili haliwezi kuwa linamtaja Mohamedi au nabii yeyote mwanadamu kwa sababu Mohamedi alionekana na kujulikana. Lakini ulimwengu hauwezi kumwona ama kumjua Msaidizi kwa sababu yeye “siyo mwanadamu; Yeye ni Roho wa Mungu ambaye huchagua ni nani atakayemjua Yeye. Kwa kuwa Mfariji ni Roho, ulimwengu hauwezi kumwona Yeye na, Wale tu ambao anaka ndani yao wanaweza kumjua Yeye—siyo ulimwengu wote.” (Sundiata 2006: 274)
- Saba, Ahadi ya [Yohana 14:26] ilikuwa na mtazamo wa uongozi wa Roho kwa kizazi cha kwanza cha wanafunzi, siyo kwa Wakristo wote ambao wangufuata. Kusudi la Yohana kuiongeza mada hii na mstari huu ni . . . kuwaeleza wasomaji mwishoni mwa karne ya kwanza jinsi gani mashahidi wa kwanza, wanafunzi wa kwanza, walivyokuwa na uhakika na uelewa kamili wa ukweli wa Yesu Kristo.” (Carson 1991: 505) Kwa uwazi Mohamedi asingeweza kufanya hivyo kwa sababu hata hakuwa amezaliwa mpaka baada ya miaka Zaidi ya 500 baadaye, na hata baada ya kuwa nabii hakuwahi kufanya kile ambacho Yesu alisema Msaidizi angekifanya.
- Nane, Yesu alisema kwamba Roho “*atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari*” (Yohana 16:14). “Yesu mwenyewe ndiye kweli [Yohana 14:6]; sasa Roho wa kweli huwaongoza wanafunzi kwenye matokeo yote ya kweli, kwenye ufunuo, kimsingi aliunganishwa na Yesu Kristo. Hakuna chembe nyingine ya ukweli; huu ni *ukweli wote*.” (Carson 1991: 539-41) Mohamedi hakufanya chochote kati ya hivi; mtazamo wake haukuwa kwenye kumtukuza Yesu bali yeye mwenyewe. Hakika, “wakati hatimaye Mohamedi alipofika, hakuwa mfariji wa Wayahudi wala kwa Wakristo: Mohamedi aliwakatili na kuwataka wafuasi wake kuendeleza pale ambapo aliachilia. Yesu hakuwa mhuzunishaji—hivyo, Asingeliweza kamwe kuahidi mtu kama Mohamedi kwa wanafunzi wake Wayahudi na kumwita ‘Mfariji mwingine.’” (Sundiata 2006: 274)

4. Madai ya Uislamu kwamba *Paraklētōs* ni uharibifu wa neno *Periclytos* kwa hakika hayana msingi.

Madai ya Uislamu kwamba “Paracletos ni usomaji ulioharibiwa wa neno Periclytos [ambalo linamaanisha ‘Mtu asifiwaye’], na kwamba kwenye misemo yao ya asili ya Yesu kulikuwa na unabii wa nabii wao *Ahmad* [ambalo pia linamaanisha ‘Mtu asifiwaye’] kwa jina” (Ali 2006: Q. 61:6n.5488). Madai haya hayana msingi wowote. Kumbuka kwamba kulikuwa na maandiko mengi ya zamani ya Agano Jipya ambayo yalikuwa ya wakati wa Mohamedi. Gilchrist anaonyesha, “Hakuna ushahidi wa maandishi wowote ambao neno la asili lilikuwa *periklutos* [i.e., *periclytos*]. Kwa kweli neno hilo halijaonekana popote kwenye Agano Jipya la Kigiriki na kwa hiyo siyo neno la Kibiblia. Madai ya Uislamu hayapo kwenye msingi wowote ulio imara, ushuhuda wa kweli lakini wazi kwenye dhana ya kujifurahisha wenyewe. . . . Hakuna chochote kwenye semi zote nne za Yesu kuhusiana na Mfariji cha kusaidia mjadala kwamba atakuwa ‘Mtu asifiwaye’. . . . Ugumu wa suala hili ni kwamba tunao ushahidi wa wazi wa Uislamu kujaribu kile ambacho wakati wote ni kwa makosa kuushtaki Ulimwengu wa Wakristo kwamba ndio wamefanya, wametajwa kujaribu kubadilisha Biblia kuyafaa mapenzi yao wenyewe!” (Gilchrist 2002: 129-30)

C. *Hitimisho*

Ingawa Uislamu wanajaribu kumpata Mohamedi akiwa amewekwa mahali kwenye Biblia, kifungu cha hapo juu kimsingi ndicho wanachokiangalia. Suala hili lina matokeo muhimu. Kwanza, madai ya Kikorani kwamba Mohamedi alitabiriwa kwenye Biblia siyo tu mambo madogo ya kutokukubaliana baina ya Wakristo na Waislamu lakini huenda kwenye msingi kwamba Yesu ni nani na kutofautiana kwa Ukristo na Uislamu. Sababu ni kwamba Biblia yote ni historia ya jinsi gani, kwa maana ya mpango mkuu ambao unahusisha kuitwa kwa

Ibrahimu na taifa la Israeli, Maandalizi ya njia ya Mungu kuujiia Ulimwengu kwa mwanadamu Yesu Kristo kuleta masamaha ya dhambi na kuurejesha ushirika na Yeye. Hivyo, Agano la Kale ni maandalizi ya Injili; Vitabu vya Injili na madhihirisho ya Injili; Matendo ni upanuzi wa Injili; Nyaraka ni mafafanuzi ya Injili; na Ufu ni matumizi ya Injili. Kiini cha takwimu za Biblia yote—mtu ambaye ni wakala mtendaji wa uumbaji, maana ya ukombozi, na chanzo cha ufupishaji wa uumbaji mpya—ni Yesu Kristo; hakika, hatimaye Agano la Kale lote lilishuhudia kuhusiana na Yesu (angalia **Luka 24:25-27; Yohana 5:39-40, 46; Matendo 3:18, 24; 10:43; 26:22-23; 2 Wakor 1:20; Waef 1:9-10; Wafil 2:6-11; Waeb 1:1-3; 1 Pet 1:10-12**). Moja ya matokeo ya hili ni kwamba hakuna hata mmoja atakayekuja baada ya Yesu—na anaonyesha hakuna mwingine yeyote—kwa sababu Yesu mwenyewe ni matumizi na ukamilifu wa mpango wote wa Mungu. Kulikosa hili ni kukosa mstari wote wa historia ya Kibiblia.

Pili, Uislamu kutafuta kumpata Mohamedi kwenye Biblia hudhoofisha madai ya Kiislamu kwamba Biblia iliharibiwa. Kwa kumtafuta na kuitafsiri Biblia kutafuta unabii wa Mohamedi huko, Uislamu wanaendelea kwenye msingi kwamba Biblia haikuharibiwa. Kwa ujumla, wazo kwamba Mohamedi alitabiriwa kwenye Biblia siyo tu kwamba siyo sahihi, lakini siyo sahihi kiasi cha kina Zaidi ya ufafanuzi halisi wa vifungu vya Biblia vinavyoweza kushauri.

VI. Maendeleo ya Korani

Korani maana yake ni “kukariri” au “kusoma.” Korani inasemekana kuwa neno halisi la Allah, likidumu milele kwenye vibao mbinguni (**Q. 85:21-22**). Kulingana na imani ya Kiislamu, Korani ilisimuliwa, kipande kwa kipande, na malaika Gabrieli kwa Mohamedi kwa kipindi cha miaka 23 (**Q. 17:106; 25:32**). “Uislamu wanaamini kwamba Yeye [Mohamedi] aliandaa mpangilio wa sura zote na aya zote chini ya maelekezo ya malaika mkuu Gabriel” (Emerick 2004: 235). Ukweli halisi unaeleza jambo tofauti.

A. *Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetoka kwa Umar bin Al-Kattab au Uthman bin Afan*

Ingawa Uislamu wanaendeleza kwamba maneno yote kwenye Korani ni neno halisi kutoka kwa Allah yaliyoletwa na Gabriel, ahadithi zinafunua kwamba marafiki wa karibu wa Mohamedi, Umar bin Al-Khattab alikuwa chanzo cha baadhi ya vifungu na uhusika wa Uthman bin Afan kwa mtu ambaye alikuwa auawe alikuwa chanzo cha angalau moja.

- *Kubadili mwelekeo wa maombi kutoka Yerusalemu kuelekea Kab’ah huko Maka (Q. 2:125)*. Umar likuwa ndiye chanzo cha hili (al-Bukhari: 402; vol. 6, book 60, no. 10; Muslim: 2399)
- *Kutokuwafanya maombi ya mazishi kwa wasio- waamini (Uislamu) (Q. 9:84)*. Umar alikuwa ndiye chanzo cha hili (at-Tirmidhi: vol. 5, book 44, no. 3097)
- *Msamaha kwa wale wanaoupigania Uislamu (Q. 16:110)*. Umar alikuwa ndiye chanzo cha hili (an-Nasa’i: 4069)
- *Kanuni za mavazi ya wanawake (Q. 24:31; 33:59)*. Umar alikuwa ndiye chanzo cha hili (al-Bukhari: 146; see also 6240; vol. 6, book 60, no. 10; Muslim: 2399)
- *Mwito wa maombi (Q. 62:9)*. Umar alikuwa ndiye chanzo cha hili (al-Bukhari: 604).
- *Tishio la Mohamedi kuwataliki wake zake (Q. 66:5)*. Umar alikuwa ndiye chanzo cha hili (al-Bukhari: 402; angalia pia vol. 6, book 60, no. 10, 438)

Gilchrist anatolea maoni, “Ugumu wa mazingira unapatikana kwenye wakati wa kila ufunuo husika. Siyo tu Allah hufanya kumpa Mohamedi ushauri halisi kama ‘Umar lakini alifanya mara zote haraka baada ya mshiriki wa karibu wa Nabii alipokuwa amemaliza kusema. Maneno yake ‘Bwana wangu, kubaliana na mimi kwenye mambo matatu’ [al-Bukhari: 402 alianza, ‘Bwana wangu kubaliana na mimi kwenye mambo matatu’ na baadaye husimulia matukio 1, 4, 6, hapo juu] ni ya kuvutia na kuonekana kwamba ushauri wake kwenye kila jambo humgusa Mohamedi kama kuwa sauti halisi na, kwenye njia yake ya upekee, aliyaruhusu kuuangazia ufahamu wake kwenye muundo ule ule kama ambavyo ufunuo mwingine ulivyokuja na kwa namna iyo hiyo ulikuja kuwa sehemu ya maandiko ya Korani kwa muda mfupi sana.” (Gilchrist 1994: 98)

B. *Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetokana na matendo na desturi za kipagani*

Kinyume na madai kwamba kila kitu kwenye Korani kilikuja moja kwa moja kutoka kwa Allah kuja kwa Mohamedi kupitia Gabrieli, dini zilizopo na mazoea ya dini huko Arabia wakati wa Mohamedi kwa uwazi zinatupa vyanzo vya vifaa kwa ajili ya Korani (na kwa Imani nyingi za Kiislamu na mila). Vyanzo hivyo ni pamoja na hivi vifuatavyo:

1. Ushirikina wa Waarabu. Kab’ah iliyoko Maka ni eneo takatifu la Uislamu. Korani inang’ang’ania kwamba Ibrahimu na Ishmael kwa asili ndio walioweka msingi (**Q. 2:125-27**). **Q. 2:144, 149-50** hitaji kwamba Uislamu waelekeze nyuso kuelekea Kab’ah ili kufanya *salat*. Hata hivyo, Ka’bah yenyewe ilikuwa eneo la

miungu ya Wapagani la kuabudia muda mrefu kabla ya Mohamedi kuzaliwa. Mohamedi mwenyewe alihusika kulikarabati wakati akiwa na umri wa miaka 35, i.e., miaka mitano *kabla* ya mwito wake wa kuwa Nabii (Ibn Ishaq 1955: 84). Licha ya miungu ya Kab'ah na ukweli kwamba Allah mwenyewe alikuwa mungu wa Kipagani aliyekuwa anaabudiwa hapo Kab'ah, **Q. 106:3** (Hilali-Khan) aliwaamuru Uislamu “*wamwabudu (Allah) Bwana wa Nyumba hii (Ka'bah iliyoko Maka).*” Safari za wapagani kwenda Kab'ah zilikuwa zinafanyika wakati na kabla ya wakati wa Mohamedi (Ibn Ishaq 1955: 87-88; A'la Mawdudi n.d.: Q. 2:196n.213). Uislamu uliyachukua mazoea hayo (**Q. 2:158, 196**). Kwa kweli, moja kati ya nguzo tano za Imani ya Kiislamu ni kufanya safari ya hija (*hajj*) kwenda Kab'ah (**Q. 3:97**).

2. Uzoroasta. St. Clair-Tisdall anaangalia, “Kwa wakati wa Mohamedi na kabla ya hapo, Waashuru waliendelea kuingiliana na Waarabu (kingono); na kuwa na uwezekano zaidi wa kujifunza kuliko kuendelea kuwa na watu wao wajinga, lazima walikuwa na ushawishi muhimu kwenye dini yao, kwenye desturi zao, na kwenye ujuzi wao kwa ujumla. Vyote historia na wachambuzi wa Kikorani walionyesha kwamba hadithi na nyimbo za Iran zilienea kwa mapana miongoni mwa makabila ya Arabuni.” (St. Clair-Tisdall 1901: 74-75) Daraja jembamba, *sirat*, ambalo ni lazima watu wapiti juu yake wakati wa hukumu “ni asili ya Ashuru, na Uzoroasta wa zamani uliliita *Chînavad*. . . . Maana ya jina hilo la Kiashuru ni ‘kiunganishi husishi,’ Daraja ambalo lilikuwa linaiunganisha dunia na Paradiso.” (Ibid.: 88) **Q. 42:17** inasema, “*Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeteremsha Kitabu kwa haki na mizani. Na ni nini kitakujulisha ya kwamba labda saa ile imekaribia.*” Gilchrist anaeleza kwamba “wazo la mizani kubwa kwenye siku ya Mwisho ni neno lililoazimwa kwenye vyanzo vya kigeni. Kwa Waashuru wa zamani Pahlavi kitabu kilichoitangulia Korani kilijulikana kama *Rashnu* kimefundisha kwamba Malaika wa Haki na moja ya hukumu tatu za wafu huchukuwa ‘Usawa’ ambao matendo ya mtu hupimwa baada ya kifo.” (Gilchrist 1995: ch.4).

3. Agano la Kale, fafanuzi ya Wayahudi, na hadithi za Wayahudi. Mwanazuoni wa Kiislamu Mahmoud Ayoub amekiri, “Kabla ya Uislamu kulikuwa na Wayahudi huko Yemen na Madīna ambao waliendelea kuchukua majukumu muhimu ya kuanzisha Imani ya Kiislamu na mtazamo wa kidunia” na kulikuwa na “fasihi mbalimbali zilizojulikana kama *Isrā’īliyyāt* (tamaduni za ki Israeli) ambao waliingiza tamaduni Uislamu kutoka kwa waongofu Wayahudi” (Ayoub 1986: 3, 4). Kulingana na mtetezi wa Uislamu Jerald Dirks, Korani inataja yafuatayo kwa wahusika wa Agano la Kale kwa muda ufuatao: Musa-177; Ibrahimu-74; Nuhu-47; Yusufu-34; Adamu-25; Sulemani-19; Yakobo-18; Isaka-16; Daudi-16; Ishmael-6 (Dirks 2008: 4).

Korani pia imechukulia kwenye maelezo mbalimbali yaliyopo kwenye Agano la Kale, ingawa imebadilisha baadhi ya mambo yake. Baadhi yake ambayo yanajulikana vema ni:

- Kuumbwa kwa Adamu, Hawa, na bustani ya Edeni (**Mwanzo 2:4-3:24**; linganisha **Q. 2:31; 7:19-25; 15:28-29; 32:7-9; 38:71-72; 55:14**);
- Kaini na Habili (**Mwanzo 4:1-16**; linganisha **Q. 5:27-30**);
- Ndoto ya Yusufu, kuuzwa kwake utumwani, na kuwa kwake mtawala wa Misri (**Mwanzo 37, 39-45**; linganisha **Q. 12:3-101**);
- Musa kwenye kisafina na kumwua Mmisri (**Kut 2:1-14**; linganisha na **Q. 20:36-40**);
- Musa na kichaka kinachowaka moto (**Kut 3:1-4:9**; linganisha na **Q. 20:9-35; 27:7-12**);
- Musa na Farao, mapigo, na kutoka (**Kut 7-14**; linganisha na **Q. 20:41-79; 26:10-68; 51:38-40**);
- Ndama wa dhahabu (**Kut 32**; linganisha na **Q. 20:83-91**); Manna na Kware Jangwani (**Kut 16:1-21**; linganisha na **Q. 20:80-81**);
- Musa na nchi ya Ahadi (**Hes 13:1-14:38; Kut 1:19-40**; linganisha na **Q. 5:20-26**);
- Yona (**Yona 1-4**; linganisha na **Q. 37:139-48**);
- Daudi na Goliathi (**1 Sam 17:17-54**; linganisha na **Q. 2:246-51** [maelezo ya kunywa mtoni, **Q. 2:249**, kwa wazi yametoka kwenye maelezo ya Gideoni kwenye **Waamuzi 7:1-8**]);
- Nabii Nathan kukabiliana na Daudi baada ya Daudi kuzini na Bathsheba (**2 Sam 11:1-12:15**; linganisha na **Q. 38:21-25** [Korani imeondoa kumbukumbu ya zinaa ya Daudi na Bathsheba na kuondoa kumbukumbu ya Nathan, lakini maelezo yapo wazi kwamba yana msingi wa Kibiblia]).¹²

Q. 27:16-44 ni maelezo marefu ya Sulemani (ambaye, kulingana na maelezo, alikuwa na uwezo wa kuelewa lugha za ndege). Malkia wa Sheba kumtembelea Sulemani kulikuwa kumeandaliwa kwa hudhudi.

¹² Baadhi ya Wachambuzi wa Kiislamu wanakataa kwamba tukio hili ni kuhusiana na Bathsheba na Uriah, lakini wanadai kwamba linamtaja Daudi akifanya hukumu kwa misingi wa kusikia kutoka kwenye simulizi ya mmoja wa walalamikaji (angalia Ali 2006: Q. 38:24n.4176-A, Q. 38:26n.4178). Wengine, inaonekana ni pamoja na wachambuzi wa awali, kulihusianisha hili na maelezo ya Kibiblia ya Daudi, Bathsheba, na Uriah. Hata hivyo, wanakataa kwamba Daudi hakika hakuzini na Bathsheba lakini kwamba Daudi alimwona tu, akampenda, na kuhakikisha kwamba Uriah anauawa vitani ili kwamba aweze kumwoa. (angalia Asad 1980: Q. 38:21n.22; Jalal 2017: Q. 38:22, 24, maoni)

Sulemani alitaka kumbadilisha kuwa Muislamu na kuandaa majaribio mbalimbali kwa ajili yake. **Q. 27:44** inasema, “*Akaambiwa: Liingie jumba. Lakini alipoliona, akalidhani kuwa eneo la maji, na akapandisha nguo miundi yake.*” Maoni ya *Tafsir al-Jalalayn* kwenye aya hii anasema kwamba Sulemani “alitaka kumwoa lakini hakupendezwa na nywele (malaika) zilizokuwa kwenye miguu yake. Hivyo shetani alifanya (uharibifu) mchanganyiko wa chokaa (nūra) na kuziondoa zile nywele.” Maoni ya Robert Spencer, “Simulizi hii ya Kikorani ina msingi wake kwenye *Targum ya Esther* ambayo ingawaje imetofautika kutoka kwenye Korani kwa baadhi ya vina, imebeba kanuni zote za msingi za simulizi: wanyama waliokuwa wakiongea, ikiwa ni pamoja na mnyama mmoja aliyekuwa anasita (jogoo kwa desturi za Kiyahudi, badala ya hudihudi), barua kwa Malkia wa Sheba, ambaye alikuwa Mpagani (aliyekuwa akiabudu bahari kwa hadithi za Kiyahudi, badala ya jua kwa toleo la Kiislamu)—hata nywele za miguuni” (Spencer 2009: 48; angalia pia Reynolds 2018: 584-89).

4. **Agano Jipya na Wakristo wa kubuni.** Kulingana na Dirks, Korani inawataja wahusika wa Agano Jipya kwa namba za wakati zifuatazo: Yesu-37; Yohana Mbatizaji-5 (Dirks 2008: 4). Korani pia imechukulia kwenye maelezo tofauti tofauti yaliyopo kwenye Agano Jipya, ingawa walifuta mambo muhimu ya kweli kutokana nayo, ikiwa ni pamoja na kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji (**Luka 1:2-24, 57-66**; linganisha na **Q. 3:38-41**); na kuzaliwa kwa Yesu (**Luka 1:26-38**; linganisha na **Q. 3:42-48**).

Baadhi ya simulizi za Kikorani zina misingi kwa wasioamini au simulizi za Wakristo wa kubuni. Miongoni mwa simulizi za kubuniwa ambazo zilipata upenyu kwenye Korani ni hizi zifuatazo: **Q. 3:35-37, 44** inapendekeza kwamba Mariamu, mama yake na Yesu, yaweza kuwa alitoka kwenye kabila la Lawi, kwamba kwa njia ya miujiza Allah alimpatia chakula, hizo kura zilipigwa kuona ni nani angeaminiwa kwenye kumtunza, na kwamba aliwekwa chini ya uangalizi wa Zechariah (angalia Dirks 2008: 12-13). Dirks anatambua kwamba mambo haya manne ambayo hayakuwepo kwenye Biblia, yalionyeshwa kwenye maandiko ya kubuni *Injili ya kuzaliwa kwa Mariamu* na *Injili ya udanganyifu ya Yakobo* (Ibid.: 13nn.24-27).¹³ **Q. 19:22-26** inasema kwamba Mariamu alizalia chini ya mti wa Mtende na baadaye kwa njia ya kimujiza alipatiwa maji kutoka chini ya ardhi mti na matunda kutoka kwenye mti. Simulizi hii imetolewa moja kwamoja kutoka sura ya 20 ya *Injili ya udanganyifu ya-Mathayo*.¹⁴ **Q. 3:49; 5:110; 19:29-34** inasema kwamba Yesu alizungumza kama mtoto mchanga, aliwaumba ndege kutoka kwenye udongo, na kuwapa uhai. Simulizi hizi zilisimuliwa kwanza kwenye *Injili ya Utoto ya Thomaso*.¹⁵

Ushahidi huo hapu juu una matokeo makini kwa ukweli wa Mohamedi na Korani. St. Clair-Tisdall inaeleza kwamba Uislamu unang’ang’ania kwamba Korani ni ya “asili ya umilele, ikiwa na kumbukumbu mbinguni, na kuwekwa kama ilivyo pale kwenye ‘Meza ya kuhifadhi’ [**Q. 85:21**]. Hivyo Mungu mwenyewe anafanyika kuwa ‘Chanzo’ cha Uislamu; na kama hivyo ndivyo, jitihada zote za kutafuta asili ya mwanadamu kwa sehemu yake yeyote ni lazima iwe ni ubatili. Sasa, kama tukiyafuatilia mafundisho ya sehemu yake yoyote, kwenye vyanzo vya kidunia, au kwa mifumo ya wanadamu iliyokuwepo nyuma kufikia wakati wa Manabii, basi Uislamu kwa ghafla utaanguka mpaka ardhini (St. Clair-Tisdall 1901: 2)

C. Baadhi ya vifungu kwenye Korani vimetokana na maisha binafsi ya Mohamedi

Vifungu vingi vya Kikorani vilihusika na masuala ya maisha binafsi ya Mohamedi na vilikuwa hasa hasa vimebuniwa kwa faida yake mwenyewe na kwa kupenda fedha (**Q. 6:90; 8:1, 41; 59:7; 93:8**), ngono na ndoa (**Q. 4:3, 128; Q. 33:4, 37, 50-51; 66:1-2, 5**), na misukumo binafsi (**Q. 24:62; Q. 33:53, 57; 49:2; 58:12**). Baadhi ya hizi zilikuwa ufunuo maalum “baada ya kweli” (angalia Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 4:128, maoni).

D. Ukusanyaji, marudio, na viwango vya Korani

Kamailivyo kwa Biblia, maandiko asili ambayo yanaifanya Korani hayapotena.¹⁶ Hata hivyo, Waislamu

¹³ *Injili ya kuzaliwa kwa Mariamu* ni “ya kughushiwa kwa makusudi kuingizwa kwenye huduma ya Kanisa takriban karne ya sita, wakati ambao kumwabudu Mariamu kulikuzwa hasa Kanisani” (Hutchinson 1939: sec.III.1.c). *Injili ya Yakobo* ni udanganyifu (i.e., mwasisi wake halisi aliihuisha kwenye takwimu za zamani) alifanya kazi hiyo kutoka takriban AD 145 (“*Injili ya udanganyifu ya Yakobo*” 1015: Uandishi mnamo mwaka). Reynolds anakumbusha kwamba *Injili ya Yakobo* “ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiashuru kunako karne ya tano” (Reynolds 2018: 115).

¹⁴ *Injili ya udanganyifu ya Mathayo* ni “mawasiliano ya kughushi baina ya Jerome na maaskofu wawili wa Kiitaliano [kutoka] siyo Zaidi ya mwanzoni mwa karne ya tano” (Hutchinson 1939: sec.III.1.b).

¹⁵ *Injili ya kitoto ya Thomaso* ni simulizi ya udanganyifu ya Kijana Yesu, iliyoandikwa takriban mwaka AD 140-170 (*Injili ya kitoto ya Thomaso*: ina matukio yaliyotofautiana ya mwaka). Gilchrist 2015 ni kwa jinsi gani nyaraka za Korani zinazomwonyesha Yesu zilivyochukuliwa kwenye vyanzo vya kubuniwa.

¹⁶ Muislamu Ahmad von Denffer anaeleza, “Mengi ya maandiko ya asili ya awali ya Korani, yote au kwenye ukubwa wa vipande, hayo tunayo hata sasa, siyo ya awali zaidi ya karne ya pili baada ya Hijra. Nakala za awali kabisa, ambayo yalithibitishwa kwenye makumbusho ya British wakati wa sherehe ya ulimwengu wa Uislamu mwaka 1976, zenye tarehe

wanasisitiza kwamba Korani iliyopo leo ni halisi kama ilivyotolewa na Gabriel kwa Mohamedi miaka 1400 iliyopita. Wanadai kwamba “Allah alithibitisha kuulinda kutokana na kuvurugwa na kubadilishwa, na kutokuwa na chochote kitakachoongezwa au kupunguzwa, mpaka wakati ambao Allah atakapoiondoa (kutoka ulimwenguni humu), jambo ambalo litatokea kabla ya siku ya kufufuliwa” (al-Athari 2005: 96). Ajijola anaeleza kwamba “haijawahi kamwe kubadilishwa ikiwa kwenye mikono ama ya rafiki zake au maadui zake, kwa ama waliosoma au wasiojua kusoma, kitabu cha wakati huo ambacho hakikuwahi kuchakaa lakini ambacho kilibakia kama ambavyo kilifunuliwa na Mungu kwa Mtume wake, Nabii wa mwisho miongoni mwa wote” (Ajijola 1972: 158). Historia ya Korani inaonyesha picha tofauti.

1. Korani wakati wa Mohamedi. Kama Mohamedi alivyopokea ufunuo wake, aliusoma kwa kinywa. Muislam Ahmad von Denffer anatambua, “Nabii Mohamedi hakuwakilisha kwa washiriki wake ufunuo uliokusanywa na kupangiliwa kwenye kitabu kimoja” (von Denffer 1981: 14; angalia pia Karim 1939: 3:664 (“Hakuna nakala ya Korani iliyopo iliyokuwa imekamili wakati wa Nabii mtakatifu”). “Sura za Korani hazikupangiliwa kwa mtiririko wa nyakati kama zilivyofunuliwa” (Ali al Imam 1998: 38; angalia pia von Denffer 1981:14 [“Aya na sura wakati wote hazikufunuliwa kwenye mpangilio wake wa mwisho, lakini zilipangiliwa baadaye”]). Hili linathibitishwa kwenye Hadithi ambazo zinatambua kwamba baada ya Mohamedi kufa kulikuwa tu na “maandiko yasiyokamilika” ya sehemu ya Korani kwenye maandishi (al-Bukhari: 4986, 7191; angalia pia vol. 6, book 60, no. 201).

Mohamedi peke yake alikiri kwamba *kulikuwa na matoleo saba tofauti ya Korani*: “Ilisimuliwa na Umar bin Al-Khattab: Nilimsikia Hisham bin Hakim akiikariri Surat Al-Furqan wakati wa uhai wa Mjumbe wa Allah na nilisikiliza na kwenye kukariri kwake niligundua kwamba alikuwa anakariri kutoka kwenye chanzo tofauti na ambacho Mjumbe wa Allah hakuwa amenifundisha. Nilikuwa karibu kumrukia wakati wa maombi, lakini nilituliza hasira yangu, na alipomaliza maombi yake, Niliishika kanzu yake ya juu nikaizungusha shingoni mwake nikamkaba nayo na kusema, ‘Ni nani aliyekufundisha surat hii ambayo nimekusikia ukiikariri?’ Alijibu, ‘Mjumbe wa Allah alinifundisha hivyo.’ Nikasema, ‘Umenidanganya, kwa kuwa Mjumbe wa Allah alinifundisha mimi kwa njia tofauti na aliyokufundisha wewe.’ Hivyo nilimburuza hadi kwa Mjumbe wa Allah na kumwambia (Mjumbe wa Allah), ‘Nilimsikia mtu huyu akikariri Surat Al-Furqan kwa njia ambayo hukunifundisha mimi!’ Kwenye hili Mtume wa Allah alisema, ‘Mwachie, (Ewe Umar!) Ewe Hisham kariri!’ Hivyo alikariri kwa njia ileile kama ambavyo nilimsikia akikariri. Basi Mjumbe wa Allah akasema, ‘Ilifunuliwa kwa njia hiyo,’ na aliongeza, ‘Kariri, Ewe Umar!’ Niliikariri kama ambavyo alinifundisha. Basi Mjumbe wa Allah alisema, ‘Ilifunuliwa kwa njia hiyo. Korani hii ilifunuliwa ili ikaririwe kwa njia saba tofauti, hivyo ikariri kwa njia yeyote iliyo rahisi kwako (au soma uwezavyo kama utakavyoona rahisi kwako).’” (al-Bukhari: 4992; angalia pia 4991, 5041) Tofauti hizi hazitakuwa tofauti rahisi kwa lahaja au matamshi, lakini yaweza kuwa utofauti wa vipengele, au vinginevyo Umar asingepatwa na hasira na kumkaba Hisham bin Hakim kwenye shingo yake! Hadithi nyingine zinazungumzia tukio hilo hilo. Kwa mfano, Ibn Mas’ud alisema, “Nilimsikia mtu akikariri (Kikorani) Aya kwa njia fulani, na nilikuwa nimemsikia Nabii akikariri Aya ilire ile kwa njia tofauti. Hivyo nilimchukua kwa Nabii na kumtaarifu kuhusiana na hilo lakini nilitambua ishara ya kutokukubaliana kwenye uso wake, na kasha alisema, ‘Nyote wawili mko sawa, hivyo msitofautiane, kwa kuwa mataifa yaliyo mbele yenu yalitofautiane, hivyo yaliangamizwa.’” (al-Bukhari: 3476; angalia pia 5062; an-Nasa’i: 941)

Ukusanyaji halisi, marudio, na viwango vya Korani—ambako kulihusisha kuharibiwa kimataifa kwa yaliyokuwepo kabisa na sehemu ya maandiko ya Korani ambavyo vilikuwepo tangu wakati wa Mohamedi—vilianza baada ya kifo cha Mohamedi. Mchakato huo ulikuwa kama ifuatavyo:

2. Ukusanyaji wa awali wa Korani chini ya Abu Bakr. Washiriki kadhaa wa Mohamedi walikuwa wasomaji wa Korani; watu hawa walijulikana kama *Qaris*. Baada ya kifo cha Mohamedi, mmoja wa wasomaji (*Qaris*), Zaid bin Thabit, anaeleza kwenye hadithi, “Abu Bakr alinitaka mimi kuwalipa kundi kubwa la majeruhi wa vita vya Al-Yamama, wakati Umar alipokuwa amekaa pamoja naye. Abu Bakr akaniambia, Umar alikuja kwangu na kusema, ‘Idadi kubwa ya wasomaji wa Korani Takatifu waliuawa kwenye siku ya vita vya Al-Yamama, na ninaogopa kwamba majeruhi miongoni mwa wasomaji wa Korani wanaweza kuongezeka kwenye uwanja wa vita mahali ambapo sehemu kubwa ya Korani yaweza kupotea. Kwa hiyo ninashauri kwamba wewe Abu Bakr hakikisha Korani inakusanywa.’ Nikasema, ‘Nitathubutuje kufanya kitu ambacho Mjumbe wa Allah hakufanya?’ Umar alisema, Kwa Allah ni jambo la faida.” (al-Bukhari: 7191, fafanuzi imeongezwa; angalia pia 4986, vol. 6, book 60, no. 201) Zaid anasimulia kile alichokifanya, “Hivyo nilianza kuiangalia Korani na kukusanya kutoka kule ambako ilikuwa imeandikwa kwenye mabua ya mitende, mawe meupe membamba na pia kutoka kwa watu ambao walikuwa wanaielewa kwa moyo, mpaka nilipoipata aya ya mwisho ya Surat at-

ya mwishoni mwa karne ya pili. . . . Hata hivyo, vipo vipande visivyokuwa vya kawaida vya upotofu wa Kikorani vinavyopatikana, ambavyo vinaonekana kuwa vya karne ya kwanza.” (von Denffer 1981: 25)

Tauba (Toba) na Abi Khuza'ima Al-Ansari, na sikuipata kwa mwingine yeyote zaidi yake. . . . Nakala iliyokamilika ya Korani ilibaki na Abu Bakr hadi alipokufa, tena na Umar hadi mwisho wa maisha yake, na baadaye ilibaki kwa Hafsa, binti yake na Umar.” (al-Bukhari: 4986)

Hata hivyo, uchunguzi wa Zaid haukudhaminiwa kuisahihisha Korani yote. “[Hadithi] kwa uwazi zinaeleza kwamba vipengele vya Korani vilipotea kwenye vita vya Yamama wakati ambao washiriki wengi wa karibu wa Mohamedi ambao walikuwa wameyakariri maandiko walipoangamizwa: ‘Vifungu vingi vya Korani ambavyo viliteremshwa chini vilijulikana na wale waliokufa siku ya vita vya Yamama ... lakini havikujulikana na wale ambao walisalia, wala hawakuwa wameviandika, wala Abu Bakr hakuwa amefanya hivyo, Umar au Uthman (kwa wakati huo) hawakuwa wameikusanya Korani, wala hawakumpata hata mtu mmoja baada yao.’ (Ibn Abi Dawud, *Kitab al-Masahif*, p.23). Athari hasi za vifungu hivyo ni vigumu kukosekana: *lam ya 'alam* – ‘haijulikani’, *lam yuktub* – ‘haikuandikwa’, *lam yuwjad* – ‘haikupatikana’, msisitizo wa mafungu hayo matatu kwenye ukweli kwamba sehemu hizi za Korani ambazo zilifukiwa na wasomaji ambao walikufa kwenye vita ya Yamama vilipotea milele na havitaweza kupatikana tena.” (Gilchrist 1989: ch.1.3)

3. Marekebisha ya Korani yaliyofanywa na Uthman. Takribani miongo miwili baada ya kifo cha Mohamedi: “Generali wa Kiislamu Hudhayfah ibn al-Yaman aliongoza safari kwenda Ashuru ya Kaskazini, akachukua sehemu ya vikosi vyake kutoka Ashuru na sehemu kutoka Iraki. Haikuchukua muda kabla ya mgongano kujitokeza kati yao juu ya usomaji ulio sahihi wa Korani. Wale waliotoka Damascus na Hems, kutoka Kufa na Basra, na kwenye kila kituo Uislamu wa kawaida walikuwa na mfumo wao wa maneno ya Korani.” (Gilchrist 1989: ch.2.2) Hali ilikuwa mbaya zaidi kuliko hiyo. Ahmad Ali al Imam anaeleza, “Wakati wa Uthman, kutokuelewana au mgogoro miongoni mwa wasomaji kulikuwa juu sana kiasi kwamba walishtakiana kila mmoja na mwingine kwa kutokuamini (*kufr*). Malalamiko mengi yaliletwa mbele ya Uthman [khalifa wa tatu], wakimsihi achukue hatua kuzuia mapigano na mgawanyiko miongoni mwa Waislamu. Mgogoro kama huo ulitokea maeneo mengi: Madina, Kufah, Basrah, Syria, na kambi za jeshi (*ajnad*).” (Ali al Imam 1998: 26)

Sunan al-Bukhari anaeleza kile kilichotokea baadaye: “Hudhaifa alikuwa na hofu juu ya tofauti zao (na watu wa Sham na Iraki) kwenye kuikariri Korani, hivyo alimwambia Uthman, ‘Ewe mkuu wa Waamini! Liokoe taifa hili kabla halijatofautiana juu ya Kitabu (Korani) kama ambavyo Wayahudi na Wakristo walivyofanya kabla.’ Hivyo Uthman alituma ujumbe kwa Hafsa akisema, ‘Tutumie maandiko ya Korani ili kwamba tuweze kuikusanya Korani kwenye nakala zilizo kamilifu na nitakurudishia nakala yake kwako.’ . . . Baada ya hapo Uthman aliwaagiza Zaid bin Thabit, Abdullah bin AzZubair, Said bin Al-As na AbdurRahman bin Harith bin Hisham kuyaandika tena maandiko kwenye nakala kamilifu. Uthman akawaambia hao wanaume watatu wa Quraishi, ‘Ikiwa mtashindwa kuafikiana kwenye jambo lolote na Zaid bin Thabit kwenye uandishi wa Korani, basi liandikeni kwenye lahaja ya KiQuraish, ambayo ndiyo lugha ambayo Korani ilifunuliwa kwayo.’ Walifanya hivyo, na walipoziandika nakala nyingi, . . . Uthman alizituma kwenye kila mkoa wa Kiislamu nakala moja ya kile walichokuwa wamekinakili, *na aliagiza kwamba vifaaa vinginevyo vyovyote vya Kikorani, ikiwa vimeandikwa kwenye vipande vya maandiko au nakala nzima, vichomwe moto.*” (al-Bukhari: 4987, fafanuzi imeongezwa)

“Uislamu wanapaswa kukiangalia na kukitafakari kwa kina kitendo alichokifanya Uthman. Korani iliainika kuwa Neno la Mungu lililofunuliwa. . . . *Uthman alichoma na kuangamiza kabisa maandishi yote ya nakala za Korani zilizonukuliwa na washiriki wa karibu wa Mohamedi.* . . . Ni fafanuzi moja tu laweza kutolewa kwa maelezo haya – hapa ni lazima yaweza kuwa zilikuwepo tafsiri nyingi tofauti tofauti baina ya maandishi yenyewe ambayo Khalifa aliona suluhisho moja tu – kuimarisha moja ya haya kama andiko maalum kwa jamii yote ya Uislamu na kuyafuta mengine.” (Gilchrist 1989: ch.2.2, fafanuzi imeongezwa)

4. Matoleo tofauti ya kisheria ya Korani. Mwanazuono Muislamu Cyril Glasse anaeleza, “Baada ya kukamilika kwa toleo la mwisho [toleo lililorekebisha] la Korani lililofanywa kwa agizo la Khalifa Uthman, maandiko tofauti yalikuwepo na, kwa hakika, yalidumu na kuongezwa kama ya washiriki ambao walikuwa wakikariri ujumbe waliokufa, na kwa sababu ya kutokuendelezwa maandiko ya Kiarabu, yanakosa ishara za vokali na hata alama za lazima za kutofautisha baina ya konsonati za kweli hazijitosheshezi.” (Glasse 2013: *Qira'ah*, 436) Kwa maneno mengine, “wakati Uthman alipotengeneza Korani yake maandiko ya Kiarabu hayahusisha alama za vokali au nukta zilizotumika kutofautisha baina ya herufi fulani. Utata huu uliruhusu maneno kuundwa (kutamkwa au kusomeka) kwa njia tofauti” (Green 2016: ch.11) Vivyo hivyo, Abu Bakr Ibn Mujahid (AD 859-936) “aliamua kuwa na matumizi ya ‘usomaji’ (*qira'at*) uliotolewa kwa mamlaka saba za “wasomaji” (*qurra'*); kwenye utaratibu, zaidi ya hayo, kuhakikisha usahihi wa kutumika, ‘wasambazaji’ wawili (*rawi*, pl. *ruwah*) walikuwa wanakubaliana mmoja na mwingine. Kutokana na matokeo hayo saba ya maandiko ya msingi (*al-qira'at as-sab'*, ‘maandiko saba’), kila moja lilikuwa na matoleo mawili yaliyosambazwa (*riwayatan*) pamoja na tofauti ndogo za kutamka, lakini yote yalibeba umakini mkubwa kwenye alama za vokali

na alama zingine za lazima kwenye lugha au lahaja.” (Glasse 2013: *Qira’ah*, 436)

“Maandiko” saba ya kikanuni au kisheria kila moja likiwa na “wasambazaji” wawili tofauti (yalifanya jumla ya matoleo 14 ya kikanuni au kisheria ya Korani) kwa kweli yalitumika kulinda njia tofauti zamuundo wa baadhi ya maneno yaliyotangulia, kama mwandishi wa Kiislamu Adil Salahi alivyosema, kila moja ya zile zilichogaguliwa na Ibn Mujahid zilikuwa “na mbinu tofauti ambazo zilielezwa kwa mapana sana na wanazuoni wa liofuata baaadaye kwenye maeneo mengi ya ulimwengu wa Uislamu” (Salahi 2001: n.p.). Hata hivyo, matoleo 14 ya kikanuni au kisheria ya Korani ya Kiarabu yote yako tofauti. Zaidi, maandiko matatu ya nyongeza, kwenye nyongeza yay ale saba ya Ibn Mujahid, pia yamekubaliwa kwa ujumla kama ya kikanuni au kisheria, yakileta jumla ya maandiko kumi ya Korani yaliyokubaliwa (Ali al Imam 1998: 128-29, 136-37). Lakini haya siyo yote. Muislamu Dr. Muhammad Roy Purwanto anaeleza, “Kwa kweli, zipo shule mbalimbali za kukariri Korani, ambazo zote upo uweundisha matamshi ya Uthmani [Maandiko ya maandishi ya Kiarabu]: Saba yaliyoaminika, matatu yaliyoruhusiwa na (angalau) manne yasiyo ya kikanuni–kwenye 8 ya tamaduni ndogo ndogo kila moja –*kufanya nukuu kuwa 80 zenye vigezo tofauti kabisa*” (Purwanto 2013: 3, fafanuzi imeongezwa). Kile hili linachokimaanisha ni kwamba Korani kama ilivyo leo imetokana na “wasomaji” mmbalimbali tofauti tofauti wa Kiarabu kwa njia tofauti ya “usambazaji.” Matoleo yaliyosambazwa *hayafanani*. Matoleo tofauti ni makuu kwenye sehemu tofauti za ulimwengu. (Angalia Green 2019: History; angalia pia Salahi 2001: n.p.)

Hata wasambazaji wawili wa toleo lilelile huleta matokeo kwenye mamia ya utofauti. Mwandishi Muislamu Adil Salahi anaeleza, “Ili kuelewa kiwango cha tofauti hizi, tumesema kwamba Aassim ibn Abi An-Najood alikuwa miongoni mwa wasomaji saba waliochaguliwa na Ibn Mujahid. Mbinu zake zimeelezwa kama zilivyofundishwa na wanafunzi wake wawili, Shubah na Hafs. . . . Watoa habari hawa wawili walitofautiana siyo chini ya mifano 520. Wote walikuwa na sifa sahihi kwa Aassim na kupitia yeye na waalimu wake kwa Nabii mwenyewe. Hizi ni tofauti ndani ya mbinu ile ile. Ni wazi, tofauti baina ya mbinu saba ni nyingi sana.” (Salahi 2001: n.p.) Samuel Green alilinganisha matoleo mawili tofauti ya Kiarabu: kwa kawaida Korani inayotumika sana, mwaka 1924 Toleo la kiwango la Wamisri msingi wake ulikuwa kwenye usambazaji wa toleo la Imam Hafs, na toleo la usambazaji wa Imam Warsh ambalo kwa kiwango kikubwa linatumika Afrika ya Kaskazini. Alizingatia aina nne za ytofauti baina ya Korani mbili—maneno ya ziada, tofauti kwenye silabi, nukta kwenye lahaja, na vokali—na kupata tofauti 1354 baina ya hizo (Green 2019: Idadi ya tofauti).

Ingawa Waislamu wanaweza kudai kwamba tofauti hizi ni “jambo la lugha au lahaja, au matamshi, na hayaathiri maana,” Green anaonyesha kwamba “hili kabisa haliwezi kuwa sababu. Mifano iliyotolewa awali inaonyesha kwamba tofauti ni za muhimu sana: hubadilisha somo la sentensi, ama kitenzi ni tendaji au ni batili, umoja au wingi, jinsi gani fasihi ya sentensi inavyotakiwa kueleweka.” (Ibid.: Kiwango ambacho tofauti zinaweza kuathiri maana) Muislamu Dr. Muhammad Roy Purwanto anathibitisha hili. Alitoa mifano ya Aya kumi ambapo “usomaji tofauti [qiraat] kwenye Korani unavyoweza kufanya maana tofauti ya Aya hizo. Kwenye hatima yake, hufanya mawazo tofauti kwenye hekima ya kisheria ya Kiislamu.” (Purwanto 2013: 5) Kiwango cha tatizo kineonyeshwa kwenye hili “Muhammad Fahd Khaaruun alikusanya maandiko tofauti yaliyokubaliwa miongoni mwa wasomaji kumi waliokubalika na kuyaweka kwenye mstari wa toleo la mwaka 1924 la kiwango la Wamisri la Korani la Hafs. Hizi siyo tofauti zote, zipo tofauti ambazo zaweza kuwa zingengezwa, lakini mwandishi alijizuia mwenyewe kwenye tofauti za Wasomi kumi waliokubalika. . . . Jumla ya idadi ya tofauti zilizoorodheshwa kwa sura zote . . . ni tofauti 10243.” (Green 2019: Linganisha Korani nyingi za Kiarabu)

5. Ayah Zilizokosekana kwenye Korani. Hadithi inafunua uhalisia wa baadhi ya aya ambazo zilikuwa sehemu ya Korani kama zilivyopokelewa na Mohamedi lakini hazipo kwenye Korani tuliyo nayo leo. Kwenye hadithi moja, Abu Yunus, mtumwa huru wa Aisha, mjane wa Mohamedi, alieleza, “Aisha aliniagiza kuandika nakala ya Korani kwa ajili yake na kusema: Wakati utakapoifikia Aya hii: ‘Linda maombi na maombi ya kati’ (ii. 238), nijulisha Mimi; hivyo wakati nilipoifikia, Nilimjulisha na aliniamuru kuandika (kama hivi): Linda maombi na maombi ya kati na maombi ya mchana, na kuwa mkweli na mwaminifu/mtiifu kwa Allah. Aisha alisema: Hivi ndivyo nilivyosikia kutoka kwa Mjumbe wa Allah.” (Muslim: 629; angalia pia Abi Dawud: 410; at-Tirmidhi: vol. 5, book 44, no. 2982)

Aisha alisimulia aya nyingine kwenye Korani ambayo kwa sasa inakosekana “Aisha (Allah apendezwe naye) alitaarifu kwamba ilifunuliwa kwenye Korani Takatifu kwamba watoto kumi wachanga kwa wazi walifanya ndoa kinyume cha sheria, baadaye iliondolewa (na kuwekewa mbadala) kwa watoto wachanga watano na ilikuwa kabla ya Mtume wa Allah kufa ilikuwepo kwenye Korani Takatifu (na kukaririwa na Uislamu).” (Muslim: 1444a) Gilchrist alieleza, “Ilielezwa wazi kwamba kiasili Korani ilikuwa na aya inayoelezea makatazo ya ndoa kwa watu wawili ambao wamenyonya ziwa la mwanamke mmoja yapata mara kumi. Aya hii baadaye iliondolewa na nyingine mbadala iliandikwa, kupunguza idadi na kuwa tano. Aya hii iko

wapi kwenye Korani? Hii pia inakosekana.” (Gilchrist 1989: ch.4.4)

Sura hizi zote zinaonekana kukosekana kwenye Korani. Abu Musa al-Ash’ari, mmoja wa wale walioidhinisha maandishi ya Korani wa kwanza na mshiriki wa karibu wa Mohamedi, alielezwa kusema kwa wasimulizi wa Basra, “Tulisimulia sura ambayo inafanana kwa urefu na kwa ukali wake kwa (sura) Bara’at [i.e., surah 9]. Hata hivyo nilikuwa nimeisahau hiyo kwa kuondolewa kwa ile ambayo niliikumbuka nje ya hiyo: ‘Kama yapo mabonde mawili yaliyojawa na utajiri kwa wana wa Adamu na akahitaji bonde la tatu, na hakuna kitakacholijaza tumbo la mwana wa Adamu isipokuwa ni vumbi.’ Na tulikuwa tunasimulia sura inayofanana na sura ya Musabbihat, na Niliisahau, lakini nikaikumbuka hii Zaidi ya ile: ‘Enyi watu mlioamini, kwanini mnasema kile ambacho hamkitendei kazi’ (Ixi 2.) na hilo limehifadhiwa shingoni mwako kama ushahidi (kinyume na wewe) na utaulizwa juu ya hilo siku ya Ufufuo’ (xvii. 13).” (Muslim: 1050) Sam Shamoun, ananukuu kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Uislamu, anaeleza juu ya vitu vingine vilivyokosekana na Aya zisizokamilika, ikijumuishwa na ukweli kwamba sura ya 33 inyo moja ya tatu ya idadi ya Aya asili iliyozibeba! (Shamoun, “Isiyokamilika na isiyofaat,” n.d.: n.p.; angalia al-Suyuti n.d.: Nasikh na Mansukh 13 [61/428]).

6. Maandiko mbadala ya Korani. Abdullah bin Mas’ud alikusanya Korani ambayo ilikuja “kupata kibali kama maandiko ya kiwango kwa Uislamu wa maeneo ya Kufa” (Gilchrist 1989: ch.3.1). Gilchrist anakumbusha kwamba “Ibn Abi Dawud aliandika siyo chini ya kurasa kumi na tisa za kazi ya kukusanya maandiko ya Korani kwenye vitabu mbalimbali vilivyopatika baina ya maandiko yake yeye Mas’ud na yale ya Zaid ambayo wakati wote ndiyo yaliyochukuliwa kama ya kiwango na Uthman” (Ibid., nukuu ya Ibn Abi Dawud, *Kitab al-Masahif*, pp. 54-73). Makusanyo ya Korani ya Mas’ud yale yaliyoteketezwa na Uthman. Jefferey anazo kurasa 89 za maandiko tofauti baina ya ujumbe wa Mas’ud na marudio ya Uthman (Jeffery 1937:25-113). Zaidi, “yapo *matukio* ambayo siyo chini ya 149 kwenye sura 2 *pekee* ambayo maandiko yake yanatofautiana na mengine kwenye mtiririko.” (Gilchrist n.d.: ch.4, fafanuzi imeongezwa). Hakika, kiwango cha maandiko tofauti kwenye uandishi wa Kikorani iliyokuwepo wakati wa marudio ya Uthman yanajaza takriban kurasa 330 za bidhaa za Jeffery kwa historia ya maandishi ya Korani! Haishangazi kwanini Uthman aliagiza nyingine zote isipokuwa iliyo yake kuteketezwa.

Tofauti miongoni mwa maandiko ya Kikorani yalieleweka vema kwa Wanazuoni wa Kiislamu. Abu al-Faraj Muhammad ibn Ishaq al-Nadim (d. AD 995) aliandika kitabu chake (*al-Fihrist*) Orodha ambacho ni mkusanyiko wa ujuzi na fasihi za karne ya kumi ya Uislamu akipitia takriban vitabu 10,000 na maandishi 2,000, pamoja na kina cha bibliografia na upinzani wa fasihi. Kitabu cha al-Nadim kina sehemu zote zilizoorodheshwa “Vitabu vinavyojumuisha kutofautiana kwa maandiko ya [Kikorani].” Sehemu hiyo imeorodheshwa vitabu vifuatavyo ambavyo baadaye vilikuwepo ambavyo vilihifadhi maelfu ya kumbukumbu zilizotofautiana miongoni mwa matoleo tofauti ya Korani:

- Tofauti baina ya maandiko ya Watu wa al-Madinah, al-Kufah, na al-Basrah kulingana na al-*Kisa’i*;
- Kitabu cha *Khalaf*, Kutofautiana kwa maandiko;
- Kutofautiana kwa Watu wa al-Kufah, al-Basrah, na Syria kuhusiana na maandiko ya, *al-Farra*;
- Kutofautiana baina ya Maandiko ya Abu Da’ud al-*Sijistani*;
- Kitabu cha al-*Mada’ini* kuhusu tofauti baina ya maandiko na ukusanywaji wa Korani;
- Kutofautiana baina ya Maandiko ya Syria, al-Hijaz, na al-Iraq, ya Ibn Amir al-Yahsubi;
- Kitabu cha Mohamedi ibn Abd al-Rahman al-*Isbahani* kuhusu kutofautiana kwa Maandiko. (Ibid.: 79)

Madai ya Muislamu kwamba Korani imehifadhiwa kamilifu, halisi kama ambavyo ilifunuliwa kwa Mohamedi, hayana msingi wowote wala ukweli wa kihistoria. Hili limekuwa wazi kimsingi kutokana na vyanzo vya Kiislamu vyenyewe. Kutoka kwenye vyanzo vya kihistoria vya Uislamu tunazijua tofauti hizi za Korani zilizokuwepo wakati wa Mohamedi na kufuatiwa na kifo chake. Ingawa Uthman alijaribu kuiweka Korani kwenye viwango, mnyororo una nguvu tu kwa kiasi cha udhaifu wa viungio vyake. “Maunganisho dhaifu kwenye mnyororo wa historia ya maandishi ya Korani hasa kwenye ukweli ambao, siku zile muhimu za mwanzo, tofauti na utofauti wa maandiko ya Korani yaliyokuwepo na ushahidi mwingine uliotolewa kwamba maandiko ya mwisho yaliyopewa viwango kama yaliyo bora kuliko mengine hayakuwa yamekamilika au kwa njia yeyote kuwa makamilifu.” (Gilchrist n.d.: ch.4) Hatimaye, Maandiko kumi yanaotambuliwa yalioanzishwa na Ibn Mujahid yanasema kwamba Korani zote zilizopo duniani leo *hazifanani*. Badala yake, zimejawa na maelfu ya utofauti, mengi yake huathiri kiini na maana ya Korani yenyewe.

VII. Mkanganviko na makosa kwenye Korani

Uislamu wanang’ang’ana kwamba Korani imetoka kwa Allah na haina kosa lolote (angalia, e.g., **Q. 15:9; 26:192-93; 56:77-80**). Uislamu waaminifu “wanapaswa kuonekana kama *kafir* [wasioamini] mtu ambaye atakataa hata neno moja tu la maandiko ya Korani, au atakayeongeza chochote kwenye Korani au kuondoa chochote ndani ya Korani” (al-Athari 2005: 97). Korani yenyewe inasema, “*Je, hawaitafakari Korani? Na kama*

ingalitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wanalikuta ndani yake hitilafu nyingi. (Q. 4:82, Hilali-Khan) “Kulingana na Aya hii, kama ‘mkanganyiko mwingine’ ungeonekana kwenye Korani, ingethibitisha kwamba *haikutoka* kwa Mungu” (Sundiata 2006: 80-81, fafanuzi imeongezwa). Kwa kweli Korani imejawa na mikanganyiko mwingi na makosa kibao. Vyanzo vimeorodhesha “Mkanganyiko kwenye Korani” (angalia Bibliography) imeorodhesha zaidi ya mikanganyiko ya ndani pekee 120, kama yalivyo mengi ya Kihistoria, Kisayansi, Kweli, Kifasihi, na makosa ya Kibiblia. Hili linajumuisha yote, mambo madogo na makubwa yanayougusa moyo wa Uislamu. Kwa uchache, lakini siyo kwa maana yote, ya mikanganyiko hii na makosa yametazamwa hapa chini.

A. Mikanganyiko

Ipo mikanganyiko mingi ya ndani ya Korani. Baadhi ya hiyo ni jinsi ambavyo Korani inajihusisha na mitazamo ya dhambi, Wokovu, hukumu, na asili ya Allah ambayo tulijadili hapo awali. Mengine machache ambayo yanaugusa moyo wa Imani ya Kiislamu na maadili ni haya yafuatayo:

- Shetani ni nini? Shetani ameelezwa kama malaika kwenye Q. 2:34; 7:11; 15:28-31; 20:116; 38:71-74. Penginepo, ameelezwa ka Jini kwenye Q. 18:50. Majini yameumbwa kutoka motoni (Q. 15:27; 55:15), na Shetani (Ibilisi) ameelezwa mwenyewe kwamba aliumbwa kutoka kwenye moto (Q. 7:12; 38:76). Kama yeye ni malaika, hili litakanganya Q. 66:6 ambayo inasema kwamba malaika “wenye nguvu, hawamwasi Mwenyezi Mungu Aliyowaamuru, na hutenda wanayoamrisha.”
- Wakristo: marafiki au maadui; wema au wabaya? Q. 5:82 inasema, “*Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu (wengine) kwa waaminio ni Mayahudi na walio washirikina; na utawaona walio karibu zaidi kwa urafiki na waaminio ni Wale wanaosema ya kuwa ‘sisi ni Wakristo’: hayo ni kwa sababu wako miongoni mwa Makasisi na Maruhubani, na kwa sababu wao hawatakabari.*” Q. 57:27 inaongeza, “*Tukamfuatisha Isa bin Mariamu na Tukampa Injili; na Tukauweka upole na rehema katika mioyo ya wale waliomfuata.*” Q. 3:55 inasema, “(Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: *Ewe Isa! Kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka Siku ya Kiyama.*”

Kwa maana nyingine, tathmini kinyume kwa Wakristo inapatikana kwenye Q. 5:51: “*Enyi mlioamini msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki; wao kwa wao ni marafiki.*” Q. 98:6 (Hilali-Khan) anaenda mbali Zaidi kwa kusema, “*Bila shaka wale waliokufuru (katika dini ya Uislamu, Korani na Nabii Mohamedi) miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina wamo katika moto wa Jahanamu, watakaa humo; hao ni waovu kabisa kushinda viumbe vyote.*”

- Wajumbe na Waonyaji walitumwa kwa kila mtu? Q. 10:47 inasema, “*Na kila umati una Mtume: basi anapofika Mtume wao inahukumiwa baina yao kwa adili nao hawadhulumiwi.*” Q. 35:24 inaongeza, “*Bila shaka Sisi Tumekutuma kwa haki ili ubashiri na kuonya, na hakuna taifa lo lote ila alipita humo Mwonyaji.*” Q. 19:54-55 kwa uhakika inaeleza kwamba Ishmael alikuwa mjumbe/mtume kwa watu wake (i.e., Waarabu). Q. 2:125-29 hata hivyo inasema kwamba Ibrahimu na Ishmael ndio waasisi wa Kab’ah!

Moja kwa moja inaikanganya hii, Q. 28:46-47 mwambie Mohamedi, “*Wala hukuwa upande wa mlima Tuliponadi, lakini (kutumwa kwako) ni rehema ya Mola wako, ili uwaonye watu wasiofikiwa na mwonyaji kabla yako, huenda watakumbuka. Na kwa nini msiba unapowafikia kutokana na vitendo vyao wenyewe hawasemi: Mola wetu, kwa nini Hukutuletea Mtume Wako ili tuweze kuzifuata Aya Zako na kuwa miongoni mwa walioamini?*” (angalia pia Q. 32:3; 36:3-6)

- Chakula cha Kuzimu. Q. 69:36 (Hilali-Khan) anasema na watu wa Jehanamu, “*Wala chakula cho chote ila uoshaji wa vidonda.*” Inaikanganya hii, Q. 88:6 (Hilali-Khan) inasema, “*Hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miiba.*” Inazikanganya aya zote hizi, Q. 37:62-68 (Hilali-Khan) anasema, “*Je, karibisho la namna hii (Paradiso) ni bora au mti wa zakkum (Mti ulio ulio mbaya Zaidi huko kuzimu)? Kwa yakini Sisi Tumeufanya jaribio kwa wadhalimu. Hakika huo ni mti uotao katikati ya Jahanamu. Matunda yake ni kama vichwa vya nyoka. Bila shaka wao watakula katika huo, na kwa huo watajaza matumbo. Kisha bila shaka watapewa juu ya huo mchanganyiko wa maji ya moto.*” (angalia pia Q. 56:52)

- Mwanadamu aliumbwa kutokana na nini? “*Soma! kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Alimwumba mwanadamu kwa tone la damu iliyoganda*” (Q. 96:1-2, Hilali-Khan); “*Amemwumba mwanadamu kwa tone la manii*” (Q. 16:4); “*Naye ndiye Aliyemwumba mwanadamu kwa maji,*” (Q. 25:54); “*Na bila shaka Tulimwumba mwanadamu kwa udongo utoao sauti, kwa matope meusi yaliyobumbwa*” (Q. 15:26, Hilali-Khan; angalia pia Q. 55:14); “*Na katika Ishara Zake ni hii ya kwamba Amewaumbeni kwa udongo, kisha mmekuwa watu mnaoenea*” (Q. 30:20); “*Je, mwanadamu hakumbuki ya kwamba Tulimwumba kabla hali hakuwa cho chote?*” (Q. 19:67). “Hakuna kiashiria kwamba aya hizi zimepewa ‘baadhi ya vikolezo tu’. Hazisomeki kwa njia hii. Kamwe hazisemi: ‘Tulimwumba mtu kutoka kwenye udongo miongoni mwa vitu

vingine’.” (“Mkanganyiko wa Korani” n.d.: n.p., fafanuzi yenye msisitizo kwenye asili)

- **Yona: alitupwa au hakutupwa ufukweni? Q. 37:145** inamzungumzia Yona, “*Lakini Tukamtupa ufukoni hali yu mgonjwa.*” **Q. 68:49** inapingana nah ii kwa kusema, “*Kama isingalimfikia neema kutoka kwa Mola wake, bila shaka angalitupwa ufukoni na hali yu mwenye kulaumiwa.*”
- **Kipi kiliumbwa kwanza: mbingu au Nchi? Q. 2:29** (Sahih) inasema, “*Yeye ndiye Aliyewaumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, tena Akaelekea kwenye mbingu na Akazitengeneza sawasawa mbingu saba, naye ndiye ajuaye kila kitu.*” **Q. 79:27-30** (Sahih) inatupa uhalisia wa kupingana kwa amri ya matukio: “*Je, ninyi ni wenye umbo gumu zaidi au mbingu? Yeye Aliijenga. Akaiinua kimo chake na Akaitengeneza vizuri, Na Akautia giza usiku wake, na Akautokeza mchana wake; Na ardhi baada ya hayo Akaitanua.*”

B. Makosa

Korani pia imejawa na makosa mengi sana: makosa ya kihistoria, makosa ya kisayansi, makosa ya Kiukweli, makosa ya kifasihi, na makosa ya Kibiblia (i.e., wakati inapozungumzia kitu kwenye Biblia huvichanganya vitu au vinginevyo huvipotosha). Orodha ya vyanzo “Korani na Sayansi” (“Qur’an and Science” n.d.) na kitabu cha Dr. William Campbell kitiwacho *Korani na Biblia kwenye mwanga wa Historia na Sayansi* (Campbell 2002), miongoni mwa vyanzo vingine, kimejhusisha na makosa haya. Kwa uchache, lakini siyo yote, ya historia ya Korani, Kisayansi, Kibiblia, na makosa ya kweli kama yafuatavyo:

- **Jua huzama wapi? Q. 18:83-86** inasema, “*Na wanakuuliza habari za DhulKarnain. Sema: Kwa yakini nitawasomeeni katika hadithi yake. Bila shaka Tulimwimarisha katika ardhi, na Tukampa njia za kupatia kila kitu. Ndipo akaiifuata njia. Mpaka alipofika machweo ya jua akaliona linatua katika chemchem iliyovurugika, na pale akawakuta watu, Tukasema: Ewe Dhul-Karnain, Uwaadhibu au uwafanyie wema.*”
- **Safari ya kuuendelea msikiti ambao wala haupo. Q. 17:1** (Sarwar) inasema, “*Utukufu ni wa Yule Ambaye Alimpeleka mtumishi wake usiku kutoka msikiti Mtakatifu (ulioko Maka) mpaka Msikiti wa mbali (ulioko Yerusalemu) ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili Tumwonyeshe baadhi ya Ishara Zetu. Hakika Yeye peke Yake Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona.*” Safari hii maarufu ya usiku ya Mohamedi ilikuwa ya kwenda Msikiti wa Al-Aqsa ulioko Yerusalemu imethibitishwa kwenye tafsiri ya Sahih, Hilali-Khan, Haleem, na Asad. Hata hivyo, Robert Spencer anavyoonyesha, “Hapakuwa na Msikiti Yerusalemu wakati ule” (Spencer 2009: 129). “Msikiti wa asili ulikuwa kijumba kidogo cha maombi kilichoandaliwa na Umar, Khalifa wa pili,” lakini hata hili halikuanza mpaka baada ya miaka kadhaa baada ya Mohamedi kufa (“Msikiti wa Al-Aqsa” 2019: Utangulizi; “Umar” 2019: Aliutembelea Yerusalemu mwaka 637 CE; angalia pia “Msikiti wa mbali sana?” n.d.).
- **Hakuna mtu aliyeitwa Yohana? Q. 19:7** (Hilali-Khan) anamwelezea Yohana mbatizaji, “*Ewe Zakaria! Hakika Tunakupua habari njema ya mtoto, jina lake Yahya (Yohana): Hatujafanya kabla aliye sawa naye .*” Kiarabu Yahya ni sawa na Kiebrania Johanan na Kigiriki Ioannes, ambalo ni sawa na kwa Kiingereza John na Kiswahili Yohana. Kwa hakika, “ipo mifano 27 ya jina Yohana ambayo imetajwa kwenye Agano la Kale. . . . Yohana wote hawa waliishi kabla ya Yohana mbatizaji. Kwa hakika Yohana lilikuwa jina la kawaida sana.” (“John the Baptist” n.d.: n.p.)
- **Manii na maendeleo mabaya? Q. 16:4** inasema, “*Amemwumba mwanadamu kwa tone la manii.*” **Q. 86:5-7** inasema, “*Basi mtu ajitazame ameumbwa kwa kitu gani, Ameumbwa kwa maji yaendayo kasi, Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo (Kiarabu-sulb) na mbavu (Kiarabu- tara’ib).* Ingawa Korani inataja Manii, kwa uwazi inaacha kutaja seli za yai zinazotolewa na mwanamke kwa kuwa zilikuwa hazijagundulika mpaka baada ya miaka mamia baada ya wakati wa Mohamedi (“Egg cell” 2019: History). Maelezo ya Korani kuhusiana na Manii ni “kulingana na uelewa wa zamani kwamba fetusi huendelezwa kwa ujumla wake kutoka kwenye ‘mbegu’ ya mwanaume mara tu mbegu hiyo inapopandwa kwenye tumbo la mwanamke (Spencer 2009: 175). Zaidi, Dr. William Campbell anakumbusha: “Kwa kuwa aya inazungumzia hali ya uzalishaji wa utu uzima isingezungumzia kuhusiana na wakati wa maendeleo ya kiinitete. Zaidi ya hayo, kwa kuwa ‘sulb’ hutumika kwa ushirikiano na ‘kumeza maji’ jambo ambalo laweza kuwa la mwilini tu na ‘tara’ib’ ambalo pia ni neno linalohusiana na mwili kwa maana ya kifua au mbavu, usingekuwa ufumbuzi. **Kwa hiyo, tumeachwa na tatizo la uhakika kwamba manii zinatoka mgongoni au kwenye maeneo ya figo na siyo kwenye kokwa za mwanaume.**” (Campbell 2002: sec.4.II.B.5, fafanuzi nzito kwenye asili.) Kwa nyongeza, **Q. 96:1-2** inasema, “*Soma (au tangaza) kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Alimwumba mwanadamu kwa tone (dogo) la damu iliyoganda.*” Dr. Campbell anaonyesha kwamba, kama suala la ukweli wa kisayansi, “hakuna hatua ya done wakati wa kuundwa kwa kiinitete kwa hiyo hili ni kosa kubwa la kisayansi” (Ibid.: sec. 4.II.B.6). **Q. 23:14** inaendelea kuelezea mpangilio wa kudhaniwa wa maendeleo ya kiinitete: “*Kisha Tukaiumba mbegu kuwa pande la damu, na Tukaumba pande la damu kuwa pande la nyama, kasha Tukaumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama,*

kisha Tukaifanya kiumbe kingine. Basi mwenye mibaraka ni Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbao.”

Nabeel Qureshi alipokea shahada yake ya udaktari na kusema, “Kiinitete hakiwi kwanza mifupa ili baadaye kifunikwe na nyama. Safu moja ya kiinitete, safu ya katikati ya misuli, hutofautisha baina ya mifupa na nyama kwa wakati ule ule.” (Qureshi 2016: 234) Hivyo, Korani haiwezekani kuuwa imetoka kwa Mungu, kwa kuwa Mungu anajua shahawa zinatoka wapi na anajua usahihi wa ukuaji wa kiinitete.

• “Kuthibitisha Biblia? **Q. 5:48** inasema, “*Na Tumekuteremsha Kitabu kwa haki, kinachosadikidha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu, na kukihifadhi, basi uwahukumu baina yao kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao kwa kuacha haki iliyokufikia.*” Kifungu kingine sawa na hicho kinaeleza kwamba Korani inathibitisha ufunuo wa awali wa Biblia (angalia **Q. 2:41, 89, 97; 3:3; 4:47; 5:15, 48; 6:90, 92; 10:37; 12:111; 35:31; 41:43; 46:9, 12, 30**). Tumekwisha kuona maeneo mengi muhimu (madai kwamba Mariamu, mama yake na Yesu, alikuwa Dada yake na Musa; Kusulubiwa; kufufuka; Yesu kama Mwana wa Mungu; madai kwamba Mohamedi alitabiriwa kwenye Biblia) ambayo Korani haijaweza kuyathibitisha, lakini inashindana na Biblia. Jambo jingine la wazi lilikuwa kwamba Korani “haikuithibitisha Biblia” ikiwa ni pamoja na:

(a) **Mwanzo 5:32-7:23; 8:18** inasema kwamba Nuhu alikuwa na wana watatu, wote waliingia pamoja naye kwenye safina, na waliokolewa wote wakati wa gharika; **Q. 11:42-43** inasema kwamba Nuhu alikuwa na mtoto mmoja ambaye alizama kwenye gharika.

(b) **Mwanzo 8:4** inasema kwamba safina ilikuja kutulia kwenye mlima wa Ararati; **Q. 11:44** inasema kwamba safina kwenye mlima wa Judi.

(c) **Mwanzo 11:26** inasema kwamba baba wa Ibrahim aliitwa Tera; **Q. 6:74** inasema kwamba baba wa Ibrahim aliitwa Azar.

(d) **Kut 2:1-10** inasema kwamba Musa aliasiliwa na Binti yake na Fara; **Q. 28:7-9** inasema kwamba Musa aliasiliwa na Fara pamoja na mke wake.

(e) Kulingana na Biblia, Musa alikuwa nabii wa kwanza wa Israeli (**Kut 3:10; Hes 12:2-8; Kumb 18:15**) na Sauli (ambaye alikuja kuishi miaka mamia mengi baada ya Musa) alikuwa Mfalme wa kwanza wa Israeli (**1 Sam 9:15-17**); kinyume na ukweli huu, **Q. 5:20** inaye Musa akiwaambia Waisraeli, “*Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowafanya Manabii kati yenu na Akawafanyeni wafalme, na Akawapeni ambayo Hakuwapa wo wote ulimwenguni kote.*”

Biblia ilikuja ya kwanza, na Korani inalitambua hilo na msimamo baina yake na Biblia kama uthibitisho kwamba pia imetoka kwa Mungu. Kwa hiyo, Kimsingi, kama hizi mbili zinapingana basi Korani siyo Biblia, ina makosa, kwa sababu Korani imejengea msingi wa madai yake kwenye Biblia na inadai kuthibitisha kile ambacho tayari kipo kwenye Biblia. Sundiata anahitimisha na matokeo muhimu ya hili: “Kama Korani haipo moja kwa moja kuhusiana na mambo ya wazi ya vitu vya ulimwengu huu ambavyo twaweza kuvithibitisha, tutaiaminije wakati inapozungumzia vitu ambavyo haviwezi kuthibitishwa kinadharia (kisayansi)?” (Sundiata 2006: 35)

VIII. Fundisho la Kuondolewa

Moja ya njia ambayo Korani na Uislamu hujaribu kushughulikia nayo mapungufu yaliyopo kwenye Korani na mkanganyiko wa ndani kwa ndani yake yenyewe ni fundisho la “kuondolewa,” ilijulikanalo kama “*al-Nasikh wal-Mansoukh*” (Mwondoaji na yaliyoondolewa). Kuondolewa kuna maanisha kwamba “ni kwenye ile hali ambayo aya zinapojikanganya moja na nyingine, aya za awali hupewa kipaumbele kuliko zile aya zilizofuatia. Mfuatano wa muda wa aya ipi iliandikwa na lini huamuliwa na mamlaka yake iliyoanzisha kanuni ndani ya Uislamu.” (Al-Araby n.d.: utangulizi)¹⁷ Fundisho hili lina msingi wa kweli kwenye aya za Kikorani: **Q. 2:106** inasema, “*Aya yo yote Tunayoifuta au kuisahaulisha Tunaleta iliyo bora kuliko ile au iliyo mfano wake: Je, hujui kwamba Mwenyezi Mungu Anao uwezo juu ya kila kitu?*” (Angalia pia **Q. 13:38-39; 16:101**) Fundisho la kuondolewa/kufutwa limetengeneza tatizo kubwa kwa Uislamu. Matatizo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

A. Fundisho la kuondolewa linapingana na maeneo mengine kwenye Korani na kuushambulia moja kwa

¹⁷ Angalia **NYONGEZA A—MPANGILIO WA KIJIOLOGIA WA SURA**. Sundiata anaonyesha kwamba “kwa kuzingatia hila hii [fundisho la kuondolewa/kufutwa] kwa kujihusisha na suala la kujikanganya kwenye Korani, Uislamu kwa njia isiyo ya moja kwa moja wanakiri kwamba Korani imejikanganya yenyewe, ingawaje Korani inasema kwamba uwepo wa mkanganyiko kwenye kurasa zake usifanyiwe kazi kwa madai ya Uungu wake” (Sundiata 2006: 82-83).

moja unyofu wa Allah

Korani inathibitisha kwamba, njia na neno la Allah havibadiliki: “*Na hakuna abadilishaye maneno ya Mwenyezi Mungu.*” (Q. 6:34); “*Na limetimia neno la Mola wako kwa kweli na uadilifu: Hakuna awezaye kuyabadilisha maneno Yake: na Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.*” (Q. 6:115; angalia pia Q. 10:64; 18:27). Aya za kuondolewa/kufutwa zenyewe zinazikanganya aya zisemazo neno la Allah haliwezi kubadilishwa. Hili moja kwa moja linaathiri unyofu wa Allah na kukubalika kwake, kwa sababu “kulinganisha na madai ya Kikorani kwamba njia za Allah hazibadiliki na ukweli kwamba anaweza kubadilisha ufunuo, ni lazima tudhani kwamba njia za Allah huwa zimetofautiana” (Sundiata 2006: 85). Hili moja kwa moja linadhoofisha madai kwamba Korani neno halisi la Allah, linadumu milele kwenye kibao kule mbinguni (Q. 85:21-22). Ni kwa jinsi gani linaweza kudumu milele mbinguni wakati limejawa na vifungu vilivyoondolewa?

B. Fundisho la kuondolewa linaifanya Korani isieleweke kwa mapana

“Idadi ya aya zilizoondolewa/kufutwa zimekuwa ziktofautiana zikikisiwa kuwa kati ya tano hadi mia tano” (Hughes 1895: 520). “Jalalu’ d-Din kwenye *Itqan* yake anatupa orodha ya aya ishirini ambazo zinatambuliwa na Wachambuzi wote kuwa ziliondolewa/futwa” (Ibid.). Ahadithi zinaorodhesha aya nyingi au sehemu ya aya ambazo zilikuwa zimeondolewa (angalia al-Bukhari: 1917, 2801, 4990, vol. 6, book 60, no. 33, 34, 53, 54, 60, 68, 69, 100, 285, 288; Muslim: 125, 630, 677a, 1145a, 3023e; Abi Dawud: 1304, 2282, 2771, 2817, 2921, 2922, 2924, 3590, 4111, 4413, 5016; an-Nasa’i: 2316, 3307, 3531, 3543, 3544, 3554, 4001, 4069, 4865; Ibn Majah: 2365, vol. 3, book 9, no. 1942, 1944; at-Tirmidhi: 798, 1568). Muislamu wa awali Anwarul Haqq, kwenye kitabu chake kiitwacho *Kuondolewa/kufutwa kwenye Korani*, aliorodhesha zaidi ya aya 250 ambazo zilikuwa zimeondolewa/kufutwa na zile zilizoiondoa/futa (Haqq 1926: 10-77). Al-Araby, ananukuu “moja ya kitabu cha kumbukumbu za jadi za Uislamu ni kilichoandikwa kwa lugha ya Kiarabu,” *al-Nasikh wal-Mansoukh* (Mwondoaji/aliyefuta na kile kilichofutwa/ondolewa) kwa Abil-Kasim Hibat-Allah Ibn-Salama Abi-Nasr, anaeleza: “Kati ya sura 14 za Korani, zipo sura 43 tu ambazo hazikuathiriwa na wazo hilo. Matokeo yapo wazi sana. Hii linamaanisha kwamba wale watakaohamasishwa kuikubali Korani kama ya kuaminika wanaweza kuchukua sura 43 tu za Korani kuwa za thamani machoni pao. Nyingi ya sura zake haziwezi kuchukuliwa kama zenye thamani. Aya zilizofutwa zimechanganywa pamoja na aya za kimamlaka na ni wanazuoni wa Kiislamu tu wanaoweza kujua ipi ni ipi.” (Al-Araby n.d.: Fundisho la Mwondoaji na Kile kilichoondolewa) Tatizo ni kwamba hakuna mfanano unaotambulika na orodha inayokubalika ya aya zipi zilizokuwa zimeondolewa/futwa na zile zilizoiondoa/futa. Vivyo hivyo, hakuna mtu anayeweza kuwa na uhakika ni amri au katazo lipi ambalo bado linafanya kazi. Tatizo moja ni kwamba nyingi ya aya zilizoondolewa/futwa zilibaki kwenye Korani. Hili linafanya ugumu Zaidi kuamua ni aya ipi ambayo iliondolewa/futwa na aya ipi ilifanywa mbadala.

C. Fundisho la kuondolewa lina madhara makubwa kwa kila anayedai kuwa Uislamu ni “dini ya amani”

Q. 9:5 inajulikana kama “Aya ya Upanga”: “*Na miezi mitakatifu itakapopita, basi waueni washirikina po pote mwakutapo, na wakamateni na wahusuruni na waoteeni katika kila maoteo. Lakini wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, basi iacheni njia yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehevu.*”

Q. 9:29 inajulikana kama “Aya ya mapigano”: “*Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya mwisho wala hawaharimishi Alivyoviharimisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa mikono yao wenyewe hali wakitii na wakubali kwamba wako chini ya utawala.*” Mahmoud Ayoub anaonyesha kwamba sura ya 9 ya Korani, ambayo imejawa na aya za Upanga na Kupigana, “ilikuwa ni miongoni mwa sura za mwisho Korani kufunuliwa. Inayofafanuliwa mara moja na kwa uhusiano wote baina ya kuimarishwa kwa jamii ya Uislamu na kunyenyekeana na wale ambao siyo Uislamu. Kwa hiyo wanasheria walichukulia sheria iliyojulikana kwenye sura hii kuondoa maagizo yote ya awali.” (Ayoub 1986: 9)

Hili lina matokeo ya kina. Maelezo ya chini ya Haqq’s *Yaliyoondolewa kwenye Korani* anaeleza, “*An-Nāsikh-wal-Mansūkh*, kwa Ibn Khuzyamh, inaeleza Aya 113 ziliondolewa kwa aya za upanga (9:5), na aya ya 9 iliondolewa kwa aya ya mapambano (9:29)” (Haqq 1926: 10n.1). Al-Araby inasema, “Zipo aya 124 ambazo zinasisitiza uvumilivu ambazo zilikuwa zimeondolewa/futwa na kubadilishwa kwa . . . Aya za Upanga” (Al-Araby n.d.: Aya za upanga). Mchambuzi wa Kiislamu As-Suyuti anaeleza juu ya Q. 9:5, “Hii ni *Ayat* ya upanga ambayo iliondoa msamaha, suluhu na kutafakari kwa kina” (as-Suyuti n.d.: Q.9:5, maoni). Vivyo hivyo, Fouda, Taha, na Al Akkad wanaitimisha kwamba “hakuna mtu anayelazimishwa kuamini kwamba Korani inasisitiza Amani kwa sababu aya zote hizi za “Amani” zimeorodheshwa ndani yake. Yote hayo yaliondolewa baada ya wanazuoni wote wa Uislamu kuthibitisha.” (Fouha, Taha, Al Akkad n.d.: 137) Ikiwa hiyo ndiyo sababu, basi karibia kila aya kwenye Korani ambayo hutoa mafundisho ya “Amani” na “uvumilivu” yaliondolewa kwenye Korani. Hili pia linamaanisha kwamba ISIS na Magaidi wengine wa Kiislamu wapo

sahihi sana wakati wanapojihesabia haki kwa ugaidi wao kwa kunukuu Korani.

D. Matatizo mengine ya fundisho la kuondolewa

Baadhi ya Uislamu wa sasa wanadai kwamba Korani iliifuta Biblia. Kitengo cha utafiti cha na uchapishaji cha Darussalam, kilichopo Riyadh, Saudi Arabia kinaeleza kwamba Allah “alimtuma Nabii Mohamedi kama wa mwisho kati ya Wajumbe na Manabii na kuvifuta/kuviondoa vitabu vyote vilivyoitangulia Korani” (Darussalam 2002b: 333). Athari sawa na hilo anasema mambo makuu kwenye vitabu vya Allah ni “*Tawrat, Injili* na Korani, na kilicho kikuu na bora ya hivi vitatu, ambacho kilivifuta hivyo vingine ni Korani” (al-Athari 2005: 93). Kama tulivyojadili hapo juu, Korani isingeweza kuiondoa Biblia kwa sababu kwenye maeneo mengi ndani yake na Mohamedi kwa uhakika alithibitisha kuaminika kwa Biblia. Muislamu wa awali Farooq Ibrahim anaonyesha kwamba wazo kwamba Korani iliiondoa Biblia halina mashiko: “Kama nilivyoangalia kwenye ushahidi kuhusiana na suala hili, Sikuona mahali kwenye Korani ambapo kufutwa/kuondolewa kulijadiliwa kwa kumbukumbu ya vitabu (kitab) vya manabii waliotangulia, lakini ni aya tu, ambazo zinamaanisha ‘ishara.’ Kimsingi wakati kumbukumbu zinapowekwa kwenye Korani kuzungumzia maandiko ya Wayahudi na Wakristo neno linalotumika ni vitabu (kitab), au hasa Torati na Injili, au maaandiko yaliyotolewa kwa Musa au Yesu. Sijaipata aya hiyo kama ipo kwenye Korani inayoelezea kwamba vitabu hivyo viliondolewa/futwa.” (Ibrahim n.d.: n.p.) Gilchrist anaongeza, “Kwenye sura 2:106 maandiko hayasemi tu kwa habari ya Ufu wa Allah kuondolewa/futwa lakini pia kuwa ulisahauliwa kwa nguvu zake – hili lingekuwa gumu kutaja maandiko ya nyuma ambayo yalikuwa yanaeleweka vema na kuhifadhiwa kunakoeleweka duniani kote kwa maelfu ya machapisho. Ingekuwa inazitaja tu aya halisi za Korani ambazo zilikuja kupuuzwa na kusahauliwa na Mohamedi na washiriki wake kwa nyakati.” (Gilchrist 1995: ch.1.4-Nadharia ya kuondolewa kwenye Korani)

Hatimaye, Sunnah (maisha binafsi ya Mohamedi) inavyoonekana *yanaweza kuiondoa na kuishinda hata Korani yenyewe*. Korani kama ilivyo haiagizi kumpiga kwa mawe hata kuua kama adhabu kwa mzinzi (angalia **Q. 4:15-16; 24:2**). Hata hivyo, Hadithi inafunua kwamba Mohamedi ndiye aliyeianzisha na kuitendea kazi adhabu ya kupiga watu kwa mawe hadi kufa kama adhabu ya kujamiiiana kusikokuwa kwa kisheria (nje ya ndoa), zoezi ambalo hufuatwa na baadhi ya nchi za Kiislamu hadi leo (angalia al-Bukhari: 6829, 6830). Tukio jingine, aliagiza wanaume waliohusika kuchapwa viboko (mia moja) 100 na kupigwa mawe hadi kufa kwa wanawake husika (al-Bukhari: 6827, 6828).

Kweli hizi zinatengeneza tatizo la kutisha la Kitheolojia: fasihi ya hadithi ni kubwa kiasi kwamba haiwezekani kujua ni maneno yapi ya Mohamedi na matendo yapi yaliyoyaondoa/futa mengine, aya zipi za Kikorani na ipi miongoni mwa hadithi zake iliiondoa/futa ahadithi ipi nyingine. Uislamu wanapaswa kumheshimu Mohamedi kama vile wanavyomheshimu Allah mwenyewe (**Q. 4:80**). Kwa hiyo, ni lazima wajue ni nini cha kutii na ni nini kilichoondolewa/futwa—bado fundisho la kuondolewa/futwa linafanya hayo yasiwezekane kutendewa kazi.

IX. Biblia na Korani: Hitimisho

Wakati Muislamu Ahmed Ali Haile alipoanza kujifunza Biblia aligundua kwamba inaelezea simulizi ya “mchezo wa ukombozi ulioanza na Adamu na Hawa Bustanini (Mwanzo 1-3) na kuishia na matumizi kwenye nyakati za mwisho, kwenye mji wa mbinguni ambao Mungu anaujenga (Ufu 21-22). Tofauti na Korani, siyo historia; ni maelekezo ya nini watu wanapaswa kuamini na kufanya. Kuna baadhi ya kumbukumbu za hila kwenye Korani, lakini haina muunganiko wa historia ya Wokovu kama ilivyo Biblia.” (Haile 2011: 56)

Wakristo wanalitambua hilo, hasa kwa sababu Biblia ni maktaba yenye “vitabu 66” inashirikisha maandishi wengi na iliandikwa kwenye desturi tofauti na maeneo tofauti ya Kihistoria. Kwa hiyo, kuelewa na kuitumia Biblia kwa usahihi na vizuri, Wakristo hujaribu wawezavyo kuelewa historia ya Biblia, utamaduni, maandishi, na muktadha, kwa sababu kuyachukulia maneno nje ya mazingira ya maelezo yake yanasababisha *Kutokuelewa vema au kulitafsiri isivyo*. Hili limekuwa na matokeo makubwa endelevu kwenye taaluma ya archeolojia na msigano wa kweli za maandishi kuthibitisha usahihi na uelewa sahihi wa Biblia.

Mbinu za Muislamu kuelewa Korani ni kinyume kabisa na mbinu za Wakristo kwenye Biblia. Uislamu, tofauti na Ukristo, haujawahi kamwe kuendeleza sayansi ya msigano wa maandiko, na hawakutilia umuhimu wowote kwa aina, Kihistoria na mazingira ya kitamaduni. Mawazo haya ya Uislamu yanaongezeka kwa fundisho lililokataa *bid’ah* (ubunifu), ambalo kimsingi humtisha mtu na Kuzimu (angalia Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 49). Matokeo ni kwamba “*sheria* [ambayo msingi wake ni Korani na Sunnah] hairuhusu nafasi ya kuifanyia mageuzi au kubadilika kwa tafsiri. . . . Kwa upendeleo wa Kiislamu kinyume cha ‘ubunifu’ na ‘utafsiri,’ *sheria* ilibaki kufunga kwa sehemu kubwa kwenye bodi ya utawala na mawazo yaliyoandaliwa ndani ya miaka mia tatu ya zama za Uislamu.” (Anyabwile 2011: 93)

Mbinu za Waislamu kwenye Korani zina madhara makubwa, siyo tu kwa Waislamu, Theolojia ya Kiislamu, na uhuru wa mawazo kwenye nchi za Kiislamu, lakini kwa Ulimwengu. Robert Spencer anaeleza, “Kwa ujumla, Wanatheolojia Uislamu hufuata mafundisho ya Ibn Ishaq: wanaziheshimu sura za Madina— ambazo zilianzisha mafundisho makubwa ya Kikorani kwenye kupigana vita na Wasioamini kwenye Uislamu —zilizopewa kipaumbele dhidi ya zile zilizoteremshwa mwanzoni kule Maka. Hizi kwa ufanisi huingiza uhalali wa ukatili wa hali ya juu wa Korani na adhabu za hali ya juu.” (Spencer 2009: 223) Kwa sababu hiyo. Siyo jambo a kushangaza kwamba Magaidi wa Kiislamu huhalalisha kila tendo la mauaji na Ugaidi kwa kuinukuu Korani (na Sunnah). Suala siyo *Waislamu*. Suala ni Uislamu na Korani yenyewe. Isipokuwa na mpaka hapo kimsingi Korani itakapo tathminiwa upya, kutafsiriwa upya, na kutumika tena *ndani ya Uislamu*, hapatakuwa na Amani duniani. Kwa bahati mbaya, kutoka kwenye kile tulichokiona, nafasi ya hili kutokea kwa ufanisi haipo.

6. KUUNGANISHA MGAWANYIKO BAINA YA UISLAMU NA INJILI

I. Utangulizi

David Garrison anaeleza: “Upepo unavuma kuipitia nyumba ya Uislamu. . . . Harakati za Uislamu kuja kwa Yesu Kristo zinaendelea kwa kiwango ambacho hatukuwahi kukishuhudia kabla. Kwa ajili ya uwazi na kuaminika, hebu tueleze mwenendo wa Uislamu kuja kwa Kristo kwa angalau kwa kuanzishwa makanisa mapya 100 au batizo 1,000 ambazo zilitokea kwa kipindi cha miongo miwili. Leo hii, Zaidi ya maeneo tofauti 70 kwenye mataifa 29, harakati mpya za waliokuwa Uislamu kumfuata Kristo zinaendelea. Kila harakati hizi zilipovuka vizingiti kwa uchache makanisa 100 mapya yalianzishwa au waamini wapya 1,000 walibatizwa, wote hao walikuja kwa Kristo kwa miongo miwili iliyopita. Kwenye baadhi ya nchi idadi imekuwa kutokana na mwenendo huu mpya kuwa makumi kwa maelfu. . . . Hakuna ukomo wa umbali kwa Ulimwengu wa Uislamu, jamii hii mpya ya Imani imetawanyika, kutoka Afrika ya Magharibi Sahel hadi kufikia visiwa vya Indonesia— na kila mahali miongoni mwa nchi hizo.” (Garrison 2014: 5-6; angalia pia Miller na Johnstone 2015: 1-19)

II. Masuala ya Jumla

Matukio binafsi au mazingira (kisiasa, vita, vurugu, majanga, hali ya uchumi, kuhamia kwenye makazi mapya, kutamani Baraka au nguvu, na msukumo wa kitamaduni) vinaweza kuhusiswa kwenye kuwafungua watu kuipokea Injili (Woodberry 2005: 12-13; Woodberry, Shubin, na Marks 2007: 85; Miller 2014: 24-25; Farrar 2013: 14; Miller na Johnstone 2015: 10-12; Abdulahugli 2005: 162-63). Kwa kiwango chake mwenyewe, Muislamu wa awali, mmissionari ambaye alikuwa akifanya kazi na Uislamu, na watafiti alionyesha baadhi ya kweli ambazo zinawaongoza Uislamu kumgeukia Kristo na ambazo zinasaidia kuwawezesha mashuhuda wa Injili kwa Uislamu.

A. Kweli zinazowaongoza Waislamu kumgeukia Kristo

Baadhi ya tafiti za kina zilizowahusisha mamia ya Uislamu kutoka sehemu tofauti tofauti za ulimwengu ambao walikwisha kumgeukia Kristo ziliendeshwa na kuzitambua sababu za muhimu ambazo huwaongoza Uislamu kugeuka kutoka kwenye Uislamu na kumfuata Yesu Kristo. Baadhi ya sababu kuu *zilizotambuliwa na Uislamu ambao walimgeukia Kristo* ni hizi zifuatazo:

1. Waongofu Waislamu 750 kutoka kwenye kila kanda kuu ya Ulimwengu wa Waislamu. J. Dudley Woodberry na wenzao waliandaa dodoso la kina ambalo liliwahusisha/kamilishwa na Zaidi ya Waislamu 750 ambao waliongoa na kumgeukia Kristo kutoka kila kanda kuu ya ulimwengu wa Waislamu. Kwenye Makala ya mwezi October 2007 ilieleza sababu walizotoa Waislamu za kwanini walimgeukia Kristo kwa mpangilio wa umuhimu (Woodberry, Shubin, na Marks 2007: 80-85):

- *Upendo: maisha ya Wakristo, maisha ya Imani kuonekana kwa nje*—Georges Housney alilithibitisha hili: “Kati ya mwaka 2005 na 2008 . . . aliandaa dodoso lenye maswali 12 na kuwapatia Zaidi ya watu 120 kwenye mikutano tofauti. Wengi wa Wakristo waliotokana na Uislamu walieleza kwamba Upendo wa Wakristo ulikuwa sababu kubwa ya kuwavuta wao waje kwa Kristo. . . . [Dr. Everett Boyce] aliwahoji watu kumi na saba wa Nchi ya Indonesia waongofu waliotoka kwenye Uislamu kwa jitihada za kutafuta/kugundua sababu kuu ambazo ziliwafanya wao waongoke. Haiwezekani kuja kama mshangao mwingine wowote kwamba asilimia mia moja walivutwa na Upendo ambao Wakristo waliwaonyesha.” [Housney 2010: 186-87]; angalia pia Woodberry na Shubin 2001: “Lililo kuu zaidi ya hili ni Upendo” [“Kwa mbali, sababu kuu iliyoonekana yenye ushawishi kwa idadi kubwa ya Uislamu waliomgeukia Kristo ni nguvu ya Upendo”]) Wakati Upendo wa Kristo unapodhihirishwa na Wakristo wa kweli kwenye kuipenda jamii, Uislamu wengi walitaja shauku ya kuungana na ushirika huu kama unaofuata kwa umuhimu. “Kundi la pili la Upendo ni ule ambao ulionyesha moja kwa moja na Mungu na kushuhudiwa

na maandiko” (Woodberry na Shubin 2001: “Lililo kuu Zaidi ya hili ni Upendo”) Hili lilionekana maalum kwenye upendo ulioelezwa na maisha na mafundisho ya Yesu. “Tabia ya Kristo wakati wote huonekana kwa Uislamu kama mvuto mkubwa mno” (Woodberry na Shubin 2001: “Yesu”)

- *Nguvu za Mungu katika majibu ya Maombi na Upanyaji*
- *Kutokutosheka na aina ya Uislamu waliokuwa wameuzoea*—Kwenye kujifunza kwao kutoka kwa Uislamu waliouacha Uislamu, Muislimu professors Khalil na Bilici walipata: “Misukumo miwili mikuu ilitambuliwa kwenye utafiti wetu kama ifuatayo: (1) *Hali za Wanawake kwenye Uislamu*. Suala la Jinsia kujitokeza wazi wazi kwenye simulizi hii, kwa hali ya wanawake kwenye Uislamu kuwa na msukumo mkubwa kiakili, na Uislamu kuwanyanyasa wanawake kuwa na msukumo mkubwa wa kijamii. (2) *Uislamu kuwa makatili, kukandamiza na mambo ya nyuma*. Hili lilihusisha aina mbili za tathmini. Ya kwanza ni kwamba, ni kulinganisha tabia za Uislamu na Wasio-Uislamu, Baadhi ya walioongoka walijikuta tabia za sasa kuwa za kuvutia zaidi. Ya pili ni kwamba wengine wanadai kwamba kubadilika kwao kunawiana Zaidi na kukataa tabia za Kiislamu kuliko mvuto wao chanya kwa tabia za Wasio-Uislamu” (Khalil na Bilici 2007: 120; angalia pia Farrah 2013: 16-17 [“kubadilika kwa wanawake kunashawishiwa zaidi na kutambua kile Yesu alichowatendea wanawake kwenye Injili”])
- *Maono na ndoto*—“Zaidi ya moja ya nne ya wale waliochunguzwa walieleza kwa msisitizo kwamba ndoto na maono yalikuwa ufunguo wa kuwavuta wao kwa Kristo na kuwawezesha kupita kwenye nyakati ngumu” (Woodberry na Shubin 2001: “Nilikuwa na ndoto”; angalia pia Greeson 2007: 50, 79-91)
- *Ujumbe wa Injili, hasa uhakika wake wa wokovu na msamaha*
- *Kweli za Kiroho kwenye Biblia*—“Nimezipitia shuhuda zilizoandikwa na Uislamu waliozaliwa ndani ya angalau nchi thelathini na tatu tofauti. . . . Kati ya hizo Zaidi ya nusu ya ukurasa kwa urefu, ni mbili tu ambazo hazikuwa na rejea kwenye Biblia, Agano Jipya (Injili), malinganisho ya Korani na Biblia, au nukuu zinazofanana.” (Maranz 2005: 61; angalia pia Brown 2006a, 2006b, and 2006c kwa mtazamo wa Kibiblia ambao una mvuto kwa Uislamu, na jedwali lenye sifa za kina za daraja, mfanano, Utofauti, na vikwazo baina ya Biblia na mtazamo wa ulimwengu wa Uislamu)

Leith na Andrea Gray wanazungumzia mwingiliano baina ya umuhimu wa Biblia kwenye uso wa nguvu na ufahamu wa Kiislamu wa mtazamo wa Kiulimwengu: “Moja ya nguvu iliyopo kwenye mtazamo wa Kiulimwengu wa Uislamu ni kwamba imefungamanisha pamoja makundi yenye mawazo ya kutatanisha kwenye mtandao wa mahusiano. . . . Ili ujumbe wa Kibiblia na mtazamo wa Ulimwengu kupata nafasi ya kweli kwenye maisha ya mtu, sura yote ya Kibiblia ni lazima ionekane. Hadithi ya Kibiblia ni ya kushawishi na simulizi inayovutia, lakini mantiki yake inaweza kuonekana kwa mapana ya mafafanuzi na kukariri.” (Gray and Gray 2008: 133; angalia pia Greenlee 2006: 22 [“Kwenye utafiti wangu kwenye nchi za Kiislamu, Nilibainisha umuhimu mkubwa wa kuwa na kozi ya mawasiliano ya Biblia (BCCs) kwenye mchakato wa mabadiliko. . . . Uislamu mara zote huhitaji muda mrefu kwenye mchakato wa kupata matokeo yaliyo bora ya kiwango cha kiufahamu juu ya kifo cha Yesu, kufufuka kwake na kuwa kwake Mwana wa Mungu.”]) Kwenye kusudi hili, kuwafanya waumini wapya kuwa *wanafunzi* ni ufunguo (angalia Greenlee 2006: 25-26; Garrison na Garrison 2008: 212-13 [kuwafanya wanafunzi ni moja ya nguzo tano kwenye harakati za kupanda Mkanisa]). Hakika, kikosi kilichofanikiwa cha Waamini waliotoka kwenye Uislamu huko Mashariki ya Kati “hujikita kwenye Uanafunzi, na siyo kwenye mabadiliko. . . . Tunaweka jitihada zetu kwenye Uanafunzi kwanza. Tunaamini kwamba mtu atakuwa na Imani halisi baada ya kuufundishwa ukweli.” (Daniel 2010: 40; lakini angalia Daniels 2015: 38 [mkakati wa uanafunzi “Kwanza” siyo vitendo endelevu vya kawaida miongoni mwa watendakazi wengi wenye tija kwenye maeneo ya Uislamu])¹⁸

Kwenye Makala mbili za awali, Woodberry alizungumzia sababu zinazofanana ambazo Uislamu huelezea kwa ujio wao kwa Kristo (Woodberry na Shubin 2001: n.p.; Woodberry 2005: 11-22; angalia pia Straehler 2007: 1-2

¹⁸ Umuhimu wa Uanafunzi unaonekana kweli kwamba Kwa Uislamu kusali kile kinachoitwa “sala ya toba” au kufanya “maamuzi ya kumpokea Kristo” “haimaanishi kwamba ni lazima kwao wote kuhudhuria Kanisani, kuhusiana na Biblia au maombi, kwa uchache Zaidi kwamba wangebatizwa. Hili kwa ujumla linamaanisha kwamba kwa wakati ule alipokutana na Mkristo (au wavuti) mtu huyu, kwa namna nyingine, hasa hasa kwa maombi ya wakati huo, humkubali Yesu kuwa ‘Bwana na Mwokozi wao’ na kumwomba Mungu awasamehe dhambi zao. Hili halimaanishi kwamba wameelewa kwa uhakika kile kilichotokea au kwamba kile wanachojisikia kwamba wanafanya kile ambacho Wakristo wanacho kwenye ufahamu wao. Muislamu mmoja alisimulia kwamba aliisema sala hiyo kwa heshima ya rafiki yake Mkristo kwa ufahamu kwamba kwakuwa Uislamu tayari wanamkubali Nabii Yesu, hakuna ambacho ni kinyume na Uislamu kuhusiana na hilo. . . . Wakati malengo ya wamissionari yaweza kuwa ni kumwona mtu huyo akiwa mtendaji kwenye Kanisa la mahali na kukua Kiroho, kwamba si la lazima kwa kile kinachotokea baada ya mtu ‘kufanya uamuzi kuja kwa Kristo.’” tu (Miller na Johnstone 2015: 6)

kwa ufupisho wa Makala tatu za Woodberry, Miller 2014: 16-19 kwa ufupisho wa Makala ya kwanza, na Perry 2015: 6 kwa ufupisho wa Makala ya tatu).

2. Waongofu Waislamu 170 wengi wao ni kutoka Afrika (70 kutoka Sudan). Jean-Marie Gaudeul anachambua Uislamu-Wakristo 170 walioongoka/kubadilisha dini, wengi miongoni mwao wakiwa ni Waafrika, na kuandaa funguo za kweli saba ambazo ziliwavutia Uislamu kuja kwa Kristo (Gaudeul 1999; angalia pia Gaudeul 2005: 81-92; Gaudeul n.d.: n.p.; na Miller 2014: 19-23 kwa mafupisho ya tafiti za Gaudeul):

- Yesu anavutia sana
- Kiu ya kweli
- Watu wasio na familia hutafuta jamii mpya
- Mvuto wa jamii ya Mungu—Kanisa
- Hitaji la msamaha
- Kiu kwa ajili ya Mungu
- Mwito kutoka kwa Mungu

3. Waongofu Waislamu 390 kutoka Afrika ya Mashariki. Ben Naja aliwachunguza Zaidi ya Wakristo 300 waliokuwa Uislamu hapo awali kutoka Afrika ya Mashariki mwaka in 2011 (Naja 2013a: 27-29; Naja 2013b: 155-60). Aligundua kwamba waamini wengi waliamua kumfuata Yesu kwa kupitia kweli mtambuka. Miongoni mwa Kweli hizo muhimu ni hizi zifuatazo:

- Aya zinazomhusu Yesu kwenye Korani—64%
- Upendo na ushuhuda wa wafuasi wengine wa Yesu—57%
- Kukutana na nguvu zisizokuwa za kawaida (njozi, maono, uponyaji, kufunguliwa)—41%
- Biblia—30% (Naja 2013a:28).

B. Kweli zinazowawezesha mashahidi wa Injili kwa Waislamu

“Kuwashirikisha Uislamu, ni lazima tuwaone kama watu, siyo tu kama wawakilishi wa dini ya kigeni, tamaduni, au mawazo ya kisiasa. Kama watu, ni mazao ya vitu hivyo, lakini pia wao ni wanaume na wake, watoto na wanafunzi, madereva wa magari na madaktari wa moyo. Wao pia ni watoto wa Mungu waliopotea, na alitupa kazi ya kuwafanya wanafunzi kutoka miongoni mwao.” (Houssney 2010: 13) Wakiwa na hili akilini, na nuru ya sababu gani huwafanya Uislamu kumgeukia Kristo, zipo hatua ambazo huwawezesha washuhudiaji wa Injili kwa Uislamu. Zifuatazo ni baadhi ya kweli hizo:

- *Maombi*. Kumshuhudia yeyote, hasa pale ambapo pana ushawishi wa kitamaduni, tofauti za kitheolojia, na mgongano wa kihistoria baina ya Ukristo na Uislamu yote yaliyotamkwa, ni jitihada za hali ya juu za Kiroho (Hammond 2010: 158; Morin 2007: 134-36; Greeson 2007: 98, 258-59; Houssney 2010: 115-16, 126; Perry 2015: 3; Goldmann 2004: 130; Michael na McAlister 2010: 119; Nehls na Eric 2009b: 95; Adams, Allen, na Fish 2009: 80). Maombi siyo tu muhimu kama maandalizi, lakini kuwafungua Uislamu kwa maombi pia ni muhimu. Dunning alipata, “Washiriki wengi walijia Imani kwa ufanisi kwa sababu watetezi wao waliwafanyia maombi ya wazi pale walipo, kwa ujumla kuanza kuwatembelea na kuwauliza mahitaji yao washiriki wanaweza kupata kile ambacho watetezi wao watawaomba” (Dunning 2013: 278; angalia pia Daniels 2015: 40).
- *Mtazamo wa kufanana na Kristo*. Kuwa mnyenyekevu na kujiandaa kusikiliza; usiwafikie Uislamu ili kubishana, lakini kumbuka wakati wote vita viko moyoni, siyo kwenye ufahamu (Hammond 2010: 157; Houssney 2010: 45, 87, 117, 125-26; Greeson 2007: 98, 250-55; Perry 2015: 5; Gilchrist 2002: 9-10, 12-13; Goldmann 2004: 131-32; Michael na McAlister 2010: 119-20; Nehls na Eric 2009b: 95-97). “Elezea, usibishane” (Goldmann 2004: 139). Sehemu ya muhimu ya mbinu hii ni kuuliza maswali. Kama Daktari anayetaka kuchunguza hali ya kiafya, tunahitaji “kugundua kile wanachokijua, wanajisikiaje, na wanataka nini. Lililo la muhimu zaidi, ni muhimu kutathmini viwango vyao vya kile wanachokipenda na uwazi wao. Wainjilisti wengi sana kwa kweli hawajihusishi na watu wanaowahubiria. . . . Wakati unapowauliza watu maswali unadhihirisha kwamba unajihusisha nao, wakati pia unapokusanya habari unazozihitaji ili kuzungumza na maisha yao kwa hekima ya kufaa.” (Houssney 2010: 129-30; angalia pia Nehls na Eric 2009b: 122-24)¹⁹

¹⁹ Houssney anaonya kuuliza maswali mengi sana kuhusiana na Uislamu wenyewe. Uislamu wengi wamefundishwa kushindana na Wakristo. Kwa hiyo, “jaribu kuepuka maswali ambayo yatampa Muislamu jukwaa la kukushawishi wewe kwa umuhimu wa Uislamu. Haya ni makosa ya kawaida ambayo Wakristo hufanya kuhusiana na Uislamu. Jaribu kusahau kwamba mtu uliye naye ni Muislamu: mtendee kama mtu wa kawaida. Wengi wa Uislamu ambao siyo washika dini wataiweka dini mbele wanapojihusisha kwenye majadiliano kuhusu Uislamu, wakati hawawezi kamwe kuelezea kama hutafanya hivyo.” (Houssney 2010: 132-33)

- *Shughulikia kweli za kitamaduni ambazo Uislamu wanaona ni za muhimu.* Jifunze ni nini kinachokubalika (*halal*) na Yaliyoharamishwa (*haram*) kwenye jamii ya chini ya Uislamu. Epuka kuwaudhi Uislamu kwa mavazi yasiyofaa au tabia. Kiuhalisia haya yaweza kuhusisha matumizi ya mkono wa kulia hasa pale unaposalimia, kula, na kubebea kitu unapomkabidhi mtu, kuvaa mavazi ambayo yanakubalika kulingana na mafundisho ya kidini ya kitabu kitakatifu, kuhakikisha kwamba Wanawake Wakristo wanavaa mavazi ambayo hayakubana na ambayo ni marefu kufunika mikono na miguu yao, kuwa na umakini mkubwa unapohusiana na watu wa jinsia tofauti na wewe (e.g., epuka kuwahudumia ukiwa pekee yako watu wa jinsia tofauti na wewe; wakati unapowaombea wagonjwa, wanaume ni lazima wawawekee wanaume wenzao mikono na wanawake kuwawekea wenzao mikono), na kutokula nyama ya nguruwe. (Hammond 2010: 157; Morin 2007: 118-25; Perry 2015: 5; Goldmann 2004: 135-36, 142; Nehls na Eric 2009b: 100-102; Daniels 2015: 40; Adams, Allen, na Fish 2009: 77-78)
- *Ukarimu.* Kuwa mkarimu, na kubali ukarimu wa rafiki yako Muislamu (Hammond 2010: 157; Houssney 2010: 120 [“Ukarimu umebeba jukumu kwenye hadithi ya wongofu wa karibia kila aliyekuwa Muislamu”]; Greeson 2007: 72-75; Goldmann 2004: 137-38; Nehls na Eric 2009b: 101-02). Ukarimu unaweza kuwa ufunguo wa kutambulisha kile Greeson anachokiita “mtu wa amani.” Alielezea, “Tumejifunza kwamba kumpata mtu wa Amani ya Mungu ni hatua ya kwanza ya muhimu kwa kuongeza harakati za waamini wapya kuja kwa Kristo” (Greeson 2007: 68). Hutumia **Luka 10:1-20** kama kielelezo kwa kwenda na kutafuta mahali gani ambapo Mungu tayari yupo kazini na kuwatambua Uislamu wale ambao wana nia (i.e., watu wa amani) (Ibid.: 68-78). Hatimaye, ni watu hao ambao, mara wanapokuja kwa Kristo, watakuwa Wainjilisti wenye ufanisi mkubwa na wapanda makanisa ndani ya jamii ya Uislamu kuliko wale ambao ni wa “kutoka nje ya eneo/Uislamu.”
- *Simamia malengo juu ya Yesu na Injili.* Ijue vizuri Biblia na Injili, hakikisha unayo Biblia na uweze kuitumia, na ufanye ujumbe wako kuwa mrahisi, wazi, na wa kufaa, ukilenga kwenye misingi ya injili: dhambi na suluhisho lake—kwamba Yesu ni Mwokozi wa Ulimwengu na kupitia yeye pekee tunapata msamaha wa dhambi (Morin 2007: 103-07; Hammond 2010: 157-58; Gilchrist 2002: 13-15; Goldmann 2004: 132-34, 141; Houssney 2010: 20, 121-23).

Mwanzoni, jaribu kuepuka misamiati ambayo Uislamu hawataielewa na watatengeneza vikwazo kwa Imani (e.g., kumwita Yesu “Mungu” au “Mwana wa Mungu” lini “Neno la Mungu” au “Isa al-Masih” watafanya au; kumaanisha “Roho Mtakatifu,” ambapo pengine kutawafanya wachanganyikiwe na Gabriel, wakati “Roho kutoka kwa Mungu” watafanya; kumaanisha “Utatu”) (Morin 2007: 107-10; Straehler 2009: 164; Goldmann 2004: 133, 140; Gray na Gray 2008: 129). Kwa kutumia misemo hiyo wakati huo huo “kunaweza kutengeneza kikwazo kwa ushuhuda zaidi. . . Ni vema kuanza na Ufahamu wa Uislamu juu ya Allah kutoka kwenye mafundisho ya Kikorani.” (Goldmann 2004: 133, 141) Kama Uislamu watakuja juu au kupinga mawazo hayo, wanaweza kuyaelezea (angalia, e.g., Houssney 2011; Gilchrist 2002: 74-78; Goldmann 2004: 145-50).

- *Usiwe mhukumu.* Kama siyo lazima usiudhihaki au kuudhalilisha Uislamu, Mohamedi, Korani, au Allah (Hammond 2010: 158; Perry 2015: 5; Gilchrist 2002: 10-12; Goldmann 2004: 139-40; Michael na McAlister 2010: 121). “Mlango unaweza kufungwa au usipatikane kwa mtazamo wa chuki” (Hammond 2010: 158).
- *Vumilia.* “Dhana imeenea miongoni mwa Wakristo wa Kenya kwamba Wokovu ni matukio huria baada ya kuelezewa mara moja kwa injili ni lazima kubadilishwa na ufahamu kwamba Uislamu ambao wana safari ya kukutana na Kristo, wanahitaji muda kwenye masuala mengi hukua taratibu tu kwenye uelewa wa Imani ya Kikristo” (Straehler 2009: 271). Wakijengea msingi kwenye uzoefu wa kina wa Uislamu hasa huko Asia ya Kusini, Kevin Greeson anaelezea, “Kwa kawaida Muislamu hampokei Kristo kama Mwokozi kwa siku ya kwanza ya kuisikia Injili. Wastani wa muda kati ya kusikia na kuelewa injili aliyopokea na wakati halisi wa kuja kwenye Imani katika Yesu Kristo unaweza kutofautiana kati ya majuma matatu hadi miezi sita. Urefu wa muda mara zote hutegemea mawasiliano na muumini Muislamu ambaye atamsaidia kuhusiana na maswali atakayokuwa nayo.” (Greeson 2007: 38; angalia pia Dunning 2013: 273 [Mchakato wa Uislamu wa Palestina kumgeukia Kristo ulitofautiana “kutoka wiki moja hadi mwaka, kwa kawaida kwa kukutana mara nyingi na wainjilisti au baada ya usomaji wa Biblia wa hali ya juu”]; Farrah 2013: 14 [“Uzoefu wa jumla wa Uislamu, hata hivyo, ni kwamba wokovu ni mchakato wa polepole ambao huchukua hatua kwa miaka mingi”]). Kwakuwa ni kazi ya Kiroho, tunahitaji kumpa Roho Mtakatifu nafasi ya kufanya kazi yake. Maneno ya kutazama kwetu ni uvumilivu na subira (Goldmann 2004: 134, 137-39; Hammond 2010: 158; Gilchrist 2002: 12-13).

III. Kutumia Korani na desturi za Uislamu kuwaongoza Waislamu kwa Yesu Kristo na Injili

Bila shaka ufanisi wa juu humaanisha kujengea daraja mgawanyiko uliopo baina ya Uislamu na Injili ni

kuanzia pale Waislamu walipo, yaani, matumizi ya maneno ya Kiislamu, mazoea ya tamaduni zao, mfumo wa mawazo, na Korani yenyewe²⁰—hasa hasa kile inachokisema kumhusu Yesu—kama daraja la kushirikisha Injili ya Kibiblia ya Yesu “halisi”. Hili ni muhimu kwa sababu Roho na tamaduni za Uislamu “aliwafundisha na kuwavisha silaha za kukataa au kushambulia chochote kilicho tofauti na Uislamu” (Shayesteh 2004: 243). Kwa hiyo, kuanzia na maneno ya Kiislamu, mazoea ya tamaduni, mfumo wa mawazo, na Korani moja kwa moja huanzisha kiwango cha ukawaida baina ya Ukristo na Uislamu, kuwapa Uislamu viwango yakini vya faraja, na kuonyesha kwamba Wakristo huuchukulia Uislamu na Korani kwa umakini.

Kevin Greeson anaonyesha: “Kutoka kwa Waamini wenye asili ya Kiislamu ambao waliwavuna familia zao, marafiki na majirani zao kwa Kristo, tumejifunza kwamba Korani imejawa na madaraja mengi ambayo sisi pia tunaweza kutumia kuwaelekeza Uislamu kwa Yesu Kristo.” (Greeson 2007: 17) Wakati uo huo, “wakati Korani inafundisha kuhusiana na Allah yaweza kuwasikizisha kweli nyingi kuhusiana na Mungu ambaye alifunuliwa kwanza kwenye Biblia, Kamwe tusiichanganye Korani na Neno la Mungu” (Ibid.: 19). Korani siyo Injili lakini huwataka Uislamu kuiamini Biblia, ambayo ni mamlaka yetu ya mwisho. Kwa kifupi, Maneno ya Kiislamu, mazoea ya tamaduni, mfumo wa mawazo, na Korani yenyewe vyaweza kuwa daraja lenye ufanisi kwa ukweli wote wa Yesu na Injili vilivyofunuliwa kwenye Biblia.

A. Korani kama darajala injili: Mbinu za NGAMIA

“Mbinu ya NGAMIA” iliendelezwa na Waamini wenye asili ya Uislamu na imekuwa ikitumika sasa “kwa kile ambacho ni mgeuko mkubwa wa Uislamu kuwa Wakristo kwenye historia” (Greeson 2007: 16). Mbinu hiyo inawafundisha wote Wakristo waseme nini kwa Uislamu na kuwapa Uislamu ruhusa kutoka kwenye chanzo chao wenyewe cha Kimamlaka, Korani, “kusoma Biblia na kuyaangalia madai ya Kristo” (Ibid.: 18). Mbinu ya NGAMIA imeelezwa kwa kina na Kevin Greeson *Ngamia: Jinsi Uislamu wanavyomwamini Kristo!* (2007) na Greeson na Owen’s 2005 ufupisho wa kina wa mbinu ya NGAMIA (angalia pia “Ufupisho wa mbinu ya Ngamia” n.d. kwa ufupisho).

“**C-A-M-EL**” inasimama kwa: **C**—Chosen (Maryam alichaguliwa na Allah kwa kusudi maalum); **A**—Announced by Angels (Malaika alitangaza kuzaliwa kwa Masihi kwa Maryam); **M**—Miracles (Nguvu za Yesu zilifunuliwa kwenye miujiza yake); **EL**—Eternal Life (Yesu anajua njia na ni njia ya mbinguni) (Greeson 2007: 104). Kusudi la mbinu ya NGAMIA siyo lazima liwaongoze Uislamu kwenye Wokovu lakini kuwatambulisha wale Uislamu ambao wanataka kujua Zaidi kuhusiana na Yesu hivyo basi tunaweza kuwapeleka kweye Biblia ambapo tutaupata ukweli wote kuhusu Yesu na Injili. Mbinu ya Ngamia msingi wake ni **Q. 3:43-56** ambayo inasisitiza habari za Yesu Kristo:²¹

⁴³. Na (kumbukeni) Malaikawaliposema: Ewe Mariamu, kwa hakika Mwenyezi Mungu Amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kulikowanawake wa walimwengu.. ⁴⁴. Ewe Mariamu, umnyenyekee Mola wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao. ⁴⁵. Hizi ni habari za ghaibu Tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa mishale yao (kwa kura wajue) nani wao atamwanga Maria, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana. ⁴⁶. (Kumbukeni) waliposema Malaika: Ewe Mariamu, bila shaka Mwenyezi Mungu Anakupa habari njema za neno litokalo Kwake, jina lake Masihi Isa mwana wa Mariamu, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu miongoni mwa waliokaribishwa. ⁴⁷. Naye atazungumza na watu katika utoto na kwenye utu uzima, na atakuwa katika watu wema. ⁴⁸. (Mariamu) akasema: Mola wangu, nitampataje mtoto na hali mtu ye vote hakunigusa? Akasema: Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Huumba Anavyopenda; Anapohukumu jambo basi Huliambia tu, kuwa, basi huwa. ⁴⁹. Na (Mwenyezi Mungu) Atamfunza Kitabu na hekima na Taurati na Injili.. ⁵⁰. Na (Atamfanya) Mtume kwa wana wa Israeli, (kuwaambia), Nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nawaumbieni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege, kasha napulizia ndani yake, mara huwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninamponya kipofu na mwenye ukoma, na kuwahuisha wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninawaumbieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu; bila shaka katika

²⁰ “Mwaka 1984, Mfalme Fahd wa Saudi Arabia aliunda tume ya kutafsiri Korani kutoka kwenye Kiarabu kwenda kwa lugha zote za jamii ya Uislamu. Kwa kuwa Korani ilikuwa imebaki kwa lugha ya Kiarabu tu, *Maimam* wanashilikilia kwa nguvu kabwa sana na kuwatawala wafuasi wao. Kwa Uislamu watu wa kawaida sasa wanasoma Korani kwa lugha zao wenyewe, tafsiri zisizokubalika za *Maimamu* sasa zimewekwa wazi. . . . Siyo Maimamu tu ambao mamlaka yao imeathirika. Korani yenyewe yaweza kuthibitisha kuwa adui yao mkubwa/mbaya zaidi. Uislamu wanapoisoma Korani kwa lugha zao wenyewe wanaona jinsi ambavyo kwa kushangaza ina mambo machache sana ya kuwasaidia.” (Greeson 2007: 47-48)

²¹ Greeson anakumbusha kwamba “Uislamu wamezoea sana majina ya surah kuliko idadi yake” (Greeson 2007: 34-35). Hivyo, mtu anaweza kujifunza jina la surah moja anayoikusudia kuitumia (i.e., angalia kwenye “Surah Al-Imran” badala ya “Surah 3”). Sawa na hiyo, kama tafsiri ya Korani unayoitumia inatumia jina la Kiislamu kwa Kibiblia/mhusika wa Kikorani (e.g., Allah kwa Mungu; Isa au Isa al-Masih kwa Yesu au Yesu Kristo; Maryam kwa Maria), bila shaka utayatumia majina hayo kama yalivyo. Hata hivyo, *Usimwite* Yesu “Nabi Isa” (“Nabii Yesu”) hata kama rafiki yako Muislamu anamwita hivyo. Mwrite “Yesu, Masihi” (“Isa al-Masih”) badala ya “Nabi Isa” inamaanisha kwamba Yesu alikuwa “siyo chochote Zaidi ya Nabii” (Nehls na Eric 2009b: 90). Kwa maneno mengine, *usimwite* Mohamedi kama “nabii” au “Nabii Mohamedi,” kwa kuwa hilo linamaanisha unaamini alikuwa nabii halisi wa Mungu. Mtaje tu kama “Mohamedi” au, labda, “nabii wenu.”

hayo imo Ishara kwenu ikiwa ninyi mnaamini..⁵¹ Na msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ili niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa, na nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, kwahiyu Mcheni Mwenyezi Mungu na nitini.⁵² Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu, basi Mwabuduni; hii ndiyo njia iliyonyoka.⁵³ Lakini Isa alipoona kufuru yao, akasema: Nani watakuwa wasaidizi wangu kwa (njia ya) Mwenyezi Mungu? Wanafunzi wakasema: Sisi ni wasaidizi wa njia ya Mwenyezi Mungu, na ushuhudie ya kwamba sisi ndiyo wajisalimishao.⁵⁴ Mola wetu, tumeyaamini Uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi Utuandike pamoja na washuhudiao.⁵⁵ Na (Mayahudi) walifanya hila, na Mwenyezi Mungu Akafanya hila, Na Mwenyezi Mungu ndiye bora wa wafanyao hila.⁵⁶ (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: Ewe Isa, kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na Nitawaweke wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama; kisha marudio yenu yatakuwa Kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkihitilafiana.”

Kimsingi mbinu ya NGAMIA (CAMEL) imeandaliwa kuwaongoza Uislamu kuyaona mambo makuu matatu ya Yesu kutoka kwenye kipengele hiki: 1. Yesu ni Mtakatifu (**Q. 3:42-47**); 2. Yesu anazo nguvu hata dhidi ya mauti (**Q. 3:48-54**); na 3. Yesu anajua njia ya Mbinguni (**Q. 3:55**). Yafuatayo ni mapendekezo maalum kwa maelezo ya kufanya na kuuliza maswali kwa kutumia mbinu ya NGAMIA (mambo haya maalum yapo kwenye kitabu cha Greeson 2007: 106-09 na Greeson na Owen 2005: 12-18 [kiuhalisia ya mwisho hasa itakuwa na msaada Zaidi kwakuwa mambo maalum yameelezwa kwa kina na yapo kwenye wavuti]):

1. **Jinsi ya kuanza:** Baada ya utangulizi wa kirafiki sema kitu kama hiki:

“Nimekuwa nikisoma Korani na nimesoma huko ukweli wa kushangaza ambao unatupa sisi tumaini la uzima wa milele mbinguni. Unaweza kusoma Sura Al-Imran 3:42-55 kutoka kwenye Korani yako ili tuweze kulizungumzia hilo?

au

Nimekuwa nikisoma Korani na kugundua kwamba inasema jambo la kufurahisha sana kumhusu Yesu. Unaweza kusoma Sura Al-Imran 3:42-55 kwenye Korani yako ili tuweze kuzungumza kuhusiana na hilo?

(Itasaidia sana kumwomba rafiki yako Muislamu kukigawa kifungu hicho kwenye vifungu vidogo vitatu anapokuwa anavisoma—mst. 42-47, 48-54, na 55—na baada ya hapo mvijadili kila kimoja tofauti na kingine.)²²

2. **Q. 3:42-47—Yesu ni Mtakatifu.** Maswali na maoni pendekezwa:

- **Kuhusiana na mst. 42-44** (Kuzaliwa kwa Yesu kulitangazwa na Malaika). Uliza, “Je unaweza kumjua Nabii mwingine yeyote ambaye kuzaliwa kwake kulitangazwa na Malaika?” (Jibu ni “hapana”)
- **Kuhusiana na mst. 45** (Yesu ni “Neno la Mungu”). Uliza, “Hili linamaanisha nini kwamba Yesu ni Neno la Mungu?” Mtu anaweza kusema mstari haisemi kwamba tutazungumza neno la Mungu tu, lakini Yeye mwenyewe ni neno litokalo kwa Mungu.
- **Kuhusiana na mst. 45** (Yesu ni “al-Masih” [Masihi]). Uliza, “Hili linamaanisha nini kwa Yesu kuitwa (Masihi) al-Masih?” Wakati Yesu anaitwa “al-Masih,” Korani haifanani hili linamaanisha nini. Simamia kwenye Yesu kuwa aliwaahidi Mkombozi na Mwokozi—“Masihi.” Hakuna nabii mwingine aliyetwa Masihi. Pia, kulingana na mst wa 45, Yesu hatawekwa kwenye heshima tu ulimwenguni hapa pia hata kwenye ule ujao.
- **Kuhusiana na mst. 46** (Yesu ni “mwenye Haki”). Uliza, “Yesu alitenda dhambi?” (Jibu liwe “Hapana”) Hata hivyo, Mtu mmoja anaweza kusema kwamba, hakuna hata Nabii mmoja aliyetenda dhambi. “Wazo hili kwamba hakuna nabii aliyetenda dhambi ni imani ya kwaida miongoni mwa Uislamu, ingawaje Korani haifundishi hivyo.” (Greeson na Owen 2005: 14) Kwa kweli, Korani inatueleza kwamba Adamu hakumtii Allah (**Q. 20:116-21**), Musa alimwua Mmisri (**Q. 28:15-16**), Daudi alifanya haraka na hukumu isiyo sahihi (**Q. 38:21-24**), wengi wa manabii waliomba msamaha kwa dhambi zao: Nuhu (**Q. 11:47; 71:28**), Ibrahimu (**Q. 14:41; 26:82**), Sulemani (**38:30-35**). Mohamedi mwenyewe alikemewa na Allah na alihitaji msamaha kwa dhambi zake za wakati uliopita na ujao (**Q. 8:67-68; 9:43; 40:55; 47:19; 48:1-2**). Baadhi ya Uislamu wanaweza kukiri kwamba manabii “walifanya makosa” lakini siyo kwamba walitenda dhambi. Unaweza kuuliza, “Kuna tofauti gani baina ya makosa na dhambi?” Kimataifa au kutokutii kusikokuwa kwa kimataifa kwa Mungu bado ni dhambi.

²² Greeson anaonya kwamba “wakati wote ni vizuri kuitumia Korani ya rafiki yako Muislamu. Wasio Uislamu wanaoenda kwenye mazungumzo wakiwa na Korani mkononi tu bila shaka huwakwaza Uislamu.” (Greeson 2007: 100) Hili linamaanisha kwamba mtu anaweza kusubiri Muislamu alete Korani yake mwenyewe au kukupeleka nyumbani kwake au msikitini. Kama Korani haipatikani, Mambo ya msingi ya mbinu ya (NGAMIA) CAMEL yanaweza kukumbukwa na kuanzia hapo, na Muislamu atatiwa moyo kwenda nyumbani au msikitini ili akajisomee mwenyewe. Mnaweza kubadilishana mawasiliano na mkutano mwingine ukaandaliwa. Kwa maana nyingine, kwakuwa ulianza kumwambia Muislamu kwamba “Nimekuwa nikisoma Korani,” hakitakuwa kikwazo kama utaitumia Korani yako kama Muislamu hana yake au hajaweza kuwa nayo. Hata hivyo, kusiwepo na alama yoyote, maneno yaliyopigiwa mstari, yaliyokolezwa rangi, au maandishi yaliyoandaliwa ama kwenye nakala yako ya Korani au ya Biblia! Uislamu huona kuwa kuweka alama kwenye vitabu vitakatifu ni chukizo kubwa kama siyo kufuru (Nehls na Eric 2009b: 102).

Bila shaka itakuwa bora Zaidi tukijikita siyo tu kwamba Yesu hakutenda dhambi lakini ni kwa jinsi gani alivyokuwa mwenye haki. Greeson anapendekeza kuuliza, “*Yesu je alimwua yeyote? Je alikuwa na mahusiano yoyote (ya kingono) na mwanamke yeyote? Aliwahi wakati wowote kujaribu kujifanya utajiri mwenyewe?* Maswali haya ya utangulizi kwa upole kuondoa tofauti kwenye ufahamu wa rafiki yako Muislamu baina ya Yesu na Manabii wengine ambao anawafahamu vizuri sana pia.”²³ (Greeson 2007: 107) Kwa nyongeza, Kuonyesha kwamba Yesu aliwaponya watu na kutufundisha kuwapenda hata maadui zetu kunatuonyesha ni jinsi gani Haki ya Yesu ilivyozidi ya Nabii yeyote (ikiwa ni pamoja na Mohamedi).

- **Kuhusiana na mst. 47 (Yesu alizaliwa na Bikira).** Uliza, “*Mstari hii je inasema kwamba Yesu alikuja moja kwa moja kutoka kwa Mungu na kwamba hakuwa na Baba wa hapa Duniani?*” Ni muhimu kuwaonyesha Uislamu Upekee wa Yesu. Wakati huo huo, unaweza kuuliza, “Kwa mabilioni ya watu waliozaliwa, Kwanini ni Yesu tu aliyezaliwa na bikira bila kuwa na Baba wa ulimwenguni?” Kama jibu ni hili kwamba “ni ishara maalum ya Mungu kwamba Yesu alikuwa nabii,” jambo la kuendelea mbele ni hili “lakini kwanini ni *Yesu pekee?*—kwa nini ni Yesu ambaye ni wa kipekee sana miongoni mwa wanadamu wote ikiwa ni pamoja na Manabii?”

Unaweza kuuliza, “*Yupo nabii mwingine ambaye hana baba wa duniani?*” Jibu linaweza kuwa kwamba “Adamu hakuwa ma baba duniani.” Kwa majibu, ni wazi kwamba kwanini Adamu asingekuwa na baba duniani—kwa sababu alikuwa mwanadamu wa kwanza kabisa. Lakini siyo hivyo kwa Yesu. Muhimu zaidi, Adamu aliibua suala la dhambi na Yesu aliibua Haki. Adamu angeweza kutembea na kuongea na Mungu bustanini kwa sababu alikuwa mwenye haki na Mtakatifu. Lakini wakati Adamu alipotenda dhambi moja tu kwa kutokumtii Mungu mara moja tu, alifukuzwa kutoka bustanini na hakuruhusiwa kamwe kurudi huko (angalia **Q. 2:35-37; 7:10-25; 20:115-23**). Kwa hiyo unaweza pia kuuliza, “*Ni dhambi ngapi alizotenda Adamu zilizomfanya aondolewe kutoka kwenye uwepo wa Mungu na kutoka bustanini?*” (Jibu: moja tu.)

Baadaye tunaweza kueleza hili linamaanisha nini: Kwa sababu Mungu ni Mtakatifu kwa 100%, hakuna ambacho siyo kitakatifu kinachoweza kuwa kwenye uwepo wake. Hili linamaanisha kwamba kama mtu yeyote anataka kwenda mbinguni, ni lazima pia awe Mtakatifu. Kama Adamu alitenda dhambi moja tu na alifukuzwa mbele ya uwepo wa Mungu, basi kujaribu kufanya kazi njema za kutosha kufunika kila dhambi uliyotenda ni kazi isiyowezekana. Hatuwafundishi watoto wetu kutenda makosa. Wote tunao mwelekeo wa kufanya yale ambayo siyo sahihi. Hakika, ni lazima tuwafundishe watoto wetu kutenda haki.

Kwa kuwa wote ni uzao wa Adam, wote tulirithi asili yake ya dhambi. Lakini kwa Yesu, huo mstari wa damu ya Adamu ulikatwa! Yesu hakuwa wa mstari wa damu ya Adamu, kwa kuwa hakuwa na Baba wa duniani. Yesu alikuwa tofauti sana na Manabii wengine wote. Kwa hakika, Yesu alikuwa wa tofauti sana kutokana na watu wote ambao waliozaliwa! . . . Yesu alitoka kwa Allah. (Greeson na Owen 2005: 15)

Unaweza kuuliza, “*Kama Yesu alizaliwa bila Baba wa kibinadamu, anaweza kurithi asili ya dhambi ya Baba yake?*” (Jibu, wazi, ni “Hapana.”) Kwa maneno mengine, Yesu pekee ni Mtakatifu Mkamilifu.

3. **Q. 3:48-54—Yesu alikuwa na nguvu juu ya kifo.** Maswali pendekezwa na maoni:

- **Kuhusiana na mst. 49 (Mijiza ya Yesu, ni pamoja na kuumba uhai na kuwapa wafu uhai).** Uliza “*Mstari hii inatueleza ninini Yesu alichokifanya?*” Tafakari juu ya Yesu kuumba uzima na, hasa, uwezo wake wa kuwapa wafu uzima. Unaweza kuuliza, “*Unamjua Nabii mwingine yeyote ambaye anaweza kuumba uzima?*” Suala ni kwamba Yesu, na Yesu pekee, anazo nguvu juu ya adui yetu mkuu—kifo chenyewe!

Muislamu wanaweza kujibu kwamba Yesu alitenda mambo haya, lakini kwa mapenzi ya Mungu tu.” Unaweza kukubali kwamba kila kitu kinatoka kwa Mungu na kwa mapenzi yake. Lakini unaweza kuonyesha hili kwamba Yesu aliyatenda mambo haya kwa neno lake mwenyewe, bila kuuliza ruhusa ya Mungu.

Kwa nyongeza, **v. 49** unaonyesha kwamba Yesu anajua siri za mioyo yetu. Unaweza kuonyesha kwamba Mungu pekee ndiye mwenye kujua siri za mioyo yetu na kuuliza, “*Unamfahamu mwingine yeyote ambaye anajua siri za mioyo yetu?*”

- **Kuhusiana na mst. 50 (kumtii Yesu).** Uliza, “*Kwenye mstari ya 50, inatueleza sisi tufanye nini?*” (Jibu: mwogope Mungu na *mtii Yesu.*) Kwa hiyo, unaweza kusema kwamba, ingawa Korani imemtaja Yesu mara nyingi na kutueleza kumtii Yesu kwa kila atakachotuagiza, haijatuambia Yesu alituagiza tufanye nini.

²³ Mtu ni lazima awe makini kuhusiana na kuiinua tabia binafsi ya Mohamedi. Mwamini mwenye asili ya Uislamu bila shaka angeuliza, “Ni aina gani ya nabii, ambaye akiwa na umri wa miaka 53, alimchukua binti mwenye umri wa miaka sita kuwa mke wake? Na alianza kumwingilia alipokuwa na miaka tisa.” Hata hivyo, mtu ambaye hatokani na Uislamu anaweza kuogopa kuuliza hili moja kwa moja kwa sababu litaonekana kama shambulio la moja kwa moja kwa Mohamedi na linaweza kufunga mlango wa kuendelea kushuhudia (angalia Greeson 2007: 216-17, 248).

Isipokuwa tu kwenye Injili (Agano Jipya) tunaweza kuzisoma amri za Yesu. Hivyo, unaweza kuuliza, “*Kwa kuwa Korani inatueleza kuwa ni wajibu wetu kwa Mungukumtii Yesu, tunawezaje kumtii ikiwa hatujui alichotuaambia tufanye?*” au “*Ni jinsi gani tunavyoweza kujua Yesu alituagiza nini na jinsi gani ya kumtii pasipo kuisoma Injili?*”

Unaweza kumwuliza rafiki yako Muislamu, “Tuseme nimekuomba kunifanyia kitu fulani, lakini sikukueleza kikoje kile ambacho ninataka unifanyie. Utakifanya?” Kwa vyovyote ni lazima atasema, Hapana. Hawezi kufanya kile ulichomwambia kwa sababu hajui ni kitu gani! Kwa maana hiyo hiyo, asingetekeleza wajibu wake kwa Allah na kumtii Isa kwa sababu hajui kile ambacho Isa amekitaka afanye! Unaweza kutumia fursa hii kumtia moyo rafiki yako Muislamu kuisoma Injili (Injili/Agano Jipya) hiyo basi anaweza kuona ninini “Yesu alichomwambia afanye.” (Greeson na Owen 2005: 16)

Hili pia linaweza kutoa njia kwako kuwaonyesha Uislamu kutoka kwenye Injili ninini Yesu alichokisema. Unaweza kumwelekeza kwenye Hotuba ya Mlimani (**Mathayo 5-7**) alipofundisha Yesu na kuzibadilisha baadhi ya sheria za Agano la Kale (kama zilivyoonyeshwa kwenye **Q. 3:50**). Muislamu mmoja wa awali alipendekeza kwamba kwa mafundisho ya kuwasisimua Uislamu kwenda kwenye kifungu na kuuliza maswali kama vile, Ni nani huyo anayezungumza? Kwa nini anazungumza? Anamzungumzia nani? Anazungumzia wapi? Anajaribu kufundisha nini? Na ni jinsi gani ninavyoweza kuyatumia kwenye maisha yangu? Muislamu anajifunza kufungua maana ya maandiko kwake mwenyewe. Hili hasa ni muhimu, kwa hili Uislamu wengi hufundishwa kukariri Korani lakini “hawaruhusiwi hata kutafsiri neno rahisi sana kwenye Korani wao wenyewe. Wamepewa sharti kutafuta jibu kutoka kwa mmoja ambaye ana mamlaka ya juu” (Daniel 2010: 38; angalia pia Housney 2010: 88-89) Kwa kujifunza kutafsiri wenyewe, Biblia inaweza kuwa hai kwa maswali ya Uislamu na kusaidia kuwaweka huru kutokana na kuwategemea Maimamu. Hasa msisitizo pengine unaweza kuuweka kwenye kifungu ambacho Yesu alizungumza kwa habari ya kuja kwake na Yeye, kwa kuwa hizi ni hatua za mwanzo za uanafunzi (e.g., **Math 11:27-30; 19:28-30; Marko 8:34-38; Yohana 3:1-21; 6:35-40; 8:31-32, 42; 15:1-17**). Hili pia linatoa fursa kwako kumpatia Muislamu Biblia au Agano Jipya.

Unapoendelea kwenye sehemu ya mwisho ya kifungu unaweza kuuliza, “*Unaweza kumjua Nabii yeyote ambaye alikuwa na nguvu kuliko Yesu?*”

- **Kuhusiana na mst. 52-53 (Wafuasi wa Yesu).** Mstari wa 50 ulisema kwamba tunapaswa “kumtii Yesu.” Sasa unaweza kuonyesha kwamba kwenye mstari wa 52 wale ambao hujinyenyekesha kwenye mapenzi ya Allah *kama wanafunzi wa Yesu* wanaitwa “Waislamu” (ambalo linamaanisha “kujinyenyekesha kwa Mungu”). Mungu mwenyewe alilichukulia hili kwenye mstari wa 55. Kwa hiyo unaweza kuuliza kuhusu kile Mungu alichokisema atakifanya kwa wale ambao ni wanafunzi wa Yesu. (Jibu ni kwamba Mungu mwenyewe alisema, “*Nitawaweka wale waliokufuata [Yesu] juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama.*”) Kumbuka kwamba Mungu ameruhusu kwamba wanafunzi wa Yesu watainuliwa juu kuliko wengine, siyo tu mpaka Mohamedi atakapokuja, lakini mpaka siku ya ufufu!

4. **Q. 3:55 (Yesu anajua njia ya mbinguni).** Kuhusiana na njia ya mbinguni, uliza, “*Kulingana na mstari wa 55, Yesu yuko wapi sasa?*” Jibu ni kwamba Yeye yu hai pamoja na Mungu mbinguni sasa.

Kisha unaweza kuuliza, “*Tuseme ninataka kutoka hapa kwenda (kwenye mji fulani). Nitamchagua nani atakayenisaidia? Nitamchagua mtu ambaye hakuwahi kuwepo huko au mtu ambaye anajua njia na kuishi kule kwa sasa?*” (Jibu la wazi ni “Yule ambaye anaishi kule”)

au

“*Kama unataka mimi nije kwako na unajua kwamba nahitaji maelekezo/kuongozwa, ni nani atakayekuwa mwelekezaji bora kuniongoza njia?*” (Wazi, jibu ni “wewe mwenyewe”)

Kwa hiyo unaweza kusema, “Mtu ambaye anao uwezo mkubwa wa kunionyesha njia ni mtu yule anayeishi pale. Mimi ni mtu mwenye dhambi. Ingawa nimefanya mema mengi maishani mwangu, Bado mimi ni mwenye dhambi na kushiriki laana ya Adamu. Ninajua kwamba kwa nguvu zangu siwezi kamwe kuwa Mtakatifu kufikia kuwa pamoja na Allah mbinguni. Lakini kulingana na Korani, Yesu alitoka mbinguni na yupo hai pamoja na Mungu Paradiso leo. Kwa hiyo Yesu ni njia ya kutufikisha pale.”

Hitimisha na swali la mwisho: “*Ninahitaji kwenda Paradiso; unataka kwenda Paradiso. Yesu yupo Paradiso na anajua njia ya kwenda Paradiso. Miongoni mwa Manabii wote, ni yupi mwenye uwezo wa kutusaidia kufika Paradiso?*”

Kama Muislamu akimjibu “Yesu,” anaweza kuwa amekuwa tayari kwa kuyafuata macho yake kuuendea Wokovu. Katika hatua hii, hata hivyo, itakuwa mapema sana kumwongoza Muislamu “sala ya toba.” Unapaswa kuhakikisha kwamba ameelewa kwa uhakika kwamba Yesu ni nai hasa ni (Mungu kamili na mwanadamu kamili) na kile Yesu alichokifanya (aliishi maisha tuliyopaswa kuyaishi, kufa kifo tulichopaswa kufa, na kulipia gharama kwa ajili ya dhambi zetu vinginevyo tulipaswa kulipa lakini kamwe haikuwezekana).

Kwa maneno mengine, anatakiwa kuielewa vizuri injili na kule kuiamini injili na kumpokea Yesu kama Mwokozi na Bwana kunamaanisha nini na kudokeza nini (ikijumuishwa na ukweli kwamba atakabiliana na upinzani kutoka kwa familia yake au Waislamu wengine). Suala ni kwamba ama anaelewa na anajitoa kuufuata ukweli. Hili linaweza kuchukua muda lakini ni muhimu.

Kwa namna nyingine, kama atasema, “Mohamedi,” kisha mwambie asome **sura 46 (Mchanga wa vilimani), mst. 9:** “*Sema: [Mohamedi] Mimi si mpya katika Mitume, wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa ninyi. Sifuati ila yaliyofunuliwa kwangu; na mimi siye ila ni Mwonyaji dhahiri.*” Usiwe mpiganaji lakini mwanana kwenye kusema, “*Kama utachagua miongoni mwa mtu ambaye hajui kitakachotokea kwake [au kwenu] baada ya kufa na mtu ambaye tayari yuko mbinguni, ni mtu yupi ambaye atakuongoza?*” (Greeson 2007: 109)

5. **Hifadhi vitu kulingana na Korani.** Waislamu wanaweza kujibu kwa kukariri hadithi za nabii kutoka kwenye Hadithi. Tunawataka kukabiliana na kile ambacho kwa uhalisia Korani inasema kumhusu Yesu. Kwa hiyo, kama Muislamu akipata njia kutoka kwenye maandiko na maana ya kifungu kwenye Korani unayojadili, unaweza kuuliza, “*Hili lipo kwenye Korani, au ni kwenye Hadithi?*” Ikiwa jibu ni “Hadithi,” unaweza kujibu, “*Unaamini kwamba Korani ni kamilifu na Neno la mwisho la Mungu, sivyo? Basi, kuendelea na kile ambacho Korani inakisema.*”

Ikiwa watakuambia ni, “Korani,” unaweza kusema, “*Hili ni jambo jema sana; Ninajifunza kuhusu Korani. Unaweza kunionyesha mahali lilipo kwenye Korani? Ningependa kulisoma.*” Mara nyingi hawataweza kujua iko wapi. Kwa hakika mara nyingi ni kwa sababu halipo kwenye Korani. Kama hawataweza kukuonyesha lilipo, kiufupi unaweza kusema: “*Tuendelea kuangalia kile ambacho tuna kiona hapa kwenye Korani.*” (Greeson na Owen 2005: 17)

B. Korani kama daraja: upeo mwingine wa mawasiliano

1. “**Njia ya iliyo sawa**” (**Q. 1:6**). **Q. 1:6** inasema, “*Tuonyeshe njia iliyo sawa.*” Hilali-Khan analitafsiri hivi, “*Tuongoze kwenye njia iliyo sawa.*” Hili kiasili linatuongoza sisi kwenye suala la dhambi ya mwanadamu na ile asili ya uovu wa kuzaliwa nao, i.e., hali ya kutokuweza kwa yeyote mara kwa mara au kufuata “njia iliyo sawa kikamilifu.” Kwa namna nyingine, Yesu alisema, “*Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; hakuna ajaye kwa Baba bila ya kunipitia Mimi*” (**Yohana 14:6**). Vivyo hivyo, kama **Q. 3:50** inavyosema, Jukumu letu ni kumtii Yesu. Kwa kujua tu ninini Yesu anachokisema kwenye Injili (Agano Jipya) tunaweza kujua njia iliyo sawa ili tuweze kuifuata. Hivyo, **Q. 1:6** ni daraja zuri kwa Yesu na Injili, hasa hasa kwakuwa **Q. 1:6** inatumia maneno yale yale ambayo Yesu aliyatumia kujieleza Yeye mwenyewe, i.e., “Njia.”

Georges Housney anatupa mfano wa mazungumzo mafupi aliyokuwa nayo na Muislamu (Fareed), akitumia maswali kumfikisha Fareed kuuona ukweli uliopo nyuma ya **Yohana 14:6:**

“Fareed, Yesu alisema “Mimi ndimi njia”. Hili linamaanisha nini?”

Alifikiri kwa muda. ‘Umm, kama barabara?’

‘Ndiyo,’ Alitikisa kichwa. ‘Barabara ya kwenda wapi?’

Fareed kwa uhalisia alionekana kuchanganyikiwa. ‘Uhh...’

‘Njia ya kwenda kwa Mungu,’ Nilisema, kuziunganisha nukta kwenda kwake.

‘Ahh!’ Niliuona uso wa Fareed uking’aa kwa kupata uelewa. . . . Nilimwuliza Fareed atueleze ninini alichokielewa kwa kila neno kwenye aya na watu tofauti kwenye timu walianza kumsaidia kwa maswali yake. Mawasiliano halisi yalianza kushika kasi. Mwanangu Pierre alimchukua pembeni na kutumia saa mbili kusoma na kuielezea Injili kwake wakati sisi wengine tukiwa tunawatafuta Waarabu wengine kuzungumza nao.

Yapo masomo kadhaa ambayo twaweza kujifunza kutokana na mkutano huu:

1. Ingawa kifungu chaweza kuonekana kirahisi kwako, usidhani wengine wanakielewa.

2. Waache wakusome Biblia, na waruhusu wajaribu kukuelezea.

3. Hakikisha wanaelewa kile unachokizungumzia kwa kuwauliza yanayofuatia. Usiulize tu, Unaelewa? Wengi watajibu ndiyo kuepuka aibu (usumbufu).

4. Wape nafasi wajaribu kujibu maswali yako. Ruhusu mchakato wao wa kugundua mafumbo kama ulivyowatajia na maswali pendekezwa.” (Housney 2010: 133-34)

2. “**Vazi la Hhaki**” (**Q. 7:26**). **Q. 7:26** inasema, “*Enyi wanadamu, hakika Tumewateremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo. Na nguo za utawa ndizo bora. Hayo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kushika mauidha!*”

Aya hii inainua suala la uovu wa mwanadamu wa kuzaliwa nao, ukweli kwamba hakuna kati yetu anayeweza kuwa mkamilifu na mwenye haki, na ukweli kwamba yupo mtu mmoja tu ambaye ni mkamilifu na mwenye haki—Yesu Kristo—sawa na ambavyo suala hili liliibuliwa kwenye mbinu ya NGAMIA (CAMEL)

kwenye **Q. 3:46-47** (angalia hapo juu). Aya hii pia inaibuua suala la Neema ya Mungu: *aliwafunika nguo juu yenu ili kuifunika aibu yenu*. Hatuwezi kuupata Wokovu wetu au “vazi la haki” kwa sababu mioyo yetu imelemewa na dhambi na hatuwezi kuibadilisha mioyo yetu bila kujali ni kwa jinsi ya juhudi kiasi gani tutajaribu. Hata hivyo, kama Mungu alivyompa Adamu vazi la mwili kuificha aibu yake ya mwili, hivyo alitupa “vazi la haki” la Kiroho kwa ajili yetu kupitia kwa mwanadamu Yesu Kristo na aliwapa muamana wa *Haki yake* wote waliompokea Kristo kwa Imani. **Q. 7:26** laweza kuwa daraja zuri la kuwaelekeza Uislamu kwenye Injili. “Vazi la Haki” limejadiliwa kwenye vipeperushi viwili vya Uislamu rafiki na R. M. Harnisch.²⁴

3. Yesu kama “ishara” kutoka kwa Allah (Q. 19:21; angalia pia Q. 21:91; 23:50). Q. 19:21 inasema, “(Malaika) akasema: Ni kama hivyo; Mola wako Amesema: Haya ni rahisi Kwangu, na ili Tumfanye Ishara kwa wanadamu na rehema itokayo Kwetu; na ni jambo limekwisha hukumiwa.” Ukweli kwamba Korani kiuhalisia inamwita Yesu “Ishara” ni muhimu pia kwa sababu kwenye angalau matukio mawili ya Korani kwa hakika yanaonya na kuwatisha watu ambao wanakataa na hawaamini “Ishara” ya Allah.” **Q. 3:4** inasema, “*Hakika wale waliozikufuru Aya za Mwenyezi Mungu wana adhabu kali; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kisasi.*” **Q. 7:36** anaongeza, “*Na wale wanaokadhibisha Ishara Zetu na kuzifanyia kiburi hao ndio watu wa Motoni, watakaa humo (milele).*” Kwenye mwanga wa **Q. 3:50, 55** ambayo inasema kuhusiana na kumtii Yesu na kutuonyesha kwamba Yesu anajua na ni njia ya Mbinguni (angalia hapo juu), **Q. 19:21** ni daraja zuri la kujadili upekee wa Yesu Kristo. Pia ni daraja zuri la kuwafikia Uislamu kuisoma Injili na kujifunza Zaidi kumhusu Yesu.

4. Kujifunza kwa Manabii. Kwenye “Mwongozo wa Uislamu kwenye Biblia,” A. J. Hague anaeleza kwa kina juu ya kujifunza manabii, ikijumuisha mada kuu ya kila nabii alivyotajwa Kikorani na Kibiblia (Hague 2013: 25-27; angalia pia “Utafiti wa Ishara” n.d.). Huu ni ufupisho wa mada kuu na dondoo za rejea:

ADAMU	NUHU	IBRAHIMU	MUSA
Mungu alitoa kutufunika dhambi na aibu zetu	Tunapaswa kuukubali utoaji wa Mungu	Mungu alitoa sadaka	Tunapaswa kuitumia damu ya sadaka ya mwanakondoo
Q. 7:11-27; Mwanzo 3 (hasa. 15 & 21)	Q. 11:25-49; 36:41; Mwanzo 6:6-8-20; 9:12-17	Q. 37:83-113 (hasa. 107); Mwanzo 15:1-6, 8-10, 17-18; Warumi 4:1-22; Wagal 3:8-9	Q. 7:103-37; Kut 4:21-23; 12: 1-14; 21-30, 38
DAUDI	YONA	YOHANA (YAHYA)	YESU (ISA)
Uzao wake utakuwa sadaka ya mateso	Kwenye kina kwa siku tatu kasha kuwa hai tena	Yesu ni Neno na mwanakondoo wa Mungu	Sadaka teule ya Mungu
Q. 4:163; 17:55; 34:10; 2 Sam 7:8-15; Zab 2, 22; 45:6-7; 110:1; Math 1:1; Marko 10:46-52	Q. 10:94-98; 37: 139-48; Math 12:38-42	Q. 3:38-45; 19:7-15; Luka 1:5-25, 57-80; 3:4-6; Yohana 1:29-34 (hasa. 29)	Q. 3:42-55; 19:19-21; 21:91; 43:61-63; Math 1:18-21; 24:14; Yohana 1:29-34; 4:41-42; 14:6; 18:36-37; Matendo 10:34-43; 2 Wakor 5:18-21; 2 Pet 1:19-21

- *Adamu*: Baada ya kutokumtii Mungu Adamu alimlilia Mungu kwa Rehema zake. Mungu alimjibu kwa kupatia vazi la haki lililotokana na sadaka ya mnyama. Kwa njia iyo hiyo ipo ahadi ya sadaka kubwa baadaye kwa ajili ya wanadamu wote.
- *Nuhu*: Kama vile waamini wa kweli walipata safina na kuwaokoa kutokana na hasira ya Mungu, waamini wa kweli wataikubali sadaka kuu itakapokuja.
- *Ibrahim*: Alipoambiwa amtoe mwanae Ibrahim alitii, lakini Mungu alimsimamisha kwenye dakika za mwisho na kutoa sadaka ya mnyama. Kwa njia iyo hiyo Mungu ndiye atakayetoa sadaka kuu ijayo.
- *Musa*: Jamii yote ya Israeli ilitakiwa kuchukua damu ya mwanakondoo mkamilifu na kuipaka kwenye miimo ya milango ya nyumba zao ili kuwalinda na malaika wa uangamizi.
- *Daudi*: Kwenye zaburi Daudi anaeleza kwamba sadaka iliyo kuu itatoka kwenye uzao wake na itapitia mateso makubwa. Unabii mwingine unasema kwamba sadaka hii itafanyika kama Rehema kwa niaba ya watu wengine.
- *Yona*: Yona alimkimbia Mungu na hivyo Bwana akamhifadhi kwenye samaki kwa siku tatu usiku na mchana. Alifufuliwa na kutumika kuona idadi kubwa ya watu wakifunguliwa kutoka dhambini. Yesu alisema ishara ya mwisho atakayotoa “ni ishara ya Yona.”
- *Yohana Mbatizaji*: Aliitwa nabii Mtakatifu kutoka kabla hajazaliwa, alilishuhudia Neno kutoka kwa Mungu (i.e., Yesu), na alimtambulisha Yesu kama Mwanakondoo wa Mungu ambaye atazichukua dhambi za ulimwengu.

²⁴ Anuani zake za kwenye mtandao zipo kwenye orodha ya vyanzo ili kwamba waweze kuzifikia.

- *Yesu*: Vitabu vyote vitakatifu vinakubali kwamba mwanadamu ametembea nje ya Njia ya Mungu iliyo sawa na anahitaji Rehema zake. Vinakubali pia kwamba Yesu ni Masihi wa Mungu asiye na hatia aliyekuja kama Neno na Rehema kutoka kwa Mungu. Kwa kuwa sadaka iliyo kuu kwa niaba yetu, Yesu alizidhihirisha Rehema za Mungu na kumwonyesha mwanadamu jinsi ya kurudi kwenye njia iliyo sawa.

Ikiwa Mohamedi alilijua hili, akasisitiza kwamba aliyakiri mapungufu yake na kutambua kwamba hakuwa njia ya Wokovu (**Q. 46:9**) lakini alirudi nyuma kwa Yesu kama Masihi asiye na waa ambaye yuko hai mbinguni sasa.

C. *Tamaduni za Uislamu kama daraja: mpango wa wokovu wa Qurban*

Mbinu hii ya kujengea daraja Uislamu na Injili imejengwa kwenye sherehe za Kiislamu ya Eid u'l-Adha (“Sherehe kuu” au “Sherehe ya kuchinja sadaka”) ambayo hukumbuka tendo la sadaka (*qurban*, wakati mwingine hutamkwa *qurbani*, *korban*, au *korbani*) ambayo kwayo Ibrahim alikuwa ameandaa kumtoa sadaka mwanae lakini Allah alimhifadhi kijana kwa kumpatia mwanakondoo kutolewa badala yake. Maelezo hayo yapo kwenye **Q. 37:100-111**. Kwa mbinu hii nadhani kwamba Muislamu unayezungumza naye ana nia ya kumjua Yesu (i.e., njia ilikuwa imeshaandaliwa na mbinu ya (NGAMIA) CAMEL au vinginevyo) na anayo nia ya kumpokea Yesu. Mbinu imeelezwa kwenye Greeson na Owen 2005: 25-26 (na penginepo tofauti na Greeson 2007: 113-20). Yaliyo ya muhimu kwenye mbinu hii ni kama ifuatavyo:

1. Abrahamu alitoa sadaka (*qurban*). Maswali pendekezwa:

- *Unaijua hadithi ya Abrahamu wakati alipoambiwa kutoa sadaka ya qurban na mwanae? Abrahamu alifanya nini?* (Jibu: Abrahamu alimchukua mwanae na kumtoa kama sadaka.)
- *Mungu alifanya nini dakika za mwisho?* (Jibu: Alimtuma malaika kusimamisha sadaka na, kulingana na Biblia na desturi za Kiislamu, alitoa mwanakondoo kama sadaka.)
- *Ni jaribu gani Mungu alilompa Abrahamu?* (Jibu: Kuona ni jinsi gani Abrahamu anavyompenda.)

2. Maana ya qurban. Maswali pendekezwa na maoni:

- *Kulikuwa na maana gani nyuma ya uzoefu wa qurban?*
- Baada ya kupewa jibu lake, “*Nimejifunza Torati na Injili na nimekuja kujua qurban halisi ninini na jinsi gani inavyotakiwa kufanyika.*” Kisha elezea:
 - a. Mnyama wa *qurban* ni lazima awe msafi na asiye na waa. Mnyama aliwakilisha kisichokuwa na hatia. Hapaswi kununuliwa kwa pesa ya rushwa au iliyotokana na biashara isiyo halali.
 - b. Tendo la *qurban* ni picha ya mmoja asiye na hatia kuchukua adhabu ya mtu mwenye hatia. Dawuud (David) alisema kwamba *qurban* iliyo bora ni ile ambayo huchukua nafasi ndani ya mtu (**Zab 51:16-17**). Kuzijutia dhambi zako ni dhabihu iliyo bora (*qurban*.)
 - c. Tendo la dhabihu (*qurban*) ni ishara ya adhabu ambayo tuliistahili kwa dhambi zetu.
- *Je hili linasikika kwako kama maombi sahihi ya dhabihu (*qurban*)?* Kisha sema, “Wakati tunapomwekea mnyama mikono, tunapaswa kusema, ‘Allah, Ninajua kwamba mimi ni mwenye dhambi na kwamba adhabu inayonstahili ni kifo kwangu. Pokea damu ya mnyama huyu kama mbadala kwa adhabu yangu na nisamehe mimi na dhambi za familia yangu.’”

3. Yesu—(*qurban*) dhabihu kwa ulimwengu wote. Maswali pendekezwa na maoni:

- Korani inalisema hili kuhusu Yesu kwenye Sura Maryam (**Q. 19:33**): “*Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa kuwa hai (tena).*” Maelezo: Baada ya Yesu kufa, Wafuasi wake waliacha kutoa sadaka ya mnyama. Kwa nini hili lilikuwa hivyo? Kabla ya kufa kwa Yesu, aliwaeleza wafuasi wake kwamba Mungu aliamua kufanya sadaka (*qurban*) kwa dhambi za ulimwengu wote, hili linaonyeha upendo Wake kwa wanadamu wote. Kama vile Mungu alivyotoa sadaka kwa Abrahamu, Yeye pekee atatoa sadaka kwa ajili ya wanadamu wote. Mungu alimsimamisha Abrahamu kumtoa mwanae, lakini Mungu hakuismamisha sadaka ya Yesu.
- *Kwanini Mungu alifanya hivyo?* Jibu: La muhimu Zaidi ni ukweli kwamba hakuna mtu anayeweza kufanya sadaka ya kutosha (*qurban*) kuzifunika dhambi zake. Kufanya sadaka (*qurban*) kufunika dhambi za ulimwengu wote, ni yule aliye mtakatifu sana, asiye na hatia, na sadaka ya mwenye haki inayoweza. Hivyo Mungu aliamua kumdhambihu yule asiye na hatia, mtakatifu, na damu yenye nguvu ambayo ulimwengu huu utaiona milele. Tunaona kwenye **Q. 3:42-55** kwamba Yesu alizaliwa na Bikira, alitoka mbinguni, hakutenda dhambi, alikuwa mtakatifu mkamilifu, asiye na hatia, na mwenye haki, na aliyerudi mbinguni. Yesu pekee ndiye anayestahili maelezo ya sadaka iliyo kamilifu (*qurban*) ambaye alikufa kwa dhambi za ulimwengu wote. Hili linadhahirisha upendo wa Allah na Yesu kwetu sisi.
- Unaweza kulihamishia kwenye Biblia, kwa mfano, **Yohana 1:29** pale nabii Yahya (Yohana Mbatizaji) aliposema kwa Yesu, “*Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!*” Kwa maneno mengine, Allah alizihamisha dhambi zetu kwenda kwa Yesu ambaye hatimaye alilipa kwa ajili ya dhambi

zetu dhabihu ya maisha yake mwenyewe kwa ajili yetu.

- *Tunajuaje kwamba Allah aliikubali sadaka ya Yesu (qurban) kuzifunika dhambi za watu? Jibu: Mungu alikubali kwamba amepokea sadaka ya Yesu kwa kumfufua kutoka kwa wafu (angalia **Luka 24:17-27; Matendo 2:29-36; 17:31; Warumi 1:1-6; 1 Wakor 15:1-4**).*

4. Uzima wa milele kupitia Imani kwa Yesu. Yapo mambo manne ambayo Uislamu wanapaswa kuyajua:

- *Kwanza, tumetenda dhambi na hatuwezi kufanya vya kutosha kuzifunika dhambi zetu. Dhambi moja ilimwondoa Adamu kwenye uwepo wa Allah bustanini mwa Edeni. Tumetenda dhambi mara nyingi (angalia **Warumi 3:10-12, 23**).*
- *Pili, Yesu alizaliwa bila dhambi na kamwe hakutenda dhambi. Yeye ni Roho kutoka kwa Mungu (“Ruhullah”), **Q. 4:171** na “*Kalamtullah*” (Neno la Mungu, **Q. 3:45**). Damu yake haina hatia kwa sababu hakurithi dhambi ya Adamu au kutenda dhambi yeyote akiwa hai. Damu yake ni takatifu na yenye nguvu. Allah alimwuliza Ibrahimu kuonyesha upendo wake kwa Allah kwa kumdhabihu mwanae wa thamani. Kwa njia iyo hiyo, kuonyesha upendo wake kwetu, Allah aliamua kutoa dhabihu (*qurban*) kwa wanadamu wote kwa kumdhabihu Yesu (angalia **Warumi 5:6-8; 2 Wakor 5:21; Waeb 4:15; 1 Pet 2:22; 1 Yohana 3:5**).*
- *Tatu, Yesu alikufa msalabani kama qurban kwa dhambi zetu. Injili inatambua, “Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu” (**1 Pet 3:18**).*
- *Nne, kama ukimwamini Yesu—ambaye alikuwa na Mungu mbinguni lakini alikuja duniani kama mwanadamu kuishi maisha tuliyopaswa kuyaishi na kufa kifo tulichopaswa kufa, kuchukua dhambizetu na adhabu tuliyostahili juu yake mwenyewe—utasamehewa dhambi zako na kuupata uzima wa milele. Injili inasema, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” (**Yohana 3:16**). Kupitia Yesu tunaweza kwenda mbinguni wakati tutakapokufa na kuishi milele pamoja na Allah. Yesu anajua njia na ni njia. Kama kweli unaamini kwamba Allah alitoa *qurban* kwa kutumia damu ya Yesu kufunika dhambi zako, unaweza kuungana na Yesu mbinguni. Hii ndiyo sababu **Warumi 10:9-10** inasema, “Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu”*

D. Tamaduni za Uislamu kama daraja: upeo mwingine wa mawasiliano

Vigezo vingine vya Kiislamu na uzoefu wa tamaduni zinazoweza kutenda kama daraja ni hivi vifuatavyo:

1. Uzoefu wa *aqiqah*. Uislamu wanayo ibada iitwayo *aqiqah* ambayo mnyama hutolewa sadaka kwa niaba ya mtoto mchanga aliyezaliwa. *Aqiqah* ni sawa na *qurban* itumikayo kwenye sherehe ya Kiislamu ya Eid u'l-Adha (“Sherehe kuu au Sherehe ya kuchinja sadaka”). Hili, linaibua suala la fidia mbadala ya Kristo. Masuala na maswali kama hayo yaliinuka kwenye (*Qurban*) mpango wa Wokovu kwa hiyo yanaweza kutumika.

2. Jitihada za baraka. *Baraka* ni neno la Kiarabu, na “wazo la Baraka ni moja ya kiini cha watu kwa ujumla wa mazingira ya Kiislamu ya Afrika” (Howell 2015: 44; angalia pia Pennington 2014: 196 [Uhuishaji wa Uislamu wa Asia ya kusini]). Kwenye uhuishaji wa uislamu kwa ujumla, msukumo wa kujizoeshia “nguzo tano” za Uislamu ni ili “kupata” *baraka*, nguvu ya kiroho isiyo ya kawaida ambayo wakati inapohifadhiwa, humsaidia mtu kuwa na nguvu ya maisha” (Van Rheenen 1991: 60). Hatimaye, baraka zinazotafutwa ni kwa ajili ya mafanikio, uzalishaji, na ambazo msukumo wake mkubwa ni kwenye uchoyo na wivu, na kuelekea kuweka mbali uovu, kunakosukumwa Zaidi na hofu (Howell 2015: 44-46). Uislamu wengi wa kawaida hutafuta uponyaji wa asili, waganga wa kienyeji/wachawi, kupiga ramli, na ushirikina kwa ajili ya baraka (Ibid.: 45-46).

Kanisa linaweza kutumia wazo hili na kuwa wakala wa baraka za kweli na za kudumu za Kiroho na kimwili ambazo watu kwa hakika huzitafuta. Richard Love anaeleza kwamba kwenye mazingira ya Uislamu wa kawaida, mambo matatu yanahitajika: “kukutana na nguvu, kukutana na kweli na kukutana na tamaduni. Zenye msingi wa ufalme wa Mungu, tunakabilia na nguvu za giza kupitia uovu na uponyaji (kukutana na nguvu), kuhubiri habari njema kwamba Yesu alikuja kuzivunja kazi za shetani (kukutana na kweli), na kuelezea ukweli wa ufalme kupitia tamaduni na mila husika (kukutana na tamaduni).” (Love 1994: 87) Alan Howell anapendekeza msingi wa daraja la *Baraka* kwamba mchakato wa jumla, ikijumuisha kuwafundisha watu kuona faida ya muda mfupi na ubatili wa wakati wote wa kuzoelea ushirikina unaofanywa kwa kutafuta Baraka na utofauti ambao ni pamoja na Baraka za kudumu zipatikanazo kwenye ufalme wa Mungu. Viongozi wa Kikristo wanapaswa kuacha kujiona kama wachungaji wa Kimagharibi na kufanya Zaidi kama watu watakatifu wa zamani, kwa kutokuzikaribisha Baraka zao wenyewe lakini kuwasaidia viungo wote wa mwili wa Kristo kuishi vizuri na maisha yenye mafanikio. Ibada za ukombozi zinaweza kuwasaidia waamini kuyaachilia mbali mazoea yao ya kichawi, na “wakati wa mazishi ni muhimu kwa kuonyesha kwamba Kanisa au jamii ya waaminio ni mawakala wa Baraka ambazo kwa upendo huwajali Yatima na Wajane” (Howell 2015: 50).

3. Uhuru wa kutoka kwenye unajisi. Chini ya mtazamo wa ulimwengu wa Uislamu, “hitaji kubwa la kihisia siyo wokovu kutoka dhambini lakini ni ukombozi kutokana na unajisi. Kila kipengele cha maisha ya muumini wa Kiislamu, kimeamuriwa na hali ya kutokuwa salama; mwelekeo wa kuangalia wakati unapokuwa umelala, maneno ya Kiarabu ambayo yanaitangulia kazi, Matamshi, au salaam, na hata namna ya kupiga chafya au kujamba. . . . Unajisi huja kwa viwango tofauti. Kila unajisi una mila inayokubalika kwa ajili ya utakaso.” (Sidebotham 2002: 4) Yesu alienda hadi kwenye kiini cha jambo—kwamba wanadamu wenyewe wote siyo safi na wamenajisika—wakati aliposema, “*Hakuna kitu kilicho nje ya mtu ambacho kikimwingia chaweza kumtia unajisi, bali vile vimtokavyo, ndivyo vimtiavyo unajisi yule mtu.*” (**Marko 7:15**). Wazo la unajisi hivyo hufanya wazo la mwanadamu kurithi uovu na uharibifu kueleweka kwa Uislamu: “Wazo la asili ya unajisi husaidia kuwepo kwa uharibifu wote. ‘Hakuna mwenye haki hata mmoja, la hata mmoja’ (Warumi 3:10) na ‘matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi’ (Isaya 64:6), kwa sababu tumenajisika. Dhambi haikurithiwa lakini imechipuka kutoka kwenye asili yetu. Sisi ni najisi na kila tunachokishika au kufanya, hata kwa kusudi jema, huchafuka. Uislamu wanaolewa kwamba ardhi imelaaniwa popote atakapokanyaga kama hajaoga baada ya kufanya ngono anajiona jinsi alivyo kwenye utumwa kwa kutokuwa na haki kunakotokana na kunajisika kwake. Hili linaweza kueleza kwanini Uislamu hung’ang’ana sana kuwa wasafi kuliko kung’ang’ana kuwa na haki.” (Ibid.: 5)

Hili, kwa namna nyingine, husaidia kufanya upatanisho kueleweka zaidi. **Waeb 12:2** inatuambia kwamba Yesu ni “*mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.*” (angalia pia **Isa 53:4-5**). Kwa maneno mengine, “Yesu hakuibeba dhambi tu; aliibeba aibu yetu” (Ibid.). *Alifanywa dhambi kwa ajili yetu “Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye” (2 Wakor 5:21).* Au, kama Petro na Paulo wote walivyosema, “*Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika*” (**1 Pet 2:6**; angalia pia **Warumi 9:33**). Msalabani kwa kufufuka kwake Yesu alishinda na kuangamiza moja ya matokeo mabaya ya unajisi wetu, ambao ni, kifo chenyewe. Tumaini letu pekee limeegemea kwa Yesu ambaye ametutakasa mara moja na kwa wakati wote kutokana na unajisi na kifo chetu wenyewe kwa Imani ndani yake Yeye—na ubatizo ni ishara ya kuonekana kwa nje kwa kukubalika huku: ni ukamilifu wa uchafuzi wa mwisho ambao unahitimisha kutokukamilika kote na utakaso wa muda ambao mila za Kiislamu zinadokeza tu.

Sidebotham anatupa mfano wa jinsi alivyotumia uelewa huu kuanza kuwasilisha Injili kwa Uislamu: “Huko Indonesia rafiki yangu mmoja aliniuliza kwanini Wakristo wanasisitiza kwamba Yesu ni Mungu na kwamba alisulubiwa. Badala ya kujaribu kumshawishi rafiki yangu kwamba wote wametenda dhambi na kila dhambi ni lazima ihukumiwe kwa kifo, niligundua kile ambacho tayari alikijua, kwamba miili yote imenajisika na kabla ya kuzaliwa ilikuwa na chembechembe zote ambazo kutokana na hizo ilihitaji kutakaswa. Nilieleza mawazo yangu kwenye ubatili wa mila za sherehe za kutufanya sisi kuwa safi vya kutosha ili kuingia mbinguni, kwa sababu uchafu hauwezi kujisafisha wenyewe kuwa bora na giza haliwezi kujifanya lenyewe kuwa mwanga. Nilisema kwamba kama vile ambavyo msumaa hufukuza giza chumbani mara unapoingia humo, Mungu aliufukuza unajisi kutoka kwenye mwili wa mwanadamu kwa kuwa mwili. Kwa maneno mengine, vitu vile ambavyo Uislamu hudai zaidi kwenye Ukristo,—kujitambulisha kwa Mungu na Uumbaji wake, ni suluhisho kwa matatizo mengi ya msingi ya mwanadamu kama yanavyotazamwa na Uislamu wengi.” (Sidebotham 2002: 4; angalia pia Hayes 2015: 29-31, ambaye “humtia aibu anayeheshimiwa” msingi wa kuwasilisha Injili kwa Uislamu)

Mtiririko wa matokeo Fulani huonekana kutokana na kile Kristo alichokifanya kutuweka huru kutokana na unajisi. Kwa mfano, Uislamu husimamia kwenye wazo kwamba Wakristo husema kwamba Yesu ni Mungu katika mwili. Bado, kwa kutumia wazo la unajisi, Muujiza wa “Asili ya Yesu” – kumponya kipofu kwa kumtemea mate na mkoma kwa kumgusa kwake – vinathibitisha kwamba alikuwa Mungu. Hakuna nabii wa kawaida ambaye angemshika mwenye ukoma na asinajisike, na wakati kaburi la nabii lazima liwe takatifu mate yake hubaki machafu kama ya mtu mwingine yeyote.” (Sidebotham 2002: 4). Bado Yesu (na mate yake) alibaki msafi na Mtakatifu (angalia **Q. 19:19**)—linalomaanisha kwamba hawezi kuwa ni mtu wa kawaida. Vivyo hivyo, Uislamu wanakwazika kwa kula nyama ya nguruwe kwa sababu inawakilisha unajisi mkubwa. Hata hivyo, Wakristo wako huru kula kile wanachokitaka. Kwa nini? Sidebotham anaeleza, “Wakati Yesu alipotangaza “vyakula vyote kuwa safi”” (Marko 7:18-23), alikuwa anamaanisha kwamba suala la usafi lilikuwa ni hali ya msingi kwa mwanadamu na siyo kwenye chakula” (Ibid.: 5). Sheria ya chakula imeonyesha hali ya uchafu wa mwanadamu kama vile ambavyo sadaka ilionyesha dhambi ya mwanadamu. Sasa, hatufungwi tena na sheria hizo kwa sababu Yesu aliundoa unajisi wetu kama vile alivyoziundoa dhambi zetu; Kwa sababu Yeye (ambaye ni msafi na asiyenajisika [**Q. 19:19**]) yupo ndani yetu, tunabaki kuwa wasionajisika bila kujali

tumekula nini (**Marko 7:15**). Warick Farrah aliliweka hili hivi, “Kupitia Imani tunaungana na utukufu wa masihi kwenye maisha yake, kifo, na kufufuka kwake. Hupata uaminifu wetu (sifa, utukufu, na heshima) na tunapata maisha yake ndani yetu, kuziondoa aibu na unajisi wetu.” (Farrah 2013: 17-18)

4. Mtazamo wa mteja-msimamizi wa Injili. Uislamu wengi wametoka kwenye jamii na tamaduni ambazo zinasisitiza uanachama kwenye kikundi, Vyeo, uhusika binafsi, na uongozi (ikipingana na ubinafsi na usawa wa Kimagharibi). Kwenye tamaduni hizo, “Kiongozi anayeniwakilisha mimi ni yule ambaye tunahusiana” (Edwards 2013: 81). Kiongozi hufanya kama msimamizi ambaye husambaza mahitaji kwa rasilimali, wakati ambapo mteja hufanya kwa uaminifu kwa viongozi. Kwa lugha ya Kiroho, Uislamu wengi wanao mtazamo kwamba, bila kujali mawazo ya Uislamu kwamba watu watahukumiwa kwa umadhubuti kulingana na uzito wa matendo yao mema dhidi ya matendo mabaya, wataokolewa kwa sababu Mohamedi ni msimamizi wao; wanautazama “Muunganiko wao kwenye kundi la Mohamedi kunamaanisha wokovu” (Ibid.: 84)

Lakini Yesu ni mwenye nguvu kuliko mwingine yeyote, ikiwa ni pamoja na Mohamedi: “Hatua ya kwanza ni tukio ambalo litavuta hisia zao kwa Yesu Masihi. Hatua ya pili ni kuchunguza Yeye ni nani, kwa kawaida kuangalia kwenye Korani. . . . Kama wanavyoendelea kwenye vyanzo vingine e.g. *Injili*, wanaona Yeye ni mwumbaji, mwanga, mwenye nguvu, nk. Kutafuta kwao kwenye *Injili* kimsingi kunategemea uelewa wao. Wanaikuta nafasi ya Yesu (*Isa*) ni ya juu kimamlaka kuliko ambavyo kwa asili walikuwa wamefundishwa. . . . Hakika lile swali halisi waliloanza kuuliza ni lile linalohusiana na hali ya mahusiano yake na heshima kwa nabii Mohamedi. Kwa jinsi ambavyo vyeo vilivyopangwa vizuri, viongozi wawili ni mmoja pia wengi; hawawezi kuwa sawa kwenye nafasi ya juu hivyo swali linaibuka kama ni nani aliye wa muhimu zaidi. . . . Wale ambao wameuweka uaminifu na imani yao kwa *Yesu* hutatua balaa hilo kwa kuamua ni Yeye ambaye anayo heshima ya juu zaidi. Nafasi hii ya thamani kisha humaanisha wanaungana pamoja naye kama kiongozi na msimamizi.” (Ibid.: 84-85).

5. Hadithi. Dr. Edward Hoskins aliandika kwamba, Kwa Uislamu, majibu kwa maswali mengi ya maisha “hayawezi kwa kawaida kupatikana kama inavyodhaniwa, kimsingi kwenye Korani. Kwa hakika, mengi yake hayapatikani kabisa kwenye Korani.” (Hoskins 2011b: 93) Hata hivyo, “Uislamu wanaamini kwamba Allah, kupitia manabii wake, hutoa kwa kila hali. . . . Kama Korani ni mifupa, basi Mohamedi ni nyama kwenye mifupa hiyo, ambayo huwaweka Uislamu wote kwenye vitendo.” (Ibid.: 96). Hoskins anaandika, “Kutumia utamaduni wa hadithi kujenga mahusiano ya haraka. Kwanini? Kwa sababu ni za karibu na za kupendwa kwenye moyo wa kila Muislamu niliyekutana naye.” (Ibid.: 104-05) Kwa Hoskins kujifunza Hadithi wakati wote amekuweka mbele kwenye kitabu chake kiitwacho, *Ufahamu wa Uislamu: Kile ambacho kila Mkristo anachopaswa kujua kuhusiana na utamaduni wa Kiislamu* (Hoskins 2011a) na kufupishwa kwenye Makala yake (Hoskins 2011b).

Mbinu ya Hoskins ni, “Ninapozungumza na rafiki Muislamu kuhusiana na Hadithi, hupenda kuchukua pamoja na kijitabu kidogo ambacho nimeandika baadhi ya tamaduni za Kiislamu ambazo nimezikusanya. Ninakuwa na hadithi moja au mbili zilizochapwa kwenye kila ukurasa zikiunganishwa na mistari ya Biblia ile niliyoiona inafanana. . . . Ninaivuta moja ninapokuwa nimekaa na rafiki yangu na kumwachia asome tamaduni zilizoambatana na aya za Biblia. Baada ya hapo ninauliza maswali machache. Moja au mawili kwa kawaida yanatosha. Hapa kuna maswali machache niliyoyaona yanafaa Zaidi kuulizwa:

- Ulizisikiaje hizi tamaduni kabla au kitu kinachofanana na hicho?
- Ni jinsi gani hadithi hizi zimeyagusa maisha yako wewe kama Muislamu?
- Hadithi hizi zinakueleza nini kuhusiana na tabia ya Mungu?
- Zinasema nini kuhusiana na hali ya mwanadamu?
- Zinapendekeza uwezekano wa njia ya kujenga daraja la mahusiano baina ya hawa wawili?
- Unaweza kuikumbuka hadithi hiyo mahali ulipoiona simulizi hiyo, ama ukiwa mtoto au mtu mzima?

Ninapomaliza wakati wote huuliza kama analo swali lolote wanalotaka la kuniuliza. Maswali haya mara nyingi huzalisha majadiliano yenye kuzaa matunda.” (Ibid.: 105) Aliendelea kutoa baadhi ya mifano ya jinsi alivyo zitumia hadithi na mistari ya Biblia ili kuisitiza ukweli wa Kibiblia.

Hoskins anaona, “Kwa Uislamu, Hadithi ni simulizi zilizo zoeleka ambazo hubeba mafafanuzi na majukumu ya kila siku ya maisha ya kiutendaji. Kufanya haya yatumike, tunalo daraja ambalo hufanya mazungumzo ya kiroho kuwa wazi na ya kueleweka. . . . Wakati nilipokuwa ninajifunza hadithi, Niligundua nyingi zenye umuhimu unaofanana na Biblia yetu wenyewe. Hadithi ni msongamano wa mada kama vile ‘kanuni ya dhahabu,’ ‘thibiti hasira yako,’ ‘Mungu huutazama moyo,’ ‘Heri wenye Rehema,’ ‘kuwalisha wenye njaa,’ na nyingine nyingi.” (Ibid.: 108, 109) Alihitimisha na tahadhari mbili: (1) “Hadithi nyingi huonyesha Uislamu na nabii wao kuwa kwenye hali ya mahusiano dhaifu. . . . Wakati utakapofikia hayo, tafadhali, tafadhali usizitumie kama silaha kuwapiga Uislamu. Bila shaka ni za thamani kubwa kwa ajili ya kukuongezea

ufahamu binafsi, lakini nimeziona zikiutumia sana hisia za marafiki zangu na kwa ujumla hazina matunda ukizitumia.” (Ibid.: 109) (2) “Kwenye kusudio letu la kutafuta umoja na uhusiano na marafiki zetu Uislamu tunaweza kuhitimisha kwa kuachilia kile kilicho cha thamani Zaidi kwetu – Kiini cha mwanadamu na kazi ya Kristo” (Ibid.). Hivyo, wakati hadithi zikitumika kama daraja, ni lazima wakati wote kuliweka akilini kwamba ni daraja kwa *Kristo na Injili*.

E. *Kushughulikia maswali na makatazo*

Uislamu wanaweza kuibua vikwazo au maswali mbalimbali. Bila shaka vile vikwazo vilivyo vya kawaida ni hivi vitfuatavyo:

1. Biblia hajaminiki. Hili limejadiliwa kwa kina kwenye kipengele cha **5.II. Maendeleo ya Biblia, 5.III. Mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia, na 5.IV. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Biblia**. Shane Bennett anapendekeza majibu mafupi juu ya mjadala huu: “Hakubaliani kwamba Mungu anazo nguvu za kutosha kulilinda neno lake? Ni nani mwenye nguvu za kutosha kuliharibu neno lake, na lini watafanya hivyo?” Baada ya kuvuta pumzi, kisha uliza ‘Unaonaje kama tukivisoma vitabu vitakatifu pamoja nami tuweze kuona halisi kile vinachokisema?’” (Bennett 2013: n.p.)²⁵

2. Yesu hakufa Msalabani. **Q. 4:157** anasisitiza, “*Na kusema kwao (kwa kujivuna): Hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumwua.*” Hili lilijadiliwa kwa kina kwenye kipengele cha **2.IV. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Kusulubiwa**. Korani inasema kwamba manabii wengi waliuawa (**Q. 2:2:87; 3:21, 183; 4:155**). Hivyo, Majibu mafupi ya Shane Bennett kwa mjadala huu ni: “Unaweza kufikiri, ni jinsi gani Mungu angemruhusu nabii wake ashindwe kwa kufa msalabani. Ngoja nikuulize swali, ‘Lililo kuu ni lipi, kwa Mungu kumwokoia nabii wake kwa kumhifadhi kutokana na kifo au kumwokoia kwa kumfufua tena na kukishinda kifo?’” (Bennett 2013: n.p.)

3. Yesu siyo Mungu na wala siyo Mwana wa Mungu. Hili limejadiliwa sana kwenye kipengele cha **2.VI. Majibu kwa mtazamo wa Kiislamu juu ya Yesu: Yesu ni “Mwana wa Mungu” na 2.VII. Matokeo ya ukweli kwamba Yesu Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili**. Majibu mafupi ya Shane Bennett kwa mgongano huu ni: “Ndiyo [tunaamini kwamba Yesu ni mwana wa Mungu], lakini bila shaka siyo kwa njia ambayo ninyi mnaifikiria. Wakristo wanaamini kuwa kutungwa mimba ya Yesu kulitokea kwa muujiza wa Roho Mtakatifu. Unaamini kwamba Mungu anaweza kujinajisi mwenyewe kwa kuwa na mahusiano ya kimwili na mwanamke, unaweza wewe kuamini hivyo?” (Bennett 2013: n.p.)

4. Wakristo huabudu miungu watatu. Hili limejadiliwa kwa kirefu kwenyekipengele cha **4.IV. Utatu**. Majibu mafupi ya Shane Bennett juu ya madai haya ni: “Unamfikiria Mungu, Yesu na Mariamu? Mbali sana kutoka hapo. Tunamwabudu Mungu mmoja, aliyejifunua kwenye Utatu, Baba, Mwana au Neno, na Roho. Ngoja nikuulize swali, ‘Ni kipi kulitangulia kuwepo kwanza kwenye Umilele: Mungu au Neno lake, au Roho wake?’” (Bennett 2013: n.p.)

5. Wewe unasemaje kuhusu Mohamedi? Haitakuwa busara kumshambulia Mohamedi wakati utakapoulizwa kumhusu kuwa mwangalifu kuwauliza Uislamu kwa sababu hilo linaweza kuwa kikwazo kikubwa na bila shaka kuhitimisha fursa yoyote ile ya kuendelea na majadiliano.

- Mtu anaweza kusisitiza kwamba “Mohamedi alikuwa kiongozi mkuu wa nchi na muasisi wa dini, kuwaleta Waarabu kutoka kwenye kuabudu miungu wengi wa Kipagani hadi kwenye dini ya Mungu mmoja wa Ibrahimu [na] Mohamedi alimzungumzia *Yesu* Masihi (kuzaliwa kwake na bikira, miujiza na kutokutenda dhambi) na kutambua kwamba *Torati, Zaburi* na *Injili* ni Neno la Mungu na ni lazima liheshimiwe” (Travis 2000: 56).

- Itakuwa vizuri pia tukiyaangalia yale ambayo Mohamedi aliyazungumza kumhusu yeye mwenyewe, hasa kwenye **Q. 46:9** aliposema, “*Mimi si mpya katika Mitume, wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa ninyi. Sifuati ila yaliyofunuliwa kwangu; na mimi siye ila ni Mwonyaji dhahiri.*”

Hili linatengeneza daraja la kumwuliza Muislamu mambo yote aliyoyafanya kujaribu kufika mbinguni (kuzifanyia kazi “nguzo tano,” kutii sheria). Mtu anaweza kuuliza, *Zipo sheria ngapi hapo? Ni ngapi kati ya hizo unazoweza kuzitii mfululizo na kwa uhakika muda wote (50%? 90%?)? Kisha uliza, Hivyo ni kwa jinsi gani unajua kwamba utaenda mbinguni?* (Atakujibu kwamba hawezi kujua; kile atakachokifanya ni kufanya

²⁵ “Baadhi ya Waislamu wanaweza kuchanganywa na tafsiri mbali mbali za Maandiko. Mabadiliko ya lugha, na matoleo mbali mbali yaliyochapishwa ili kuifanya Biblia Takatifu kuwa rahisi kusomeka na kueleweka. Tunaweza kuonyesha kwamba matoleo mengi ya Korani yametafsiriwa kwa Kiingereza [na kwa lugha nyingine] na Wanazuoni mbali mbali, kama vile Pickthall, Yusuf Ali, Mohamedi Ali, na Dawood. Kila mmoja alitafuta kuwa mkweli kwenye maana ya asili.” (Goldmann 2004: 147)

kwa ubora awezao, lakini Allah analo neno la mwisho.)

Hilo litajenga daraja la kuuliza, *Ungependa kujua Biblia inasema nini kuhusu jinsi ya kupokea msamaha kutoka dhambini na kile kitakachokupa sifa za kuingia kwenye uwepo wa Mungu mbinguni?*

Kama Muislamu atafunguka, unaweza kutofautiana na kile Mohamedi alichokisema kwenye **Q. 46:9** na kile Yesu alichokisema kwenye **Yohana 14:1-3, 6**. Unaweza kuielezea Injili.

IV. Kuunganisha mgawanyiko baina ya Uislamu na Injili: Hitimisho

Georges Houssney anasema, “Kwa Muislamu kukubali kutokuuliza swali kuhusu utambulisho wake labda kinaweza kuwa kikwazo kikubwa cha kuifikisha Injili kwake” (Houssney 2010: 83; angalia pia Morin 2007: 118-22; Greenlee 2013: 6). Utambulisho wa kitamaduni wa Uislamu una matokeo ya muhimu sana kwa kueneza Injili kwenye jamii ya Uislamu. Kwa sababu Uislamu ni sehemu ya utambulisho wa maisha yote ya kitamaduni—dini, jamii, tabia, familia nk.—tafiti nyingi zinaonyesha kwamba Injili imekuwa ikihubiriwa, makanisa kupandwa, na harakati zenye ufanisi hutokea kutoka kwa wale waamini wenyeji wenye asili ya Uislamu, Kimsingi kupitia *mitandao ya kijamii iliyopo* miongoni mwa (Waliokuwa) Uislamu wenyewe (Gray na Gray 2009a: 19-28; Gray na Gray 2009b: 63-73; Naja 2013b: 157 [“hasa, ingawa siyo sana, miongoni mwa wanafamilia”]; Naja 2013a: 28; Dutch 2000: 15-24; Greeson 2007: 38).

Kwa matokeo hayo, Wakristo wengi wanaofanyakazi miongoni mwa Uislamu huendelea kushirikisha Injili siyo tu kwa mtu mmoja mmoja lakini, kwa kiwango wawezacho, “Kwenye mazingira ya asili ya mtandao wa kijamii, kwa taratibu kuubadilisha mtandao kumwelekea Kristo, bila kujali kiwango cha Imani ya mwanachama wa mtandao” (Gray, et al. 2010: 89; angalia pia Greeson 2007: 34-40; Gray na Gray 2009b: 63-73; Adams, Allen, na Fish 2009: 78-80; Adams 2013: 23).

Ingawa idadi kubwa ya waamini wenye asili ya Uislamu hubakiza viashiria vingi vya kitamaduni vya kuwa “Uislamu” asilimia kubwa hukutana na mateso baada ya kuja kwa Kristo, ikiwa ni pamoja na kukataliwa, kuhofia mahusiano ya familia na jamii, kufungwa jela, kupigwa, tishio la kifo na mateso ya namna nyingine nyingi (angalia Naja 2013b: 157; Adams 2013: 23-24; Greeson 2007: 40-41; Gaudeul n.d.: 11; Greenham 2010: 152; Dunning 2013: 287-88; Abdulahugli 2005: 162-63). Cha kuhuzunisha ni kwamba, wengi wa hawa waamini wenye asili ya Uislamu pia hawakubaliwi wala kukaribishwa na Wakristo ambao hawana asili ya Uislamu kwa sababu tofauti ya tamaduni zao (Greenlee 2013: 6; Gaudeul n.d.: 11). Hili ni suala ambalo linaugusa moyo wa Kanisa. Kutokuwakumbatia waamini wenzetu kwa sababu ya tofauti za kitamaduni ni kinyume na Injili yenyewe (angalia **Wagal 2:11-21**). Kwa ukweli na ufanisi wa kujenga daraja lililotugawanya baina ya (Ukristo) Injili na Uislamu, wale wanao hubiri Injili ni lazima waiishi, hasa kwa kuyadhihirisha maneno ya Kristo mwenyewe “*Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi*” (**Yohana 13:35**).

NYONGEZA A—MPANGILIO WA KIJIOLOGIA WA SURU

Kumbuka: Jedwali hili limechukuliwa kutoka http://tanzil.net/wiki/Revelation_Order.

Maendelezo na tafsiri ya Kiingereza ya Suras yametoka kwa Ali, Yusuf. 2006. *Maana ya Korani tukufu*. Online: <http://www.unitedamericanmuslim.org/pdf/english-quran-with-commentaries%28yusuf-ali%29.pdf>.

Mpangilio wa kupokelewa na Mohamedi	Jina la Sura	Idadi ya Sura	Aina	Kumbuka
1	Al-Alaq (Tone la Damu)	96	Maka	
2	Al-Qalam (Kalamu)	68	Maka	Isipokuwa 17-33 and 48-50, Kutoka Madina
3	Al-Muzzammil (Iliyofungwa)	73	Maka	Isipokuwa 10, 11 and 20, kutoka Madina
4	Al-Muddaththir (iliyozungushwa)	74	Maka	
5	Al-Fatiha (Sura ya ufunguzi)	1	Maka	
6	Al-Lahab (Moto)	111	Maka	
7	At-Takwir (Iliyokunjwa)	81	Maka	
8	Al-A'la (Mwenye enzi)	87	Maka	
9	Al-Layl (Usiku)	92	Maka	
10	Al-Fajr (Mapambazuko)	89	Maka	
11	Ad-Dhuha (Nuru ya utukufu ya Asubuhi)	93	Maka	
12	Al-Sharh (Upanuzi wa matiti)	94	Maka	
13	Al-Asr (Nyakatti za umri)	103	Maka	
14	Al-Adiyat (Wale wakimbiao)	100	Maka	
15	Al-Kawthar (Utele)	108	Maka	
16	At-Takathur (Kupiga)	102	Maka	
17	Al-Ma'un (Msaada wa jirani)	107	Maka	1-3 Pekee toka Maka; zingine zote toka Medina
18	Al-Kafirun (Makafiri/wanaoikataa imani)	109	Maka	
19	Al-Fil (Tembo)	105	Maka	
20	Al-Falaq (Mchana)	113	Maka	
21	Al-Nas (Mwanadamu)	114	Maka	
22	Al-Ikhlash (Usafi wa imani)	112	Maka	
23	An-Najm (Nyota)	53	Maka	Isipokuwa 32, toka Madina
24	Abasa (Alishangaa)	80	Maka	
25	Al-Qadr (Usiku wa nguvu/heshima)	97	Maka	
26	Al-Shams (Jua)	91	Maka	
27	Al-Buruj (Nyota)	85	Maka	
28	Al-Tin (Mtini)	95	Maka	
29	Quraysh (Kabila la Quraysh)	106	Maka	
30	Al-Qari'a (Janga kubwa)	101	Maka	
31	Al-Qiyamah (Kufufuka)	75	Maka	
32	Al-Humazah (Mbukulia/Mchochezi)	104	Maka	
33	Al-Mursalat (Waliotumwa)	77	Maka	Isipokuwa 48, toka Madina
34	Qaf	50	Maka	Isipokuwa 38, toka Madina
35	Al-Balad (Mji)	90	Maka	
36	Al-Tariq (Nyota za usiku)	86	Maka	
37	Al-Qamar (Mwezi/mbalamwezi)	54	Maka	Isipokuwa 44-46, toka Madina
38	Sad	38	Maka	
39	Al-A'raf (Urefu)	7	Maka	Isipokuwa 163-170, toka Madina
40	Al-Jinn (Roho)	72	Maka	
41	Ya Sin	36	Maka	Isipokuwa 45, toka Madina
42	Al-Furqan (Kigezo)	25	Maka	Isipokuwa 68-70, toka Madina
43	Fatir (Muumbaji)	35	Maka	
44	Maryam (Mary)	19	Maka	Isipokuwa 58 na 71, toka Madina
45	Ta Ha	20	Maka	Isipokuwa 130 na 131, toka Madina
46	Al-Waqi'ah (Isiyoepukika)	56	Maka	Isipokuwa 81 na 82, toka Madina
47	Al-Shu'ara (Mashairi)	26	Maka	Isipokuwa 197 na 224-227, toka Madina
48	Al-Naml (Siafu)	27	Maka	
49	Al-Qasas (Simulizi)	28	Maka	Isipokuwa 52-55 toka Madina na 85 toka Juhfa wakati wa Hijra
50	Al-Isra' (Safari ya usiku)	17	Maka	Isipokuwa 26, 32, 33, 57, 73-80, toka Madina

51	Yunus (Yona)	10	Maka	Isipokuwa 40, 94, 95, 96, toka Madina
52	Hud (Kibanda cha Nabii)	11	Maka	Isipokuwa 12, 17, 114, toka Madina
53	Yusuf (Yusufu)	12	Maka	Isipokuwa 1, 2, 3, 7, toka Madina
54	Al-Hijr (Njia mwambani)	15	Maka	Isipokuwa 87, toka Madina
55	Al-An'am (Ng'ombe)	6	Maka	Isipokuwa 20, 23, 91, 93, 114, 151, 152, 153, toka Madina
56	As-Saffat (Wale walio na safu mbalimbali)	37	Maka	
57	Luqman	31	Maka	Isipokuwa 27-29, toka Madina
58	Saba (Sheba)	34	Maka	
59	Al-Zumar (Umati)	39	Maka	
60	Ghafir (Mwenye kusamehe)	40	Maka	Isipokuwa 56, 57, toka Madina
61	Fussilat (Fafanuzi)	41	Maka	
62	Al-Shura (Ushauri)	42	Maka	Isipokuwa 23, 24, 25, 27, toka Madina
63	Al-Zukhruf (Mapambo ya dhahabu)	43	Maka	Isipokuwa 54, toka Madina
64	Al-Dukhan (Moshi)	44	Maka	
65	Al-Jathiya (Kupiga magoti)	45	Maka	Isipokuwa 14, toka Madina
66	Al-Ahqaf (Njia ya vilima vya mchanga)	46	Maka	Isipokuwa 10, 15, 35, toka Madina
67	Adh-Dhariyat (Upepo uliotawanyika)	51	Maka	
68	Al-Ghashiyah (Matukio makubwa mno)	88	Maka	
69	Al-Kahf (Pango)	18	Maka	Isipokuwa 28, 83-101, toka Madina
70	Al-Nahl (Nyuki)	16	Maka	Isipokuwa aya tatu za mwisho toka Madina
71	Nuh (Nuhu)	71	Maka	
72	Ibrahim (Abraham)	14	Maka	Isipokuwa 28, 29, toka Madina
73	Al-Anbiya (Manabii)	21	Maka	
74	Al-Mu'minun (Waamini)	23	Maka	
75	Al-Sajdah (Uharibifu)	32	Maka	Isipokuwa 16-20, toka Madina
76	At-Tur (Mlima)	52	Maka	
77	Al-Mulk (Utawala)	67	Maka	
78	Al-Haqqah (Uhakika wa ukweli)	69	Maka	
79	Al-Ma'arij (Njia za kupanda)	70	Maka	
80	Al-Naba (Habari kuu)	78	Maka	
81	Al-Nazi'at (Wale watupao)	79	Maka	
82	Al-Infitar (Kuachilia mbali)	82	Maka	
83	Al-Inshiqaq (Kutupa mbali)	84	Maka	
84	Ar-Warumi (Warumi)	30	Maka	Isipokuwa 17, toka Madina
85	Al-Ankabut (Buibui)	29	Maka	Isipokuwa 1-11, toka Madina
86	Al-Mutaffifin (Kujihusisha na udanganyifu)	83	Maka	
87	Al-Baqara (Mtamba)	2	Madina	Isipokuwa 281 toka Mina wakati wa Hija ya mwisho
88	Al-Anfal (Nyara za vita)	8	Madina	Isipokuwa 30-36 toka Maka
89	Al-Imran (Jamaa ya Amramu)	3	Madina	
90	Al-Ahzab (Washirika)	33	Madina	
91	Al-Mumtahinah (Wale wanaotahini)	60	Madina	
92	Al-Nisa (Wanawake)	4	Madina	
93	Al-Zalزالah (Tetemeko la Ardhi)	99	Madina	
94	Al-Hadid (Chuma)	57	Madina	
95	Mohamedi	47	Madina	Isipokuwa 13, ilifunuliwa kipindi cha Nabii Hijrah
96	Al-Ra'd (Radi)	13	Madina	
97	Al-Rahman (Fadhili kuu)	55	Madina	
98	Al-Insan (Mwanadamu)	76	Madina	
99	At-Talaq (Talaka)	65	Madina	
100	Al-Bayyinah (Ushahidi wa wazi)	98	Madina	
101	Al-Hashr (Kusonga)	59	Madina	

102	Al-Nur (Nuru)	24	Madina	
103	Al-Hajj (Safari)	22	Madina	Isipokuwa 52-55, ilifunuliwa kati ya Maka na Madina
104	Al-Munafiqun(Unafiki)	63	Madina	
105	Al-Mujadilah (Mwanamke mwombaji)	58	Madina	
106	Al-Hujurat (Vyumba)	49	Madina	
107	At-Tahrim (Marufuku)	66	Madina	
108	At-Taghabun (Kubadilishana kukosa na kupata)	64	Madina	
109	Al-Saff (Safu ya vita)	61	Madina	
110	Al-Jumu'ah (Ijumaa)	62	Madina	
111	Al-Fath (Ushindi)	48	Madina	Ilifunuliwa wakati wa kurudi kutoka Hundaybiyya
112	Al-Ma'ida (Hifadhiwa)	5	Madina	Isipokuwa 3, ilifunuliwa Arafat kwenye Hija ya mwisho
113	Al-Tawbah (Toba)	9	Madina	Isipokuwa aya tatu toka Maka
114	Al-Nasr (Msaidizi)	110	Madina	Ilifunuliwa Mina kwenye Hija ya mwisho, lakini inajulikana kama sura ya Madina

ORODHA YA VYANZO

Kumbukumbu kamili ya bibliografia kwa nukuu kwenye maandiko yameonyeshwa kwenye bibliografia ya *Ukristo na Uislamu: Mambo Muhimu* ambayo yapo kwenye Wavuti ya ECLEA website at <http://www.eclea.net/courses.html#islam>.

MWANDISHI



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada yake ya B.A. kwa masomo ya sayansi ya siasa kutoka kwa Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, na taaluma ya heshima, mnamo mwaka wa 1974, baadaye akajumuika na Phi Beta Kappa kwa kuwa na heshima ya kijamii. Tena akapata J.D. kutoka kwa Shule ya Uanasheria cha Cornell, magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akawekwa kwenye mamlaka ya Kisheria ya Coif haki za heshima ya jamii. Akaitumia miaka iliyofuata 28 akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye akashirikiana na Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Alikuwa muumini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982.

Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake kwenye Theolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu au Master of Divinity kwenye chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Na sasa yeye ni mkurugenzi wa Huduma ya Kuwawezesha Viongozi wa Kanisa Afrika Mashariki (Equipping Church Leaders East Africa. "ECLEA"): www.eclea.com. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na tovuti hii, na barua pepe kwa anuani hii: jonathanmenn@yahoo.com.